ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

MHE. ZUBEIR ALI MAULID	-	SPIKA
1. Mhe. Mgeni Hassan Juma	-	Naibu Spika/ Nafasi za Wanawake
2. Mhe. Mwanaasha Khamis Juma	-	Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Chukwani
3. Mhe. Shehe Hamad Mattar	-	Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Mgogoni
4. Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	-	MBM/Makamu wa Pili wa Rais /Kiongozi wa Shughuli za Serikali/ Jimbo la Mahonda
5. Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu)	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Chwaka
6.Mhe. Haji Omar Kheri	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ/ Jimbo la Tumbatu
7. Mhe. Haroun Ali Suleiman	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora /Jimbo la Makunduchi
8. Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar/ Uteuzi wa Rais

9. Mhe. Dkt. Khalid Salum Mohamed	-	MBM/Waziri wa Fedha na Mipango /Jimbo la Donge
10. Mhe.Mahmoud Thabit Kombo	-	MBM/Waziri wa Afya/ Jimbo la Kiembesamaki
11. Mhe. Riziki Pembe Juma	-	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali / Nafasi za Wanawake
12. Mhe. Balozi Amina Salum Ali	-	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko Zanzibar/ Uteuzi wa Rais
13.Mhe. Balozi Ali Abeid Karume	-	MBM/Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji/ Uteuzi wa Rais
14. Mhe. Rashid Ali Juma	-	MBM/Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Jimbo la Amani
15. Mhe. Hamad Rashid Mohamed	-	MBM/Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Uteuzi wa Rais
16. Mhe. Maudline Cyrus Castico	-	MBM/Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto/ Uteuzi wa Rais
17. Mhe. Salama Aboud Talib	-	MBM/Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/ Nafasi za Wanawake
18. Mhe. Juma Ali Khatib	-	MBM/ Waziri Asiekuwa naWizara Maalum/Uteuzi wa Rais

19. Mhe. Said Soud Said	-	MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/ Uteuzi wa Rais
20. Mhe. Khamis Juma Mwalim	-	Naibu Waziri, Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora/ Jimbo la Pangawe
21. Mhe. Harusi Said Suleiman	-	Naibu Waziri wa Afya/ Jimbo la Wete
22. Mhe. Mmanga Mjengo Mjawiri	-	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali /Jimbo la Mkoani
23. Mhe. Mohamed Ahmada Salum	-	Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji / Jimbo la Malindi
24. Mhe. Chum Kombo Khamis	-	Naibu Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Nafasi za Wanawake
25. Mhe. Lulu Msham Abdalla	-	Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Nafasi za Wanawake
26. Mhe. Juma Makungu Juma	-	Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/ Jimbo la Kijini
27. Mhe. Abdalla Ali Kombo	-	Jimbo la Mwanakwerekwe
28. Mhe.Abdalla Maulid Diwani	-	Jimbo la Jang'ombe
29. Mhe. Ali Khamis Bakar	-	Jimbo la Tumbe

30. Mhe. Ali Salum Haji - Jimbo la Kwahani
31. Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata) - Jimbo la Kijitoupele
32. Mhe. Ame Haji Ali - Jimbo la Nungwi
33. Mhe. Amina Iddi Mabrouk - Nafasi za Wanawake
34. Mhe. Asha Abdalla Mussa - Jimbo la Kiwengwa
35. Mhe. Bahati Khamis Kombo - Jimbo la Chambani
36. Mhe. Bihindi Hamad Khamis - Nafasi za Wanawake
37. Mhe. Hamad Abdalla Rashid - Jimbo la Wawi
38. Mhe. Hamida Abdalla Issa - Nafasi za Wanawake
39. Mhe. Hamza Hassan Juma - Jimbo la Shaurimoyo
40. Mhe. Hassan Khamis Hafidh - Jimbo la Welezo
41. Mhe. Hidaya Ali Makame - Nafasi za Wanawake
42. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu (Bhaa) - Jimbo la Mtoni
43. Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Jimbo la Paje
44. Mhe. Khadija Omar Kibano - Jimbo la Mtambwe
45. Mhe. Machano Othman Said - Jimbo la Mfenesini
46. Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi Makoti - Jimbo la Mtopepo
47. Mhe. Makame Said Juma - Jimbo la Kojani
48. Mhe. Maryam Thani Juma - Jimbo la Gando
49 Mhe. Masoud Abrahman Masoud - Jimbo la Bububu
50. Mhe. Mihayo Juma N'hunga - Jimbo la Mwera
51. Mhe. Miraji Khamis Mussa - Jimbo la Chumbuni
52. Mhe. Moh'd Mgaza Jecha - Jimbo la Mtambile
53. Mhe. Mohamed Said Mohamed - Jimbo la Mpendae
54. Mhe. Mohammedraza Hassanaali Mohamedali- Jimbo la Uzini
55. Mhe. Mtumwa Peya Yussuf - Jimbo la Bumbwini
56. Mhe. Mtumwa Suleiman Makame - Nafasi za Wanawake
57. Mhe. Mussa Ali Mussa - Jimbo la Ole
58. Mhe. Mussa Foum Mussa - Jimbo la Kiwani
59. Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa - Nafasi za Wanawake
60. Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis - Nafasi za Wanawake
61. Mhe. Dkt Mwinyihaji Makame Mwadini - Jimbo la Dimani
62. Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy- Jimbo la Chaani
63. Mhe. Nassor Salim Ali - Jimbo la Kikwajuni
64. Mhe. Omar Seif Abeid - Jimbo la Konde
65. Mhe. Panya Ali Abdalla - Nafasi za Wanawake

66. Mhe. Rashid Makame Shamsi	-	Jimbo la Magomeni
67. Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa	-	Nafasi za Wanawake
68. Mhe. Said Omar Said	-	Jimbo la Wingwi
69. Mhe. Said Hassan Said	-	Mwanasheria Mkuu
70. Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma	-	Nafasi za Wanawake
71. Mhe. Salma Mussa Bilal	-	Nafasi za Wanawake
72. Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	-	Nafasi za Wanawake
73. Mhe. Shaib Said Ali	-	Jimbo la Chonga
74. Mhe. Shamata Shaame Khamis	-	Jimbo la Micheweni
75. Mhe. Simai Mohammed Said	-	Jimbo la Tunguu
76. Mhe. Suleiman Makame Ali	-	Jimbo la Ziwani
77. Mhe. Suleiman Sarahan Said	-	Jimbo la Chakechake
78. Mhe. Tatu Mohamed Ussi	-	Nafasi za Wanawake
79. Mhe. Ussi Yahya Haji	-	Jimbo la Mkwajuni
80. Mhe. Viwe Khamis Abdalla	-	Nafasi za Wanawake
81. Mhe. Wanu Hafidh Ameir	-	Nafasi za Wanawake
82. Mhe. Yussuf Hassan Iddi	-	Jimbo la Fuoni
83. Mhe. Zaina Abdalla Salum	-	Nafasi za Wanawake
84. Mhe. Zulfa Mmaka Omar	-	Nafasi za Wanawake

Ndugu Raya Issa Msellem	-	Katibu wa Baraza la Wawakilishi

Kikao cha Nane - Tarehe 31 Mei, 2016

(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Spika (Zubeir Ali Maulid) alisoma dua

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Spika, naomba kuweka hati mezani inayohusiana na suala la Hotuba ya Makadirio na Mapato ya Matumizi ya Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Mhe. Spika, naomba kuwasilisha.

Mhe. Simai Mohammed Saidd (Kny. Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa): Mhe. Spika, ahsante, kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha hati mezani ya Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kuhusu Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa mwaka 2016/2017. Naomba kuwasilisha.

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 79

Wasanii wa Michezo ya Asili Kutokualikwa katika Tamasha la Nchi za Jahazi

Mhe. Suleiman Sarahan Said – Aliuza:-

Serikali kupitia Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo kwa muda mrefu sasa imekuwa ikiunga mkono Tamasha la Nchi za Jahazi (*ZIFF*), linalofanyika katika viwanja vya Ngome Kongwe ambapo sehemu kubwa ya tamasha hilo huchukuliwa na wasanii wa Kizazi kipya na kuziacha kabisa ngoma za asili na michezo mengine ya kienyeji, ikiwemo mchezo wa ng'ombe hatimae kupelekea kutotambulika katika ramani ya utamaduni wa hapa Zanzibar.

a) Kuna utaratibu gani wa upangaji wa washiriki wa pamoja na sanaa zinazohitajika kuonyeshwa katika tamasha hilo la *ZIFF*.

b) Serikali ina mpango gani wa kizifufua ngoma na michezo ya asili ikiwemo mchezo wa ng'ombe ili irudi hadhi na haiba yake kama pale zamani.

Mhe. Naibu ya Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwanza na mimi nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwenye rehema na kutuamsha salama na kufika hapa katika Baraza lako tukufu.

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 79 lenye vipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kabla ya kumjibu Mhe. Suleiman Sarahan, naomba kutoa maelezo ya kina.

Mhe. Spika, serikali kupitia Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo kwa muda mrefu sasa imekuwa ikiunga mkono Tamasha la nchi za Jahazi (*ZIFF)* linalofanyika katika viwanja vya Ngome Kongwe ambapo sehemu kubwa ya tamasha hilo huchukuliwa na wasanii wa kizazi kipya na kuziacha kabisa ngoma za asili na michezo mingine ya kienyeji ukiwemo mchezo wa ng'ombe hatimaye kutotambulikana katika ramani ya utamaduni hapa Zanzibar.

Mhe. Spika, Tamasha la *ZIFF* ni miongoni mwa matamasha yaliyoanzishwa na kusajiliwa kwa mujibu wa taratibu tulizojiwekea. *ZIFF* ni miongoni mwa taasisi binafsi (*NGO,s*) ambazo zinaendesha shughuli zake kama zilivyo "*NGO,s*" nyengine, tofauti iliyopo ni kwamba taasisi hii inajishughulisha sana na maonesha ya Sanaa na Utamaduni.

Mhe. Spika, hata hivyo, miongoni mwa majukumu yanayotekelezwa na wizara yangu ni kuzikaguwa na kuzitolea maelekezo kazi zote zinazokusudiwa kuoneshwa kabla ili kuondoa uwezekano wa kuvunjwa kwa maadili, pamoja na hatua hiyo tumekuwa karibu sana na watendaji wa *ZIFF* ili kuwaelekeza umuhimu wa kuwashirikisha wasanii wetu na kazi zao, hatua mbayo imekuwa ikitekelezwa ikiwa ni pamoja na kushirikisha michezo mbali mbali ikiwemo mchezo wa ng'ombe, resi za ngarawa na hata michezo ya watoto ambayo ni yetu na ni ya kiasili.

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako sasa naomba nimjibu swali lake Mhe. Mwakilishi.

(a) Kuhusu upangaji wa washiriki wa tamasha hilo kazi hii inafanywa na uongozi wa *ZIFF* ambapo sanaa zetu zikiwemo za ngoma na michezo hupata nafasi hapa Unguja na kule Pemba kwa mujibu wa hali inavyo aruhusu.

(b) Mhe. Spika, miongoni mwa hatua zilizochukuliwa na zinazotarajiwa kuendelezwa na wizara, ni pamoja na kuhakikisha kwamba vikundi vyetu vya michezo ya asili na sanaa ambavyo vimo katika maeneo mbali mabli vinarejeshwa na kuendelezwa kwa lengo la kukuza, kuimarisha na kuuendeleza utamaduni wetu.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Mhe. Spika, namshukuru Mhe. Naibu Waziri, kwa majibu yako mazuri, nina swali moja la nyongeza lenye (a) na (b).

(a) Kwa kuwa kwa wenzetu kama Spain kuna mchezo wa ng'ombe unaoitwa *bullfighting,* lakini mchezo huu uko tofauti sana na mchezo wetu wa ng'ombe ulioko kisiwani Pemba. Je, serikali haioni umuhimu zaidi wa kukuza, maana yake mchezo huu unaonekana sana uko Pemba. Je, na Unguja hauonekani umuhimu wa kuanzishwa hapa ikawa kama ni kioo katika mchezo wetu wa ng'ombe baina ya Pemba na Unguja.

(b) Ni kwamba ukiachia mchezo kama wa ng'ombe kuna michezo ya Kelbu Taaban, Msewe, Kumbwaya, Gonga na hili tamasha mara zote linamalizia hapa Unguja. Je, serikali ina mpango wa kuianzisha ile *ZIFF* ikaanzia Pemba ikaja ikafanya majumuisho Unguja.

Mhe. Naibu ya Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo: Mhe. Spika, kwanza nakubaliana na Mhe. Mwakilishi kwamba, kuna umuhimu zaidi wa kuanzishwa tamasha hili au michezo hii ya mchezo wa ng'ombe kwa kisiwa cha Zanzibar.

(a) Nataka nimuahidi kwamba, serikali kupitia Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo nalipokea na unapokewa ushauri wake na hili tutalisimamia. Sisi ndio wasimamizi naahidi kwamba tutasimamia na tutatafuta zile sehemu ambazo zilikuwa zinachezwa mchezo huu kwa mfano Pemba na tuwafundishe na wenzetu wa Unguja kama ulikuwa haupo basi tuuanzishe ili na wao tuweze kuwa pamoja kwa kuimarisha tamasha hili la *ZIFF*.

(b) Mhe. Spika, pia serikali ina mpango wa kufanya majumuisho ya tamasha hili, kwa sasa hivi Mheshimiwa kasema kwamba mara nyingi tamasha hili linakuwa linafanywa huku Unguja, lakini nimuahidi kwamba kupitia

uongozi mpya wa Wizara ya Habari tutafanya hivyo na ushauri wake naupokea na kuufanyia kazi. Ahsante sana.

Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis: Mhe. Spika, ahsante sana, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri, mimi nina swali moja la nyongeza.Wizara kwa kushirikiana na Kamisheni ya Utamaduni ilitoa elimu katika wilaya ngapi Unguja na Pemba ili kuelimisha juu ya kudumisha utamaduni wa ngoma za asili.

Mhe. Naibu ya Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo: Mhe. Spika, serikali kupitia Wizara ya Habari imetoa mafunzo kwa wilaya zote za Unguja na Pemba kwa kuwapa elimu wananchi wetu juu ya tamasha hili la *ZIFF*. Mfano wa haya wizara imeandaa ziara mbali mbali kwa mfano Kojani, Maziwa Ng'ombe, Kiuyu na kwengineko na hili nimhakikishie Mhe. Mwakilishi kwamba, serikali iko pamoja na wananchi wake na Taifa kwa jumla kwa kuimarisha matamasha yetu.

Mhe. Simai Mohammed Said: Mhe. Spika, ahsante, kwa kuwa ahadi ni deni na serikali imekuwa inapigia kelele sana na kuimba Wimbo wa Taifa kuhusiana na masuala ya tamasha kwamba kuna umuhimu wa kuyasaidia. Swali, ni lini serikali itaji-*commit* kuleka Sheria ya kuanzisha Mfuko wa Utamaduni hapa ili sisi Waheshimiwa Wawakilishi tuweze kuujadili. Hiyo ni (a).

(b) Ni vikundi vingapi vya sanaa kutoka visiwa vyetu vya Zanzibar vimeweza kushiriki katika matamasha mbali mbali ya kimataifa au ni vipi. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Spika: Mheshimiwa, jibu swali (a) kwa sababu swali (b) linahitaji takwimu.

Mhe. Naibu ya Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo: Mhe. Spika, (a) Kwanza nakubaliana na Mhe. Mwakilishi, juu ya suala lake alilolitoa na pia nipokee kwamba ni ushauri anatutaka serikali kupitia Wizara ya Habari tuweke mpango maalum, yaani tuunde sheria kuipitisha humu ndani ya Baraza ili tuijadili na tuweke sheria hii kwa kusimamia haya matamasha. Hili nalipokea kwa upande wa wizara na serikali pia, tutalifanyia kazi kwa kukaa pamoja tukishirikiana pamoja na nyinyi Waheshimiwa Wawakilishi wenzangu tuitunge hii sheria na kuileta hapa, kuijadili, hatimaye itumike kama zinavyotumika sheria nyengine. Ahsante sana.

Nam. 42

Matatizo ya Umeme Mdogo Makunduchi Tangi la Maji

Mhe. Ali Suleiman Ali (Kny. Mhe. Jaku Hashim Ayoub) - Aliuliza:-

Wananchi wa Makunduchi Tangi la Maji kwa muda mrefu wamekuwa wakipata umeme ukiwaka chini ya kiwango (*low voltage*) na kuwapa wananchi wakati mgumu wakati wanalipia kama wananchi wengine, wakati shirika linalifahamu lakini hakuna hatua zilizochukuliwa hadi leo hii.

a) Je, lini shirika litaondoa tatizo hili kwa wananchi hao ili nao wapate huduma hiyo kama sehemu nyengine.

b) Je, shirika limewafidia vipi wananchi walioathirika na tatizo hilo kutokana na umeme wanaoupata kuwa hauna uwezo wa kutumika katika shughuli za uwezeshaji au uhifadhi.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 42 lenye vipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kabla ya kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake naomba kutoa maelezo machache kama ifuatavyo:

Lengo la Shirika la Umeme ni kuhakikisha kuwa wananchi wote wanapata huduma ya umeme yenye kuridhisha. Kwa kawaida tatizo la kuwepo umeme mdogo linatokana na ukuaji wa miji na vijiji pamoja na mwamko wa wananchi katika utumiaji wa umeme, hali inayosababisha kuzidiwa kwa *transformer* au miundombinu yake katika kipindi kifupi baada ya kuwekwa. Katika kutatua matatizo kama hayo, wizara yangu kupitia Shirika la Umeme huchukua hatua mbali mbali kama vile kubadilisha *transformer* au kuongeza njia za kusambazia umeme.
Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo sasa naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 42 lenye (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, tatizo la umeme mdogo Makunduchi Tangi la Maji limesawazishwa kwa kubadilisha *transformer* iliyozidiwa ya 50*kVA* na kuweka *transformer* yenye uwezo mkubwa ya 100*kVA*. Hivyo, kama bado yupo

mwananchi anaendelea kupata umeme mdogo tunamuomba atoe taarifa katika kituo chetu cha huduma kwa wateja kiliopo hapo hapo Makunduchi.

(b) Mhe. Spika, kwa kawaida Shirika la Umeme linao utaratibu wa kuwalipa fidia kwa wananchi wanaoharibikiwa na vifaa vyao kunakosababishwa na hitilafu za umeme kutoka katika miundombinu ya shirika. Lakini shirika halilipi fidia kwa wananchi wanaopata umeme mdogo au wanapokosa huduma ya umeme.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri, kwa ruhusa yako naomba kuuliza swali la nyongeza. Kwanza nampongeza Mhe. Naibu Waziri kwa hatua kubwa ya kutuhakikishia katika Baraza hili kwamba tatizo la kukatika umeme au *low voltage* katika sehemu ya Makunduchi limeondoka. Lakini swali langu lipo hapa.

Kwa kuwa tatizo hili linawagusa wananchi wa Kijitoupele Melinne, Uzi, *transformer* ambayo mara kwa mara huwa umeme wake unakuwa mdogo na kukatika mara kwa mara. Je, Mhe. Naibu Waziri, hatua gani itachukuliwa juu ya kuliondosha tatizo hili kama lilivyoondoka la Makunduchi.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata), swala lake la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, ni wajibu wa shirika kufanya kila linalowezekana kuhakikisha kwamba wananchi wanangara na inapotokezea hitilafu ama haja ya kubadilishwa kitu tunaomba taarifa tuletewe za uhakika na kwa haraka. Basi kwa hiyo nimuombe tukimaliza tuwasiliane ili kufatia na wataalamu tuone tunafanyaje, *inshaallah*.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Katika jibu lako mama ulizungumza kwamba Shirika la Umeme limelipa fidia wananchi walioharibikiwa na vifaa vyao kwa sababu ya matatizo ya umeme.

(a) Ni wananchi wangapi wamefaidika na fidia hiyo kutoka Shirika la Umeme.

(b) Uthibitisho gani ambao unafanya utafiti kwamba hawa ni kweli wameharibikiwa kwa sababu ya matatizo ya umeme.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Spika, kuhusu takwimu tutakuletea kwa maandishi na kuhusiana na njia gani tunatumia mimi naomba hili tuliache kwa sababu itakavyokuwa tumelitoa wale wajanja watatafuta njia nyengine za kusingizia. Hili naomba libakie kwenye shirika mbinu tunazotumia katika kuhakiki kujua kwamba kweli huyu kapata athari kutokana na miundombinu yetu ya umeme. Ahsante. (*Makofi*)

Mhe. Simai Mohamed Said (Mpaka basi): Ahsante Mhe. Spika, kwa kuwa masuala ya *low voltage* yanatokana na matumizi katika maeneo haya ya kijiji na maeneo tofauti kwenye kanda zetu ambazo hutumika katika mahoteli na biashara ya utalii.

Ni utaratibu gani unaotumika kwa wizara yako kwa kupita na shirika ili kuweza kuthibitisha kwamba matumizi yanapoongezeka hayaathiri wananchi katika vifaa vyao majumbani mwao na katika pale pia panapotokezea na ujenzi katika maeneo tofauti nyumba kuongezeka za makaadhi ili wizara iwe na taarifa kamili pamoja na taarifa husika. Ahsante.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Spika, Wizara yangu kupitia shirika tunasisitiza wananchi wasifanye hila, yaani wasiibe umeme, kusudi wanapofanya wataalamu wetu wanapata taarifa sahihi na kujua hapa panahitaji ongezeko la aina gani. Nadhani nimekujibu. Ahsante sana. (*Makofi*)

Nam. 57

Ahadi za matengenezo ya barabara ya Buyu na Shakani

Mhe. Mwanaasha Khamis Juma: - Aliuliza:-

Wananchi wa Buyu walipopewa ahadi na Rais wa Awamu ya Sita ya kutengenezewa barabara ya Chukwani Buyu na kwa kuwa Waziri dhamana wa wakati huo aliahidi mbele ya Rais na wananchi wa Buyu kuwa barabara hiyo ingetengenezwa ndani ya wiki mbili, na ahadi hiyo hadi leo haijatekelezwa. Aidha, matengenezo ya barabara ya Shakani ambayo inaleta shida kwa wananchi wanaotokea Chukwani Buyu kuelekea Shakani mzunguko unakuwa mkubwa.

a) Je, ile ahadi ya Serikali kutengeneza barabara ya Chukwani Buyu kwa muda wa wiki mbili, itatekelezwa lini tena wakati wiki mbili zimeshamalizika na sasa ni miaka mingi.

b) Je, mpango gani madhubuti wa kutengenezwa barabara ya Shakani kupitia Kisauni ili kuwaondolea usumbufu wananchi wa Shakani.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji - Alijibu:-
Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 42 lenye vipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, barabara ya Chukwani – Buyu ni miongoni mwa barabara zinazoshughulikiwa na Halmasharui ya Wilaya ya Magharibi 'B' na kwa taarifa, mnamo miaka ya 2000 barabara hiyo ilijengwa kwa kiwango cha kifusi na mradi wa *TASAF* kutoka Chukwani hadi Buyu (Pwani). Mnamo mwaka 2014, Wizara yangu iliifanyia matengenezo makubwa sehemu ya barabara hiyo kwa kuiwekea lami kiasi cha mita 700 kwa kutumia fedha za Mfuko wa Barabara (*ZRF*).Hata hivyo, matengenezo hayo hayakuweza kuendelea zaidi kutokana na kwamba barabara hiyo imepita kwenye eneo la hifadhi ya kiwanja cha ndege cha Kimataifa cha Abeid Amani Karume na ndiyo maana kuna baadhi ya nyumba zilitiwa alama kwa ajili ya kupisha eneo hilo.

(b) Kama ilivyo barabara ya Chukwani – Buyu, barabara ya Shakani ni miongoni mwa barabara zinazosimamiwa na Halmashauri ya Wilaya ya Magharibi 'B' chini ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ. Kuanzia mwaka wa fedha 2015/16, Mfuko wa Barabara umeanza kuitengea fedha Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kwa ajili ya matengenezo ya barabara zilizo chini ya usimamizi wake zikiwemo za Halmashauri na tayari imeshaanza kuzitumia fedha hizo kwa miradi mbali mbali ya matengenezo ya barabara. Namshauri Mhe. Mjumbe, awasiliane na Halmshauri yake ya Wilaya ya Magharibi 'B' ili barabara hiyo iingizwe kwenye bajeti ya matengenezo husika.

Mhe. Mwanaasha Khamis Juma: Mhe. Spika, kwa kuwa nimemuuliza Mhe. Waziri, tayari barabara ya Buyu na Chukwani iliahidiwa na Rais wa Awamu ya Sita kuwa itafanyiwa matengenezao na ahadi hiyo imetolewa mbele ya wananchi wa jimbo la Chukwani wakaazi wa Buyu.

(a) Je ni lini ahadi ile iliyotolewa na Mhe. Rais wa Awamu ya Sita itatekelezwa

(b) Kuna mipango gani madhubuti ambayo itatengeneza barabara ya Shakani kupitia Kisiuni ili kuwaondolea usumbufu wananchi wa Shakani. Je, ni muda gani na wakati gani barabara ile ya Shakani, japo kuwa amenambia Mhe. Naibu Waziri, majibu yake kama kuna uwanja wa ndege lakini bado barabara ile watu wanaihitaji na wanapata usumbufu sana wa jimbo la Chukwani na ikizingatiwa wizara yake imo ndani ya jimbo langu la Chukwani na Afisi yake iko hapo namuomba Mhe. Waziri anihakikishie wakati gani na muda gani matengenezo ya barabara ile yatafanyika.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji:

(a) Napenda kukubaliana na yeye kwamba sisi hatuna kawaida ya kupinga ahadi zinazotolewa na viongozi wetu wa serikali. Lakini vile vile tunazingatia taratibu na sheria za nchi kwamba *master plan* ya uwanja wa ndege na hii tungependa ifahamike kwamba sisi hivi sasa tunataka tuwe na Uwanja wa Kimataifa ili tupate watalii wengi zaidi na vile vile kuchukuwa mizigo mingi na kusafirisha mizigo mingi.

Sasa tatizo hapa limeonekana kwamba iwapo tutakuja kuijenga njia ile na baadae iwapo Uwanja wa Ndege tutakapoupanua na zile nyumba kuondoshwa, maana yake kwamba barabara ile haitokuwa na faida kwani itakuwa haipitiwi na watu.

Lakini licha ya hivyo, namuahidi Mhe. Mwanaasha Khamis Juma, tutakaa nae ili kuangalia njia gani tunaweza kulitatua tatizo hili. Lakini kwa hivi sasa barabara ile inapitika vizuri sana kwa sababu ipo katika hali nzuri na pale ambapo kuna matatizo au sehemu korofi basi huwa tunazirekebisha.

(b) Napenda kumuhakikishia kwamba Mhe. Mwanaasha Khamis Juma, sisi wakati wowote tunafanya kazi kwa karibu na Wizara ya Nchi, Afisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ. Kwa vile napenda kumuhakikishia kwamba Mhe. Waziri hivi juzi tu alikutana na viongozi wa Mfuko wa barabara na akawataka kwamba barabara zote zile ambazo zina umuhimu ahakikishe kwamba zinatengenezwa kwa kiwango cha lami, na sisi tutaangalia uwezekano wa barabara yake hiyo vipi tuifanyie kazi na kama itaonekana inakipaumbele hatutoacha kuchukuwa hatua zinazostahiki. (*Makofi*)

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Mhe. Spika, kutokana na mradi mkubwa wa ujenzi wa barabara Mwanakwerekwe Fuoni na imekuwa kipindi kirefu toka ianze mradi ule kwa sababu tuliahidiwa kwamba mwezi wa tano barabara ile itakamika, kutokana na usumbufu wanaoupata watumizi wa barabara ile kama mavumbi na kuzalisha wagonjwa wengi wa vifua.

(a) Je, serikali inatuhaidi nini kwamba ile barabara iliyokuwa tukabidhiwe ndani ya miezi mitano.

(b) Je, serikali haoni sababu ya kumwagilia maji japo mara mbili kwa wiki katika kuondoa matatizo yale ya vumbi.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji:

(a) Ni kweli kabisa barabara ile hivi sasa imesita ujenzi wake kwa sababu kuna taratibu zetu maalum tunazozifanya ili kutafuta mkandarasi wa kiimalizia ile kwa kiwango cha lami na napenda kumuarifu kwamba hivi sasa tumeshafikia hatua ya mwisho ili baadae mkandarasi huyu aanze kazi mara moja na mimi kama nilivyose katika masuala yangu ya kipindi kilichopita kwamba tuliweka katika mpango wetu kwamba barabara ile hadi ikifika mwaka 2016 Disemba iwe tayari imeshakamilika. Bado tuna muda wa kuikamilisha kwa wakati na vile vile naomba kuwaomba radhi sana wananchi kwa usumbufu wanaoupata hivi sasa wa mavumbi, lakini wawe na ustahamilivu kama ilivyokuwa barabara za Pemba hasa Ole na Konde zile zote ilikuwa wakati huo zina matatizo lakini baadae wananchi wamekuja kufurahia, basi tustahamilieni kwa hilo.

(b) Suala lake la pili kusema la ukweli tunalichukuwa na tutalaifanyia kazi kwa haraka ili kuondosha matatizo ya vumbi yalioko hivi sasa.

Mhe. Simai Mohamed Said (Mpaka basi): Mhe. Spika, kwa kuwa wananchi wangu wa kisiwa cha Uzi miaka nenda rudi imekuwa maji yakijaa huwa wanavuka kwa kutumia boti zao za asili na mitumbwi. Lakini maji yanapotoka ile barabara huwa unaweza kuendesha gari mpaka kufika kisiwa cha Uzi. Lakini ile barabara huwa inahitaji kuwekewa kokoto na kuhakikisha kwamba inashughulikiwa kila baada ya muda.

Ni utaratibu gani serikali yako imejipangia kuhusiana na barabara ya kutoka Uzi mpaka Unguja Ukuu ili wananchi waweze kufahamu kwamba lao ni moja ni hili kwamba hawatopata daraja lakini barabara hii itakuwa inashughulikiwa

kwa gharama za serikali ili wajue wao maisha yao wanakwenda nayo vipi. Ahsante.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Spika, kusema la ukweli barabara ile mimi naijua vizuri kwa sababu na mimi ni mdau wa barabara ile. Kwa hiyo, napenda kwanza kumpongeza kwa juhudi zake anazozichukuwa katika kuhakikisha kwamba barabara ile anapunguza ule ukali wa mawe ikisha watu wanaweza kupita na gari zao kila wakati hasa pale maji yanapotoka ili kwenda katika shughuli zao na makaazi yao yanayoishi kule Uzi hadi Ngambwa.

Kwa hiyo, mimi napenda kumwambiwa kwamba ile barabara iko katika Halmashauri ya Wilaya ya kati, lakini tutahakikisha kwamba tunashirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Kati kuzifanyia ukarabati zile sehemu korofi hasa pale kwenye mawe mengi pale ili tupite vizuri na barabara ile itumike wakati wowote na magari yasipate pancha. Ahsante sana Mhe. Naibu Waziri.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, kipindi cha maswali kimekwisha na kwa bahati nzuri hakuna hata tangazo la wageni. Kwa hivyo, tunaendelea.

Utaratibu

Mhe. Mohamed Said Mohamed: Mhe. Spika, nimesimama kwa kifungu cha 42. Mhe. Spika, Kanuni za Baraza la Wawakilishi toleo la mwaka 2012, naomba kuwasilisha hoja ya kujadili jambo la dharura kwa kutumia Kanuni ya 42 na Kanuni zake ndogo kama zifuatazo (1,3,4,5,9,10), toleo la 2012.

Mhe. Spika, hoja yangu inahusu muelekeo wa uvunjifu wa amani kufuatia kitendo cha Katibu Mkuu wa Chama cha Wananchi CUF kuwahamasisha wananchi wa Zanzibar kushiriki katika mikutano mbali mbali na sheria ya uvunjifu wa amani hapa nchini.

Mhe, Spika, kwa kuwa Katibu wa Chama cha Wananchi CUF amekuwa na tabia ya kupita majimboni na matawini mwa chama chake na kuwataka wananchi wa chama hicho kuonesha vitendo vya kutokuitambua serikali yao ikiwa ni pamoja na kuwataka wasilipe kodi yoyote wanayotozwa na serikali;

Na kwa kuwa wananchi wamechukuwa vitendo na maelezo hayo ya chama chao na hatimae wanabagua wananchi wa Zanzibar hasa wa Chama cha Mapinduzi kwa kuzingatia, kutokuwauzia bidhaa mbali mbali;

Na kwa kuwa vitendo vya Katibu Mkuu wa chama hicho vinawapelekea wananchi wa chama chake kuhujumu mali mbali mbali ikiwemo mikarafuu na mali nyengine za serikali pamoja na majengo ya chama;

Na kwa kuwa vitendo hivyo Katibu Mkuu wa Chama hichi ameanzisha kisiwani Pemba kwa muda wa mwezi mmoja sasa;

Na kwa kuwa katika mkutano wake wa Jumapili wa tarehe 29 katika Jimbo la Donge na majimbo mengine ya Bumbwini Kaskazini. Katibu wa chama hicho amewakataka wananchi wa chama wasishirikia katika shughuli zozote za maziko, harusi na shughuli nyengine za kijamii dhidi wananchi wanaoaminika na wanachama wa Chama cha Mapinduzi. Hali inaonesha wazi mgawanyiko wa kisiasa nchini kwetu na kupelekea wananchi wetu kufanyiwa hujuma mbali mbali inaoneshwa na ubaguzi wa misingi ya kisisa;

Ni vyema Mhe. Spika, naamini kwa kuwa kuna haja kubwa hii hoja kuijadili Baraza lako tukufu kuonesha vitendo visivyokuwepo hapa nchini huku ikielekea kuacha jambo hilo pasipo kuchukuliwa hatua yoyote na serikali, inatupelekea jambo hili kuweko na mashaka makubwa majimboni mwetu, lakini vile vile katika serikali hii yetu;

Sasa ningeomba Baraza lako tukufu liweke kanuni kando na kutupa muda wa saa moja ili kuona tunajadili Baraza hili tukufu la wananchi wote ambayo majimbo yote yako hapa tunajadili kwa saa moja ili kuona tunapata mustakabali mzuri; (*Makofi*)

Lakini vile vile tuone serikali inachukuwa juhudi gani za kuweza kukomesha vitendo hivyo, ukizingatia mwezi wa Ramadhani umekaribia na waumini wengi wanataka kufanya sala zao na ibada zao.

Mhe. Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

Mhe. Spika: Ahsante sana Mheshimiwa, jambo unalolileta wala halihitaji kuwekwa kando kanuni kwa sababu tayari kanuni imeshalia- *accommodate*. Kanuni ya 42, hoja ya kujadili jambo kwa dharura, lakini fasili ya tano inasema endapo Spika ataliona jambo hilo ni la dharura na ni la muhimu kwa umma ataruhusu hoja hiyo itolewe na mjadala juu ya hoja utaendelea kwa muda usiozidi saa moja.

Kwa vile Mheshimiwa tayari umeshaeleza ule msingi wa jambo lenyewe na jambo lenyewe kweli linaonekana kweli ni la dharura na linahitaji lijadiliwe.

Kwa hiyo, kwa mujibu wa kanuni ya 42, fasili ya 5 nitaruhusu jambo hili tulijadili kwa muda usiozidi saa moja. Kwa maana hiyo kwa bahati nzuri pia nina majina ambayo tayari yameshakuja juu ya wachangiaji wa hiyo hiyo hoja na ili tusipindukie hiyo saa moja basi, nitaomba kuyataja haya majina ili wahusika wajijue halafu nitawasimamisha mmoja baada ya mwengine wachangie kabla sijamwita Mhe. Waziri ambaye Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais ili naye aje ahitimishe hii hoja, kabla sijakuita mwenyewe kwa kumalizia.

Wachangiaji nilionao kwanza nitamwita Mhe. Suleiman Sarahani Said wa Chake Chake, Mhe. Ussi Yahya Haji, Mhe. Miraji Khamis Mussa na baadae ataanza Mhe. Said Soud Said katika Mawaziri kabla sijamwita Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais. Naomba sasa Mhe. Suleiman Sarahani.

Mhe. Suleiman Sarahani Said: Dakika ngapi Mhe. Spika?

Mhe. Spika: Muda kila ukiwa mfupi itakuwa nzuri zaidi ili kuwapa nafasi wengine Mheshimiwa, kwa kadri itakavyowezekana. Dakika kumi au kumi na tano isizidi.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Ninakushukuru Mhe. Spika, kwa hoja ambayo imeletwa ili tuweze kuiangalia kwa kina, nini athari ambazo zitaleta katika nchi yetu.

Mhe. Spika, kwa kweli hii hali tuliona kama ni masihara hasa kule Kisiwani Pemba. Chanzo cha habari hizi baada ya uchaguzi wa tarehe 20 kumalizika, hali ya nchi ilikuwa shwari sana. Na kwa kweli watu wote walikuwa wanashirikiana katika mambo yao yote na kila hali inapoendelea ilikuwa bado msisitizo wa amani unaendelea na hali ilikuwa nzuri sana.Lakini kulianza mambo ya chokochoko madogo madogo hasa Misikitini, maeneo ya maduka, maeneo ya magari, maeneo ya kuvushana ambayo kama eneo langu la Chake Chake Mhe. Spika, jambo lile lilimalizika katika hali ya utaratibu kabisa na watu wote walielewana.

Lakini Mhe. Spika, hali ilionekana kwamba haijasaidia kuikomoa serikali au kuwakomoa watu. Mhe. Spika, nataka nisema kwamba wakati wa uchaguzi kuanzia Mhe. Rais, Tume ya Uchaguzi, watu wote uchaguzi huu ulipoahirishwa, kila mtu alipewa taarifa ya kutosha kwamba uchaguzi baada ya tarehe 25 ya Oktoba, 2015 uchaguzi utakuwa lini. Na ilikuwa ni kelele nyingi huku nyuma uchaguzi lini mpaka tarehe ikatolewa na Tume, ikaambiwa tarehe 20 Machi, 2016 tukafanya uchaguzi.

Mhe. Spika, viongozi wa Chama cha Upinzani kama *CUF* na vyama vyengine vilianza kutoa hoja zao za msingi kwa chama chao cha kusema wao hawatoshiriki au hawamo au hawahusiki. Walinasihiwa vya kutosha Mhe. Spika, ili kuhakikisha hili jambo kwamba linafanyika katika amani na utulivu na watu wote washiriki. Watu wale walinasihiwa sana. Baadhi ya vyama vilikubali kuingia, baadhi ya vyama havikukubali kuingia lakini hiyo ni shauri yao na itikadi yao, haiwezi kuingiliwa na serikali wala Tume. Yale ni mashauri yao.

Mhe. Spika, kulikuwa na tashtiti nyingi zilikuwa zikitokea ambapo wenzetu labda hawakujifahamu kama zinaweza zikawaathiri. Walikuwa wakitwambia sana kwamba mutapiga peke yenu, mwaka huu sijui uchaguzi haupo. Kila masuala mengi mengi yalikuwepo. Tuliwanasihi sana wenzetu waingie katika uchaguzi ili tuwe salama na usalimini tufanye kazi zetu.

Mhe. Spika, ninataka nijitolee mfano kama mimi. Mimi nishafanya uchaguzi huu mara nne ambao ninapigwa na chini na wenzangu wa *CUF*, wala sina kiburi nao, wala sina chochote. Na nilikuwa ninashirikiana naye, huyo Mwakilishi wangu niliyekuwa naye na Mbunge nilikuwa naye tukifanya kazi tukisalimiana, kila hali ilikuwa tukenda. (*Makofi*)

Lakini ninashangaa kwamba kupata mimi leo moja au kupata wenzangu mara moja imekuwa nongwa, imekuwa balaa, yamekuwa mashaka. Hali hii ambayo Mhe. Spika, mimi ninataka niseme tu na tunakwenda kwenye mwezi wa Ramadhani keshokutwa, lakini turudi tena kwenye *tawhid* ya Mwenyezi Mungu. Wenzetu sifikirii dini gani wanayoitumia ya kuweza kuhakikisha kwamba mambo haya wanafanya. (*Makofi*)

Mimi ninavyofahamu huu ni mchezo wa dunia. Siasa ni mchezo wa dunia, bado dini zitabakia, bado watu watabakia, bado udugu utabakia, bado Uzanzibari wetu na Utanzania utabakia lakini bado amani na utulivu unahitajika. (*Makofi*)

Mhe. Spika, mimi ninataka nisema kwamba tusichezee amani iliyopo. Mhe. Spika, tumeshaona nchi ambazo zilikuwa zikifaidika na matunda yao kama Libya, Syria na nchi nyengine ambazo ukiachia hizi za Uswahilini, hizo za Waraabu waliokuwa wakitumia tende, halua na mambo mengine na pesa za kulipwa. Nchi hizi sasa hivi hazielewani, hajulikani mtoto, wala baba, wala kitu gani. Zanzibar na Tanzania kwa ujumla Mhe. Spika, mimi hapa nilipo nishampanga mpaka mjukuu wangu, nishapanga kila aina ya mambo yangu na

kila mmoja hapa anapanga nyumba yake, mtoto wake, mjukuu wake. Nikitaka kustaafu nitakwenda kuhamia wapi kwa usalama uliopo Mhe. Spika. Kwa kweli Zanzibar inasifikana na Tanzania kwa ujumla kwa amani iliopo. (*Makofi*)

Lakini Mhe. Spika, hivi vitendo mimi ningeshauri sana kuwa serikali ikakaa chini kutakari kwa kina na hasa hasa Pemba. Mhe. Spika, *CUF* wanawaonea wananchi wa Pemba kwa kweli. Kwa sababu hatupo hivyo Mhe. Spika, zamani mtu anakufa Konde, walioko Mkoani wanakwenda kuzika. Mimi niseme hasa hiyo serikali ilikuwa ikivumilia. Maofisini mote hamna watu wanakwenda kuzika. Lakini leo nyumba na nyumba hawasemi, leo mtu kumsaidia mwenzake hawezi, basi hata kufa.Kuna Mweshimiwa mmoja jana alisema hata kura haji kutia tena. Bado mtu unamwambia maiti siendi kumzika, amekukosa nini? Tumetoka wapi Mhe. Spika, tunakwenda wapi.

Sasa mimi ningeshauri sana Mhe. Spika, ndugu zangu waliopo Pemba hasa wenye utaratibu wa *CUF* wakautizama kwa kina kosa limetokea kwa nani? Isiwe ng'ombe wa mbele hataki kwenda ukampiga wa nyuma. Waliokuwa hawakutaka kuingia kwenye uchaguzi aliyewazuia wanamjua na wao wenyewe wananielewa hili. Sasa wao wenyewe kama wanamjua mtu aliyewazuia wasiingie kwenye uchaguzi na bado Wawakilishi walikuwa na hamu ya kuingia humu, kwa nini wasingepinda, wakaingia kwenye uchaguzi wao, halafu wakaingia. (*Makofi*)

Sasa Mhe. Spika, mimi ninataka niseme ukweli kwamba tena naomba kuwa kusema kwa kiongozi na watu wenye, kwa sababu sasa hivi hakuna wajinga tena. Watu wote wamesoma na wana akili timamu, lakini waangalie kwa kina yale madhila unayofanya au vile vitendo unavyofanya, unamfanyia nani. Unamfanyia ndugu yako, unamfanyia mama yako, unamfanyia baba yako, unamfanyia kila mmoja. Na sote Pemba na takriban Zanzibar ni ndugu sote, unamfanyia nani.

Mhe. Spika, ningeshauri kweli kweli ikiwa hatua za kisheria za juu zaidi za kuweza kumwita kiongozi wetu aliyekuwa Makamu wa Kwanza wa Rais, hili suala akaweza kuvumilia akaliacha kama lilivyo na akasubiri mwaka 2020, tukaingia kwenye ulingo mwengine, watu wakaendelea na shughuli zao. Maendeleo yakaja, siyo serikali inafanya maendeleo halafu wao wanavunja wanabomoa.

Mhe. Spika, hili jambo ningeshauri sana na Masheikh wetu wangerudi nyuma kwa Mwenyezi Mungu wakamuangalia, wakatazama tunakokwenda na kuona hatma ya maisha yetu, hapa tulipo tu matatizo tuliyonayo ni tele. Watu wana

maradhi tele ya kansa, wana matatizo ya sukari, moyo, *pressure*. Watu wengine ndiyo kama unavyowaona wameshakaa katika roho roho. Ikifika siku unasikia leo kutakuwa na maandamano haya, kutakuwa na kitu hichi.

Mhe. Spika, uchaguzi kama ilivyokwisha kusema serikali umeshakwisha. Wenzetu kila mmoja aliye-*support* ni kawaida ya binadamu panapofanyika uchaguzi, matokeo madogo madogo yanajitokeza. Lakini baadae munasamehena na inakuwa ni la msingi kweli kweli. Mimi Mhe. Spika, ningewaomba ndugu zangu wa Pemba, majirani zangu, watu wangu, ndugu zangu sana, hiyo kauli za kivita au za kusema kugoma goma tungeziacha tukarudi kwa Mwenyezi Mungu tukasaidiana.

Mimi ninachokuhakikishia Mhe. Spika, Mwenyezi Mungu hajafanya makosa, aliyenileta mimi hapa na kama kuna mwengine anaweza kunigeuza basi ageuze, lakini mimi ninavyojua nimeletwa na Mwenyezi Mungu. Mwenyezi Mungu ndiye aliyefanya yote hapa na aliowafanyia wote hawa Mwenyezi Mungu ndiye aliyetaka na hufanya kitu anachokitaka yeye. Ikiwa Mwenyezi Mungu hajamjaalia Maalim Seif kuwa Rais hapa, hatokuwa maisha. Lakini akimjaalia kuwa anataka atamuweka siku yoyote. Na Wawakilishi kila mmoja kaingia kwa rehma ya Mwenyezi Mungu na mambo yake yalivyofikia.(*Makofi*)

Mimi Mhe. Spika, ningewashauri sana Wawakilishi waliokosa na vyeo vyengine waliokosa wastahamili. Wengine wamepata wa *CUF* wapo Bungeni, mbona sisi hatuwabughudhi. Wamekaa kule Bungeni wana starehe zao na sisi tupo huku Baraza la Wawakilishi tuna starehe zetu. Tuwaachiwe tuwashughulikie wananchi wetu. Wananchi Mhe. Spika, kwanza mimi ninataka nikuhakikishie Pemba ni asilimia kama ni hamsini, basi ninaweza kukwambia sitini jambo hili hawalitaki. Mhe. Spika, limekuwa tatizo tu la kulazimishwa. (*Makofi*)

Mhe. Spika, mimi niseme sana kama mtu kweli kweli ndiyo anasema kitu hakitaki, kwani lazima afundishwe kugoma, si mwenyewe tu atakuwa hataki. Lakini Mhe. Spika, ukenda kwenye kura watu wanakaa barabarani wanawazuia watu, wanakutishia wanakwambia ukenda utazikwa maiti peke yake. Sasa mtu ana hiyari, kura yake ni hiyari yake. Ilikuwa kuna haja gani Mhe. Spika, ya kumlazimisha mtu na kumuwekea vikwazo.

Mhe. Spika, ninachoona tu hawa watu wanalazimisha kitu ambacho sijui hata wafahamu ni kitu gani, kwa sababu wao wameshasema mengi. Wameshasema wanamuachia Mmarekani, wamuachie Mmarekani basi, atafanya hayo atakayo

Mmarekani. Lakini wasifanye wao. Maana kauli zinageuka siku hadi siku. Leo utasikia subiri tutakwenda sijui *ICC*, sijui wapi. Sawa. (*Makofi*)

Kwa hivyo, mwengine anasema sijui kutakuwa na kitu gani. Sasa mimi ningeshauri kama kuna hoja, kama kuna mambo mazuri ambayo wanayo kisheria. Hata Mhe. Rais, wetu hapa kishawaambiwa waende Mahakamani, waende huko kwenye *ICC*, waende kila pahala. Lakini suala la kugomeana, la kugombana na kutukanana na kukashifiana Mhe. Spika, suala hili ningeliomba sana kwa ndugu zangu, wazee ndugu na Masheikh tungeliacha tukamtazama Mwenyezi Mungu atatupeleka wapi ili tuendelee na nchi yetu. Mhe. Spika, mimi ningeomba serikali itazame kwa kina umuhimu wa suala hili, hasa amani na utulivu itawale katika nchi hii.

Mhe. Spika, ninakushukuru. (*Makofi*)

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Suleiman Sarahan Said. Sasa naomba nimwite Mhe. Ussi Yahya Haji, atafuatiwa, nitafanya mabadiliko kidogo atakuja Mhe. Shadya, baada ya Mhe. Ussi.

Mhe. Ussi Yahya Haji: Mhe. Spika, awali ya yote na mimi nishukuru kwa kupata nafasi hii ndogo kuchangia machache kuhusiana na hoja ya Ndugu yangu Mohamed Said Mohamed.

Mhe. Spika, kwanza awali ya yote lazima tutafakari huu ulimwengu kwamba sisi tupo visiwani Zanzibar (Unguja na Pemba). Mwenyezi Mungu si mjinga kutupa visiwa hivi. Kuna *Europe*, kuna India, kuna Marekani, kuna Wachina na wengineo. Sisi tupo Afrika na tuna kisiwa chetu cha Unguja na Pemba. Hatujafanya maajabu Unguja na Pemba kuwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. (*Makofi*)

Na hii Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar haikuja hivi hivi. Ilitafutwa na kwa nini imetafutwa. Tulidhalilishwa Waswahili wa Unguja na Pemba kwa miaka zaidi ya mia tatu. Tulifanywa watumwa, tulinyimwa elimu, uchumi, ardhi na kila kitu hapa kwa miaka mia tatu. Wazee wetu hawakusoma chochote. Walikaa na unyonge wao. Wakaamua tarehe 12 Januari, 1964 tukapata Serikali yetu. (*Makofi*)

Sasa Serikali hii imeundwa kwa misingi ya vyama. Vyama hivi vilivyotafuta serikali hakikuwa cha *Afro-Shirazi* tu kwanza. Kulikuwa na *ZNP, ZPP* na *ASP*. Ni vyama vitatu hivi. Sisi tukapata serikali kwa kupindua. Kwa hiyari

hatukupewa. Sultan hakutupa serikali kwa hiyari. Tulifanya Mapinduzi ya Zanzibar.

Baada ya kufaya Mapinduzi, tukaunda Serikali ya Jamhuri ya Watu wa Zanzibar. Baadae tukaunda Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Tukawa na Serikali kwa Chama cha *Afro-Shirazi* kwa muda wa miaka kadhaa. Mwaka 1992 tukaamua wenyewe tulete mfumo wa vyama vingi Zanzibar. Tukaruhusu mfumo wa vyama vingi. Lakini hivyo vyama vingi vya Zanzibar vilivyoundwa vilikuwa vina sheria. Sheria hiyo inasema kwamba chama chochote kitakachoundwa kisiwe na *elements* ya vyama vilivyopita, iliundwa hivyo.(*Makofi*)

Lakini Chama cha *CUF* ni punda yule yule, soji lile lile wa *ZNP*. Sasa hii *CUF* baada ya kuunda chama chao na kukosa kuunda Serikali Zanzibar imekuwa kama mtumwa ya wale waliotutawala, wanaambiwa hapo fanyeni hivi, fanyeni hivi. Kwa sababu wanayofanya leo, wanayohubiri leo. Katibu Mkuu anayohubiri leo yamehubiriwa zamani na ndiyo maana tukafanya Mapinduzi. Kwa mfano tumenyang'anywa ardhi, tulikuwa watu hatuzikani, hawawaziki *Waafro*-Shirazi. *Waafro*- Shirazi wakafukuzwa kwenye mashamba, kwenye ardhi, makazini na kila pahala. (*Makofi*)

Sasa yeye leo Katibu Mkuu anasema watu wagome. Wagome nini. Hivi Mpemba amgomee Muunguja na Muunguja amgomee Mpemba, vereje. Nani Mpemba, nani Muunguja. Wapemba na Wanguja ni baba mmoja, mama mmoja. Wala asitwambie kwamba tugomeana. Tumgomee nani. Mimi nikamgomee Mpemba. Mimi ni Mpemba kwa kiwango kikubwa sana. Na kama yeye anajisema Mpemba anawaambiwa Wapemba, mimi Mpemba kuliko yeye.(*Makofi*)

Mhe. Spika, tunaiomba Serikali mfumo wa vyama vingi vina sheria yake. Mwananchi hapa ana sheria ya kuishi, ana sheria ya atii Serikali iliopo madarakani na Serikali iliopo madarakani ni Serikali ya Chama cha Mapinduzi. Kwa Zanzibar inaongozwa na Rais Dkt. Ali Mohamed Shein na kwa Tanzania na Mhe. John Pombe Magufuli. (*Makofi*)

Serikali zote mbili zinataka kutiiwa sheria, hujatii sheria huwezi ukaishi katika Serikali hiyo. Kwa hivyo, ikiwa anatembea Mikoani kuwaambia watu wagome, musilipe kodi na musizikane, Serikali ipo. Tunaiomba sana Serikali yeyote yule, si yeye Katibu Mkuu tu, yeyote atakayevunja sheria katika visiwa hivi achukuliwe hatua za kisheria. Hilo la kwanza (*Makofi*)

La pili, ninawaomba wazee na vijana wenyewe wanaoambiwa iingieni barabarani tusiige Ulaya. Wao wanatazama kwenye *T.V* pale wanaona ooh! Marekani kuna mgomo, Syria kuna mgomo, Libya kuna mgomo. Wasifananishe Syria na Marekani na Zanzibar. Sisi ni maskini. Wazee ninakuombeni kwamba sisi ni maskini, hatuwezi leo kuingia barabarani, serikali ikahamaki hapa tukaambiwa *indoor,* tusitoke masaa mawili tutakula nini. Na maisha yetu sote Wazanzibari kwa Unguja na Pemba, maisha kama ndege au kuliko ndege. Maana yake ndege anatoka asubuhi anakwenda hajui atakula nini. Sisi hatujui chakula cha asubuhi tutakula nini, hatukijui, wachilia mbali cha kesho, cha asubuhi hatukijui. Leo tunakwenda kuingia barabarani, serikali ikasema hapana mtu kutoka, tunakwenda wapi. (*Makofi*)

Ninakuombeni ndugu zangu wa Kipemba, ninakuombeni ndugu zangu wa Matemwe, wa Kaskazini, wa Donge, wa Makunduchi na Tumbatu ambao munaambiwa mgome, mfanye ghasia, mfanye ghasia. Mbona juzi Mkwajuni hamkufanya ghasia yoyote. Mabomu matatu tu yamefyatuliwa na hamukupigwa. Wale waliosema kumelia mabomu Mkwajuni wamepigwa, hakupigwa mtu Mkwajuni. Lakini yamefyatulia kuambiwa musifanye ghasia, hivyo sivyo.

Na ile ilikuwa ni *warning*. Kwa hivyo, tunaiomba Serikali. Serikali ina madaraka kamili. Vyama vyetu hivi vimeletwa kwa mujibu wa sheria. Tufuate sheria. Ikiwa chama hakifuati sheria. Hakuna sababu kuwa tusikifute ati. Kama tutakifuta chama kimoja kinachofanya ghasia. Tuna vyama ishirini na mbili hapa Tanzania na sisi hatukuunda Serikali, *CUF* haikuingia kwenye Serikali. Si lazima ati *CUF* iingie kwenye Serikali. Tuna vyama vile pale viwili viko katika Serikali na tuna uhuru huo. Tuna uhuru wa kuleta *TADEA,* tuna uhuru wa kuleta chengine. Lakini sasa wao wenyewe wamesema hatutaki. Wakati wote wanaomba dua kwa vyetezo dunia nzima. Eeeh! Mwenyezi Mungu tupatie tupatie Rais mwenye kheri. Rais mwenye kheri ni Shein kishakuja. (*Makofi*)

Vyetezo Unguja nzima na Pemba, eeeh! Mwenyezi Mungu tupatie Rais mwenye kheri, Unguja yetu iwe salama na amani. Ndiyo hii. Hakuna mwengine, amani anayo Mhe. Shein. Na vile vyetezo vyenu Mwenyezi Mungu katakabalia.

Kwa hivyo, tunaomba amani na utulivu wetu usichezewe na mtu. Mhe. Makamu wa Pili wa Rais upo mwenye shughuli za serikali. Mfumo wa vyama vingi upo, taratibu zake zipo, sheria za polisi zipo, sheria za makosa ya jinai zipo na tatizo lenyewe Mhe. Spika, tatizo la hawa wanaranda huku na huku, baadhi ya mambo yetu hatuchukui hatua. Kuna *suspect* wa mabomu hapa

wametolewa, *DPP file* kalifungia chumbani, hakuna kesi inayokwenda, ingawa sistahili kuzungumza hivyo, kwa sababu liko mahakamani.

Lakini mtu akifanya makosa hatua zichukuliwe. Kama hazikuchukuliwa hatua ndio leo atakwenda hapa na atatomasa, leo anatomasa hapa na hapa na wala wanaotomaswa masikini ya Mungu hawaelewi dunia inavyokwenda, watakuja kuripuka pale tupate matatizo ya bure, amani yetu itoweke, hakuna Msikiti, hakuna baba, hakuna mama wala shangazi. Kwa hivyo, naiomba serikali idhibiti amani ya visiwa vya Unguja na Pemba ipasavyo.*(Makofi)*

Mhe. Spika: Naomba sasa nimwite Mhe. Shadya Mohammed, halafu atafuatiwa na Mhe. Miraji Khamis.

Mhe. Shadya Mohamed Suleiman: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipatia nafasi hii ya kuweza kujadili hoja iliopo mbele yetu. Mhe. Spika, kwanza naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyeniwezesha asubuhi hii kusimama hapa katika hali ya uzima na afya njema.

Baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu Mhe. Spika, namuomba Mwenyezi Mungu pia anijaalie nisiwe na jazba wala kitetemeshi na mwisho nikaja nikalia. Mhe. Spika, mimi niliyesimama hapa ni Mpemba, nasema haya na ninaizungumzia hali halisi iliyoko kisiwani Pemba.

Mhe. Makamu wa Pili, nakumbuka hivi karibuni ulifanya ziara ya kwenda Pemba tunakupongeza sana, na ulionana na wanachama wetu wa Chama cha Mapinduzi waliofikwa na mikasa mbali mbali. Kuna baadhi ya wanachama wetu wameachwa baada ya kwenda kupigia kura Chama cha Mapinduzi. Lakini tuseme kwamba muda umefika na mtoaji riziki ni mwenyewe Mwenyezi Mungu, na *Inshaallah* Mwenyezi Mungu atawala riziki nyengine.

Mhe. Spika, nimnukuu Mhe. Rais alivyosema kwamba *enough is enough*. Kusema kweli Mhe. Makamu wa Pili sasa umefika muda tumechoka, vitendo vilivyokuwepo Pemba sio vya kawaida, sio vya kibinadamu, sio vya Kiislamu, tunahisi kama hatuko katika nchi yetu, hususan wanachama wetu walioko vijijini wanateseka sana, wanapata shida sana, wanakuwa na hofu.

Niseme tu Mhe. Spika, mimi nimesimama hapa nazungumzia suala la Pemba lakini nina hofu, niko hapa nazungumza nasema, sijui nyuma yangu kwangu watoto wangu wataishije, lakini Mwenyezi Mungu *kadir* nitasimama kutetea haki yetu. Hapa tuko katika nchi yetu; sisi sio wakimbizi ni wazaliwa wa nchi hii, kwa nini tusiwe na raha katika nchi yetu. Mtu mmoja huyu Mhe. Makamu

wa Pili wa Rais anatupeleka wapi, kwa nini tumeletewa vyama vingi hapa, iwe mtu kuchagua Chama cha Mapinduzi iwe ni kosa, kila mtu ana mapenzi yake na anakwenda anapopenda mwenyewe. Kwa hivyo, mimi nimeamua kuwa mpenzi wa Chama cha Mapinduzi kosa langu liko wapi, nibaguliwe, niteseke, ninyanyaswe, nipewe majina yaliyokuwa hayana maana, nikose raha, hali hii inatupeleka wapi Mhe. Makamu wa Pili.

Mhe. Spika, naiomba serikali watu hawa wanajulikana wachukuliwe hatua, ili wananchi waishi kwa raha katika nchi yao. Hivi leo mtu kusema wewe ni mwanachama wa Chama cha Mapinduzi una hofu, japo kuwa unajulikana, kama kwetu Pemba mnajulikana kwa hesabu fulani na fulani wote CCM wanajulikana, lakini wanakuwa na hofu, kwa nini. Nategemea kwamba ingekuwa kuna japo watu wawili au watatu waliochukuliwa wakatiwa adabu na wananchi wakaona basi kila mwananchi angeishi kwa raha, anajua kwamba nitakapofanyiwa chochote kile najua kwamba hukumu itachukuliwa.

Lakini leo wananchi wetu mashamba yanatiwa moto, wanapigwa na nyumba zinatiwa moto, huoni kinachoendelea. Utasikia tu watu wako kwenye mikono ya sheria lakini hatimayake unaona kimya. Hii inavunja sana moyo, tunaiomba sana serikali jamani, jambo hili walifanyie haraka iwezekanavyo. Tunaambiwa nyinyi wana-CCM stahamilini. Huu Uislamu uko kwetu sisi tu, au hii subira wanayo wana-CCM tu, inafika pahala na wao wanachoka. Tunaiomba serikali jambo hili sio la kuweka, lifanyiwe kazi kwa haraka ipasavyo.

Mhe. Spika, nasema hivi kwa sababu gani, nazungumzia Pemba nimesema, nakwenda katika kijiji kinaitwa Mjimbini. Mhe. Spika, pale kuna wanachama wetu wa Chama cha Mapinduzi, lakini kuna hawa, nitawataja kwa majina wawili wanapata bughdha kubwa sana. Kuna mwanachama anaitwa Bikombo na kuna mwanachama anaitwa Faida ambaye huyu aliachwa na mumewe baada ya kwenda kukipigia kura chama cha Mapinduzi. Hawa wanapata tabu sana katika kijiji hicho, mara maandamano watukanwe, wasusiwe. Huyu Bikombo ana mumewe, huyo mumewe alikuwa anachunga na mwenziwe wa *CUF*, hatima yake wakenda kumwambia ng'ombe sasa tugawane, uchukuwe upande wako na mimi nichukuwe upande wangu, utowe shilingi 300,000, mnyonge wa Mungu masikini ataipata wapi shilingi 300,000 kwa ghafla, akamwachia, lakini bado yuko anaishi na riziki zake Mwenyezi Mungu anampa.

Mhe. Spika, jamani hii ngoma tunaiona ndogo, lakini hii ngoma sio ndogo, ngoma kubwa hususan kwa upande wa Pemba, wananchi wetu wanateseka sana, tunaiomba serikali jamani hatusimami hapa kwa mzaha, tunawatetea wananchi wetu, wana-CCM wanateseka sana tena sana Pemba. Leo mwana-

CCM akiwa na harusi basi muambizane CCM, mchukuane wa Mkoani wa Stahabu na kwengine, leo mwenzetu yuko Mtangani ana harusi ya mwanawe, mwende pale mkashughulikie mwenzenu mpaka amalize jambo lake.

Mhe. Spika, ikiwa pamefiwa mujikusanye wana-CCM mwende mkamshughulikie mwenzenu. Hivi kweli Uislamu ndivyo unavyotuelekeza hivi. Kila siku CCM tunaambiwa ndio makafiri, hao wanaojifanya wana dini, ndivyo walivyofundishwa hivyo au kuna kitabu kilichowafundisha wao hivi. Leo mtu anafikia kufa, basi maiti msikiti unakwenda kufungwa, atoke kiongozi wa nchi na polisi uende kufunguliwa msikiti ili aingizwe maiti, hivi hii ni haki na huu ndio Uislamu unavyotuelekeza. Jamani serikali ipo, Serikali ya Chama cha Mapinduzi ipo, tunaiomba sana tena sana wakati umefika sasa kwa vitendo.

Hili jambo Mhe. Makamu wa Pili liko Pemba, lakini na hapa Unguja limeshaanza, tumeshaanza kusikia kwamba kuna wana-CCM waliokodi nyumba za *CUF* sasa hivi wameshatolewa, wanaambiwa nendeni kwa mliowapigia kura wawape nyumba mukae, hii ni haki. Tunaiomba jamani serikali, serikali yetu tunajua ni sikivu, tulivu na inawapenda sana wananchi wake. Lakini tunaliomba hili jambo lifanyiwe haraka iwezekanavyo, hatua madhubuti zichukuliwe kwa hawa wakorofi wote wasioitakia Zanzibar mema na wanaochafua amani ya nchi hii.

Uchaguzi umekwisha Mhe. Makamu wa Pili, tulikuwa tunakwenda vizuri, sasa hivi kumetokea kidudumtu hicho kinachoanza kuharibu amani na utulivu wa nchi yetu. Hivi mtu huyo analindwa na nini jamani, hata mpaka kila siku achokonowe huku na huku. Juzi amekwenda Pemba kumetoka mabango mabaya ya viongozi wetu jinsi wanavyodhalilishwa, Mhe. Makamu wa Pili hatuwezi hata kuyasema, mabango yamewekwa juu, kwa nini hazichukuliwi sheria. Inatuuma sana Mhe. Makamu wa Pili sana.

Sisi wengine bila ya Chama cha Mapinduzi hatuna pakwenda hapa, bila ya Chama cha Mapinduzi, tunasema fawahisha hatuna pakwenda, tunajulikana fika. Mimi nimeshafika kuambiwa baba yangu mwanao tutakuletea nyama yake kwenye pakacha, nikamwambia twende. Lakini sitotoka kwenye Chama cha Mapinduzi wala sitobabaika, nimelelewa kwenye Chama cha Mapinduzi na nikasoma nilipofikia kwa Chama cha Mapinduzi, na ninaishi hapa kwa Chama cha Mapinduzi sibabaiki, litakalokuwa na liwe.

Mhe. Spika, sisi ni Waislamu tunasali sala tano, na tunaposali tunamuomba Mwenyezi Mungu kheri, Ewe Mwenyezi Mungu tujaalie kheri ya nchi hii na utuletee kiongozi mwenye kheri na nchi hii. Huyo hapo amekuja Dkt. Shein

ndiye mwenye kheri yetu na Mwenyezi Mungu anampa mtu kutokana na imani yake na Mwenyezi Mungu ameona huyu ndiye kiongozi wetu mwema, imani yake thabiti kwa wananchi wake na ametuletea na *Inshaallah* Mwenyezi Mungu atatujaalia tutakwenda naye huyu kwa muda wa miaka mitano, akimaliza yeye atakuja kiongozi mwengine, lakini hapa tunasema CCM mbele kwa mbele.*(Makofi)*

Mhe. Spika, nichukuwe nafasi hii tu kuwaambia ndugu zangu wa Pemba, jamani chonde chonde amani haipatikani bure bure, kuikosa amani ni siku moja, unaweza ukafanya fujo ikatoweka, lakini kuirudisha amani inaweza ikachukua si chini ya miaka mia moja. Tusichezee amani, tusidanganywe na watu wanaopata kula yao, wanaopata raha zao, mtu akiumwa sasa hivi keshapelekwa hospitali huko, wewe maskini ya Mungu upo, mijitu mizima na akili yenu mnapelekeshwa na mtu mmoja. Hapa uchaguzi tunasema umekwisha, tusubiri mwaka 2020 Mwenyezi Mungu atakaemjaalia uzima. *(Makofi)*

Baada ya hayo machache Mhe. Spika, nakushukuru sana, naiomba serikali itufahamishe lipi linalochukuliwa dhidi ya hii, ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Shadya Mohamed kwa mchango wako. Waheshimiwa Wajumbe, wanaoomba kuchangia ni wengi sana, lakini kanuni inatubana kuhusiana na muda. Kwa hivyo, wale niliowataja ndio watakaochangia, nilimuongezea Mhe. Shadya Mohamed, kwa sababu uwiano wa kijinsia haukuwepo, kwa hivyo, nikaruhusu na yeye achangie, lakini baada ya hapo nikarudi katika ule utaratibu. Kwa hivyo, sasa hivi nitamwita Mhe. Miraji, achangie, halafu baada yake yeye atafuatia Mhe. Said Soud Said. Mhe. Miraji Khamis Mussa, tafadhali. *(Makofi)*

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Mhe. Spika, kwanza nishukuru na mimi kunipa nafasi ya kuchangia hoja iliyowasilishwa mbele yetu. Mhe. Spika, kwa kuwa maelezo mengi waliyoyasema wenzangu ya upotoshwaji wa wananchi, uharibifu wa mali za umma, lakini na vitendo vinavyofanyika ambavyo vinahatarisha amani ya nchi yetu vinanifanya nisimame na mimi niungane na wenzangu kupinga matendo haya kwa asilimia zote.

Mhe. Spika, niseme tu kwamba ni kweli matendo sasa hivi yanayofanyika ndani ya nchi yetu baada ya uchaguzi kumalizika yanatunyima raha sisi na wananchi wenzetu wa Zanzibar. Serikali ipo, vitendo vinafanyika katika wilaya zetu ambazo serikali pia zipo, na kuna kamati za ulinzi na usalama katika wilaya, kuna kamati za ulinzi na usalama katika mikoa yetu, lakini zipo zile za

kitaifa. Zote hizi zinatakiwa zisimamie matendo haya machafu yanayofanyika au kauli chafu zinazotolewa na viongozi mbali mbali. Tumesikia yaliyotokea Pemba na tunaendelea kusikia siku hadi siku upotoshaji huu unaofanywa na viongozi wa Chama cha *CUF*.

Mhe. Spika, naomba ninukuu kauli ya Mhe. Jecha, baada ya kumtangaza Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Alisema; "Uchaguzi umekwisha na kazi kama ile ya kumtangaza Rais itafanyika mwaka 2020 Mwenyezi Mungu akitujaalia". Sasa tunaposikia kuna viongozi ambao wanaitangaza nafasi kama ile katika mtazamo mwengine ni sehemu kubwa sana ya kuwapotosha wananchi na uvunjifu wa amani wa nchi hii.

Mhe. Spika, siku moja wananchi wa Taifa hili baada ya kuamini kuwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Ali Mohemmed Shein, basi watakuja kuamini wana Rais mwengine, kitu ambacho tukiendelea kukivumilia sasa kitatuharibu, kitawaharibu wananchi wetu na iko siku serikali ikiendelea kuvumilia katika jambo kubwa kama hili, basi mizongano na migogoro huko ya kuoneshana nani wana Rais katika nchi hii, utakuja kuwa mkubwa kuliko yale matarajio ambayo tunayachukulia juu juu, naomba sana. Serikali sasa najua haikulala, lakini sasa kwa umahiri wa viongozi wetu tuliokuwa nao tuanze kuyashughulikia ipasavyo matendo yanayojitokeza. *(Makofi)*

Mhe. Spika, juzi tu katika Mkoa wa Kaskazini wenzangu wamesema, upotoshwaji huu ulianzia Pemba na juzi Kaskazini Mkoani kwetu kule wameanza. Wameanza kuzungumza kauli kama ambazo baadhi ya wajumbe wenzangu wamezungumza, lakini mpaka leo kuna ukimya mkubwa sana wa serikali tunayoiamini sisi kuwa ina dhamana ya wananchi wa nchi hii katika kushughulikia vitendo kama vile. Kwa hivyo, naiomba serikali kupitia Baraza lako hili tukufu, ianze kuvishughulikia vitendo vile mara moja. *(Makofi)*

Mhe. Spika, mengi wameyasema wenzangu, sitaki niyanukuu tena, kwa sababu sehemu kubwa ya hoja hii ni vitendo vya uvunjifu wa amani, kauli chafu, uharibifu wa mali za watu vinavyofanywa na ndugu zetu wale. Tuliona mengi baada ya uchaguzi. Tukirudi nyuma wakati wa Dkt. Salmin Amour tulianza na mambo ya tindikali wakatiwa ndugu zetu, tulipokuja kwa Dkt. Aman Karume baada ya uchaguzi vitendo kama hivi vikaendelea kuongezeka na yakafanyika mengi. Sasa uongozi huu wa Dkt. Ali Mohammed Shein kiongozi ambaye ana busara kubwa sana katika kuongoza watu, tujipange na tuishauri serikali wasije wakaharibu sifa za msingi za Mhe. Rais katika kuwatumikia watu, ni lazima tuwadhibiti mara moja. Tukiwadhibiti sasa hawatatupa shida baadae, na

wanapofanya ziara hizi wakenda kufanya mambo ambayo sio ya msingi katika nchi hii, tunayaona.

Mhe. Spika, mimi niipongeze serikali juzi kwa hatua ndogo tu ambayo walipotaka kufanya upumbavu wao kule Mkwajuni, wakapunguza zile hasira na vurugu ambazo zilitaka kuanza kule. Kwa hivyo, naendelea kuipongeza serikali lakini naiomba pia ichukuwe jitihada za makusudi sasa ya kudhibiti vitendo vyote vya uvunjifu wa amani vinavyoletwa na viongozi hawa wa *CUF*.

Mhe. Spika, mwisho, kwa sababu ya muda na niwape fursa wenzangu. Naomba kuunga mkono hoja hii iliyoletwa mbele yetu na kaka yangu Mhe. Mohammed Said Mohammed Mwakilishi wa Jimbo la Mpendae. Mhe. Spika, nakushukuru. *(Makofi)*

Mhe. Said Soud Said (Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum): Mhe. Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii kwa ajili ya kutaka kuchangia hoja hii ambayo imeletwa na sisi kama serikali hatuna budi kuhakikisha kwamba hoja hii inapokelewa na tunaifanyia kazi. *(Makofi)*

Mhe. Spika, Zanzibar ilifanikiwa kufanya Mapinduzi yake mwaka 1964, tarehe 12 Januari, yaliyoongozwa na Hayati Mzee Abeid Amani Karume pamoja na wenzake. Mapinduzi hayo yaliongozwa na Chama cha *ASP*, chama ambacho kwa muda mrefu kilikuwa kinahangaika kutafuta utawala lakini kilikuwa kinabanwa na mazingira yake kikaamua kufanya Mapinduzi kwa ajili ya kuwatafutia Wazanzibar haki yao, baada ya chama hicho kushika madaraka kilifuta chama cha *ZNP* na *ZPP* Zanzibar ikawa na chama kimoja tu cha *ASP*, ilivumilia hadi mwaka 1977 *ASP* ikakubali kuungan na Chama cha *TANU* na hatimae kaulimbiu ya vyama hivyo ikasema tutaendeleza mema ya *ASP* na mema ya *TANU* ndani ya Chama cha Mapinduzi.

Sasa tujiulize mema ya *ASP* ndio haya ya kuwabagua watu leo, maana CCM inafanya kazi ya Chama cha *TANU* na *ASP*, sasa mema ya *ASP* ndio haya ya kuwabagua watu ambao walikombolewa tarehe 12 Januari, 1884, tunachosema ni kwamba kiongozi huyu wa Chama cha Wananchi *CUF* ni mtu ambaye amechanganyikiwa, ni jambo la kusikitisha na la aibu kwamba yeye hadi hii leo analipwa na Serikali hii hii na karibuni hivi alipelekwa India akapoteza milioni mia tatu za Wazanzibari, kwa nini, kwenda kutibiwa yeye na *delegation* yake na aliporudi akabakia Serena akashughulikiwa pale na Serikali ya Jamhuri ya Muungano pamoja na Serikali ya Zanzibar. Inashangaza sana leo kwamba yeye anawaambia watu wasilipe kodi wakati yeye pesa zake zinatiwa kwenye *account* yake.

Inashangaza sana kwamba yeye anawaambiwa watu wasilipe kodi wakati mkataba wake yeye na familia yake atalipwa mpaka wafe, sasa mimi nawaambia wa Pemba wasicheze ngoma kwa zumari ya watu, zumari inapigwa ikawa wao wanadimka huku wanacheza, huyu mtu si mtu mzuri, mtu ambaye ana utaratibu wa kuwagawa watu lazima Serikali ya Zanzibar na Serikali ya Muungano ifikirie kwamba kwa nini anafanya vitendo kinyume na utaratibu. Baba wa Taifa anasema hivi; "Ukizoea kula nyama ya watu utaendelea kula nyama za watu". Sasa huyu bwana ameanzisha utaratibu wa kugawa watu familia kwa familia haielewani, utaratibu huu unaendelea kijiji kwa kijiji havielewani, utaratibu huu unaendelea Jimbo kwa Jimbo hayaelewani, utaratibu huu unaendelea Wilaya kwa Wilaya hazielewani, Utaratibu huu utaendelea Mkoa kwa Mkoa haielewani na ushahidi upo *CUF* walioko Kusini Pemba wanaitwa *CUF* jike, na *CUF* waliko Kaskazini Pemba wanaitwa *CUF* Dume.

Mhe. Spika, utaratibu huu utaendelea hatimae atawagawa Wazanzibari na Watanganyika kamaalivyopita kuwagawa waislam kwa waislam na hatimae waislam watagawika na wakristo na baadae Watanganyika na Wazanzibari, tujiulize Muungano utakuwepo, maana yake ni kwamba sera yake ya kuvunja Muungano anaihangaikia, tunatoa wito kwa msajili wa vyama vya siasa, Sheria Nam. 5 ya Vyama vya Siasa inaruhusu kusajili na kufuta na tumeshuhudia Mhe. John Tendwa alifuta vyama vya siasa ikiwemo chama cha *PONA* na vyenginevyo na *FORD*. Sasa leo inakuwaje *CUF* iachiliwe inahatarisha amani ya Tanzania, Tanzania ni nchi ya amani, vita vikitokea Zanzibar maana yake vimetokea Dar-es-Salaam mjini ndio maana yake.

Mhe. Spika, vita vikitokea Pemba maana yake vimetokea Mwanza, humo mote ni mwahala mwa Watanzania, sasa leo hii Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar iko katika hali ya kulishulikia hili kisheria, lakini kwa wakati huu tunamkabidhi msajili wa vyama aende Pemba akafanye utafiti wa kina, halafu atoe majibu ya haraka, kwa sababu huyu mtu sisi tumeshachoka nae, kwa mujibu wa taratibu wa vyama vya siasa unapokuwa na mambo matatu, moja katika hilo ukilifanya maana yake umetoka katika reli; kuwagawa watu kwa dini zao, kuwagawa watu kwa kanda, kuawagawa watu kwa makabila, maana yake tayari umeshafuta usajili wako, ushahidi upo wa kuwagawa watu huyu na msajili aende Pemba, tunamuomba msajili wa vyama vya siasa kwa sababu yeye ndiye nayesajili na yeye anayefuta, hii hoja ya kuambiwa hana uwezo wa kufuta si kweli na huyu msajili ni mtu wa imani sana. Kwa sababu ushauri alioutoa kabla ya uchaguzi wa marejeo alitoa barua kwa vyama vyote vya siasa kuviomba viingie katika uchaguzi, bwana huyu alikataa, yaani alipinga mpaka ile kauli ya msajili, sasa kwa nini aendelee kuwepo kwenye ulingo wa vyama vya siasa.

Sasa si vizuri Serikali inamshauri na inamuomba Msajili wa vyama vya siasa aende Pemba akapae ushahidi halafu atujuilishe sisi kama serikali ili na sisi tupate nafasi ya kuwaeleza Wazanzibari hali halisi, kimsingi huwezi kufanya biashara ya kusaga ugoro mshahara wako ukawa ni kukohowa, hatuwezi kabisa hicho kitu. Tunachokiomba sasa hivi msajili wa vyama vya siasa ndio muamuzi wa chama hichi afute mara moja, chama hichi kifutwe mara moja, baada ya kufanya haya na kuyaeleza haya nawaomba Wazanzibari waheshimu Serikali ilioko madarakani, kwani ndio Serikali pekee iliyo na mamlaka ya kisheria kwa sasa na si mtu mwengine yoyote, waachane na tabia ya mtu anayewashawishi; eti wasilipe kodi, eti wasiheshimu viongozi, eti wasiheshimu sheria, watakwenda kujikuta wanaingia jela pasi na utaraibu na huyu bwana ameshawatumbukiza Wazanzibari katika majanga mbali mbali.

Katika kipindi cha uchaguzi fulani uliopita vijana mia nane wa kipemba waligoma kwenda maskuli hatimae wakabakia Darajni pale wanauza mikanda na chupi kwenye mikono, hawakwenda tena skuli, hana lolote alilowasaidia, utaratibu wake aliwafanya baadhi ya wafanyakazi wa Serikali wakawa washabiki na hatimae Serikali ikawatenda wakabakia kunung'unika kwamba Serikali imewaachisha kazi. Sasa na hii ni ile ile Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inayoongozwa na Dkt. Ali Mohammed Shein wasije wakanung'unika kwa yale ambayo yatafanywa na Serikali hii. Mhe. Spika, ahsante sana. (*Makofi*)

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, kwanza nashukuru kwa kunipa nafasi pia nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia na kutuamsha salama na kutuwezesha kufanya shughuli zetu kama tulivyopanga. Aidha, nimshukuru mtoa hoja hii Mhe. Mohammed Said Mohammed Muwakilishi wa Mpendae kwa tafakuri yake kubwa na dhamira yake ya kuimarisha amani na utulivu katika nchi yetu. Na mimi nikubaliane nae kwamba rasilimali pekee ya Wazanzibari ni amani, utulivu na umoja wa nchi hii, siasa yoyote ile inayohatarisha amani, inayochochea chuki, inayochochea hasama na kuwatafautisha wananchi katika karne ya leo haikubaliki.

Mhe. Spika, kiongozi yeyote mwenye siasa ya namna hiyo amepitwa na wakati na haifai kabisa kumsikiliza, maana anatupotezea wakati wa kufanya mambo ya msingi ya maendeleo, hapa tulikuwa tujadili hotuba ya bajeti kwa misingi ya kuwaletea maendeleo wananchi wetu, kwa misingi ya kuondosha matatizo yaliyopo na changamoto zilizo mbele yetu ili wananchi wetu waishi kwa furaha zaidi na mazingira mazuri zaidi na kupambana na umasikini uliopo na kuondosha matatizo ya ajira na matatizo mengine ambayo vijana wetu

yanawakabili. Ni jambo la kustaajabisha sana unapoona vijana wadogo wa miaka 20 wanaingizwa katika siasa ambazo hazina tija kwao, tena wanaowaingiza wana umri wa zaidi ya miaka 70 miaka ambayo hatuwezi kusema ndio unakaribia na kuondoka duniani, lakini 'unaoiva ndio unaovunwa' kwa hivyo, kwa vyovyote vile mtu mwenye umri mkubwa yuko karibu zaidi kuondoka duniani kuliko mtu mwenye umri mdogo, kwa hivyo, unapokuwa na umri zaidi ya miaka 70 na kitu kwa mujibu wa wastani wa maisha ya binaadamu wa Zanzibar maana yake umri wake kati ya miaka 58 na 60.

Mhe. Spika, unapokuwa na zaidi ya miaka 70 tunasema unatumia ushei, kwa hivyo, kijana mwenye umri wa miaka ishirini ambaye tunamtarajia kuwa na muda zaidi ya miaka 50 ya kuishi anamsikiliza ambaye ameshapitwa na wakati kuhatarisha maisha yake, ni jambo la kusikitisha sana sana, kwa hivyo, mimi niwaombe sana vijana na wazee kwamba amani ya nchi yetu inaanzia ndani ya familia zetu. Kwa hivyo, tuchukue hatua zinazofaa katika kulea vyema familia zetu ili vijana wetu wasibabaike wakaingia katika fujo katika mambo ambayo yanahatarisha amani ya nchi. Nchi hii ni yetu sote tunahitaji kuilea, tunahitaji kuifanyia mema kwa ajili yetu na vizazi vinavyokuja, vizazi vyetu vitatuuliza sisi kama wazee mmefanya nini kutuwekea mustakbali mwema wa nchi yetu, tunapofanya mambo yanayohatarisha amani maana yake unaiondoa nchi katika mstari.

Mhe. Spika, nirudie kusema neno nililosema jana kwamba, anayechochea kuhatarisha amani sio wanaoathirika, maana huwa na mbinu zake za kujificha asiipate athari hiyo, wale wanaoshiriki ambao kuwa wengi ni vijana na wale masikini za Mungu kama wanawake na watoto ndio ambao wanaathirika zaidi. Kwa hivyo, lazima tufike mahala tuone jamani tuna nia ya kuadhibu mama zetu, jamani tuna nia ya kuadhibu watoto wetu, jamani tuna nia ya kuivunja nchi yetu? Kwa fikra za kawaida jambo hili haliingii maanani na hakuna nchi yoyote duniani inayopata matatizo ikaamua kufanya vurugu na fujo ikamaliza matatizo yao kwa salama, hao wote wanaogombana mwisho wake wanarudia katika meza ya mazungumzo, mfano hai hapo Libya nchi ilikuwa imetulia vizuri, inakwenda vizuri, mambo mazuri wameitia midomo na mikono mikono nchi wameivuja matokeo yake sasa hivi wanalia kuitafuta amani ambayo wameiharibu, wanakaa kuzungumza kuirudisha amani ili yarudi yale mafanikio waliyoyapata, wapi "maji yakishamwagika hayazoleki" Libya imekwisha.

Hivyo hivyo Syria na wengine na wengine, kwa hivyo, hatuwezi kuchukua mifano ambayo tunaona kabisa inahatarisha amani ya nchi, inavunja nchi ikawa ni kigezo cha kuwasikiliza watu wa aina hii, lazima tufike pahala tujue kwamba wapo watu hawaitakii mema nchi yetu, wapo watu ambao wana choyo

kuwaona wenzao wanafanya mema ya kuwatumikia wananchi, wana choyo kumuona Rais wetu Dkt. Ali Mohammed Shein anafanya wajibu wake wa kutumikia wananchi, wana choyo kuona Mawaziri wanafanya wajibu wao wa kuwatumikia wananchi, wana choyo kuwaona Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wanawatetea wananchi kupata haki zao.

Sasa watu wa namna hiyo sijui tuwaweke katika fungu gani, mimi nawaombeni sana sana wenzangu viongozi wa CCM tunayo kazi kubwa ya kuonyesha njia tusivunjike moyo kuonyesha njia kwa ajili ya mema ya nchi yetu, tujitahidi sana kuonyesha mazuri kwa kuwa ndio dhamira yetu na wale ambao wamekusudia shari ili waitie nchi hii katika matatizo tuendelee kuwaelimisha ili wafahamu njia sahihi na kuachana na tabia zao hizo.

Napenda nitoe wito na nilimsikia mwenzangu mmoja akisema hapa kwamba viongozi wetu wa dini hususan mashehe na maimamu katika misikiti wafanye kazi kubwa ya kutanabahisha waumini wetu waelewe umuhimu wa amani, upendo na umoja wa nchi yetu, tukifanya vyengine vyovyote vile ni kuhatarisha amani ya nchi na kuivuruga, niseme wakati wa malumbano umekwisha na kampeni zimemalizika, sasa shughuli ya kujenga nchi. Hawa wanafanya makusudi kutuondoa katika mstari kwa kuwaletea watu maendeleo, wanajua wakifanya hivi uchoro uchoro uchoro tutashughulika na haya.

Sisi tunasema sasa hatutaki tena kusikia maneno ya malumbano, hatutaki kusikia siasa hizi za maji taka, sasa ni wakati wa kufanya kazi za maendeleo kwa watu. Lazima tuondoke huko wasitutoe katika msingi tulioukusudia wa kutekeleza ilani yetu, tunae kiongozi wetu mkuu Jamadari wetu wa maendeleo Dkt. Ali Mohammed Shein, kiongozi muadilifu, mwenye busara na hekima, aliye tayari na anayejitolea kuitumikia nchi yake katika mazingira yote hayo, kilicho mbele yetu ni kuunga mkono jitihada zake tukawatumikia wananchi wetu. Na niseme Zanzibar zaidi ya asilimia 95 sisi ni waislam, tena waislam ambayo dhehebu letu kubwa ni sunni ni watu wa dini moja, ni watu wamoja, ndugu mmoja, utamaduni mmoja, tabia moja, jambo gani linalotufanya kila asubuhi tutafute namna ya kuhitilafiana.

Mhe. Spika, wenzetu wa dini nyengine waliopo hapa Zanzibar wamekaa kimya wanatustajabia inakuwaje waislam hawa, lazima tujifunze wenzetu wa dini nyengine hapa wamekaa kimya wanaimarisha amani na utulivu, wanaasa watu wao wema. Sisi wenyewe kwa wenyewe tunatofautiana, Dunia inatucheka. Kwa leo tumefikia hatua hii ambayo kwa njia moja au nyengine inarudisha nyuma maendeleo.

Mhe. Spika: Mheshimiwa. una dakika moja.

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Kwa hiyo, kwa kumalizia Mhe. Spika, niseme yafuatayo, Serikali yetu imeona wazi kwamba hatua hizi zinazofanywa hususan mikutano ya ndani inayofanywa na Chama cha *CUF* kwa wakati huu kwa njia moja au nyengine inaashiria kuhatarisha amani ya nchi, kwa hivyo, Serikali tayari ilishavitaka vyombo vyake vya ulizi na usalama hususan Jeshi la Polisi kuchukua hatua zinazofaa, narudia kwa kuwa Jeshi la Polisi lina mamlaka kamili inapoona mikusanyiko, mikutano ambayo inahatarisha amani ya nchi, wanayo haki kisheria kuisimamisha mikutano hiyo na mikusanyiko hiyo inayohatarisha amani ya nchi. Kwa hiyo, tunawataka Jeshi la Polisi kuchukua hatua hizo mara moja.

Pili, misafara mirefu ya Mhe. Makamu wa Kwanza wa Rais Mstaafu ambayo kwa njia moja au nyengine kwa taratibu za kisheria hairuhusiwi kutokana na hadhi yake ya kuwa Makamu wa Kwanza wa Rais. Utaratibu unaojulikana wa kisheria na vyombo vyetu vya ulinzi na usalama ndio vinavyopanga msafara wa Makamu wa Kwanza wa Rais Mstaafu, na mara nyingi huwa ni gari yake moja na walinzi wake. Kuwa na vyombo vingi vya maringi mawili hususan vespa wakati mwengine hazina hata namba zinaendeshwa kinyume na sheria za usalama barabarani, magari mengi, vurugu nyingi inayotoa usumbufu kwa wananchi, inayohatarisha usalama na amani ya watu, inayohatarisha watembeaji wa miguu na watu wengine wenye vyombo vyao vya usafiri jambo hili halikubaliki.

Kwa hivyo, pia nawataka Jeshi la Polisi kuchukua hatua zinazofaa kuona taratibu za kisheria zinalindwa na misafara ya namna ile hairuhusiwi, na hasa ukitilia maanani kwamba wakati wa kampeni umemalizika sasa ni wakati wa kufanya kazi.

Mwisho wale wafanyabiashara ambao tayari kwa taarifa za ki-*intelligence* tumepata habari kwamba wana nia na dhamira ya kufunga maduka ili kutoa usumbufu kwa wananchi na kuwaharibia wananchi kutokupata huduma muhimu za shughuli zao za maisha ya kila siku. Tunatoa onyo kali kwamba mfanyabiashara yeyote atakayefunga duka kwa dhamira ya kuwakosesha wananchi huduma muhimu basi leseni yake itafungiwa milele na hatopewa. Watu wa namna hiyo hawatopewa tena ruhusa ya kufanya biashara hapa Zanzibar. (*Makofi*)

Mhe. Spika, naomba kuwasilisha nakushukuru kwa kunipa nafasi. (*Makofi*)

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Mhe. Spika, kwanza nichukue fursa hii kukushukuru sana kwa imani yako ya kuikubali hoja yangu na kuona hoja yangu ina mantiki kubwa sana.

Mhe. Spika, niishukuru sana Serikali yangu ya Mapinduzi Zanzibar ikiwa chini ya mtendaji Mkuu wa Serikali katika Baraza la Wawakilishi Makamu wa Pili wa Rais nao kwa kuunga mkono hoja yangu. Lakini nichukue fursa hii sana, sana ndani ya sakafu ya moyo wangu kuwashukuru Wajumbe wote wa Baraza lako la Wawakilishi, kwa kuniunga mkono na kwa kujua dhamira yangu ya dhati ya kuleta amani katika nchi hii. (*Makofi*)

Mhe. Spika, kwanza niwataje wachangiaji walioichangia hoja yangu.

1. Mhe. Suleiman Sarahani Said
2. Mhe. Ussi Yahya Haji
3. Mhe. Shadya Mohammed Suleiman
4. Mhe. Miraji Khamis Mussa
5. Mhe. Said Soud Said (Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum)
6. Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais

Mhe. Spika, michango yote ilikuwa na maana kubwa na kuelekeza umakini wa kuleta amani katika nchi yetu. Vile vile nimshukuru sana Mhe. Waziri ametoa jambo la serikali kubwa na mimi naliunga mkono, na kwa sababu hiyo basi itoshe kusema Baraza lako tukufu tutoe maazimio lipinge vikali vitendo hivi vya kiharamia vinavyofanywa.

La pili serikali kuchukua hatua za haraka sana ingawa Mhe. Mohammed Aboud Mohammed tayari amesema na tuna ushahidi mkubwa kuwa leo Makamu wa Kwanza Mstaafu amehojiwa na polisi hivi saa nne ili kukomesha vitendo hivi. Vile vile baadae sheria iweze kuchukua mkondo wake kwa yale mambo yote ambayo yanaendelea kuashiria kuvunja amani hii.

Mhe. Spika, kwa hayo machache sana ambayo tunaazimia ninaomba kutoa hoja ili Baraza lako liweze kuazimia mambo hayo.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, hoja ya dharura ya Mhe. Mohammed Said Mohammed (Dimwa) imetolewa na naona imeungwa mkono, kwa hiyo mimi kazi yangu ni ndogo tu ya kuwahoji kwa wale wote ambao wanakubaliana na hoja ya Mhe. Mjumbe wanyanyue mikono, wanaokataa. Waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, mimi nitoe shukurani zangu za dhati tu kwa sababu imekuja kwa dharura na pamoja na kwamba ilikuja kwa muda mfupi lakini nimepata muda wa kujaribu kuitafakari na umuhimu wake na nikaona ni vyema basi ije ijadiliwe na kwa bahati mbaya tu walioomba kuchangia hii hoja ni wengi sana tofauti na nilivyodhani. Lakini muda tulionao kwa mujibu wa Kanuni ni saa moja tu, kwa hiyo imebidi tuitumie hiyo hiyo saa moja lakini mambo ya msingi yamezungumzwa.

Na namshukuru sana Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa namna alivyomalizia mchango wake, kwa sababu kwa kiasi kikubwa sana amejaribu kuonesha ile *commitment* ya serikali kwenye suala hili hasa la kuhakikisha kwamba amani ya nchi inaendelea kuwepo.

Waheshimiwa Wajumbe, baada ya hapo sasa naomba nimwite Katibu ili tujue shughuli zinazoendelea. Katibu tafadhali.

Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 – Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Spika, awali ya yote sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu.

Pili kukushukuru wewe kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Bajeti ya Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

Mhe. Spika, naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako tukufu, likae kama kamati kwa madhumuni ya kupokea, kujadili, kuzingatia na hatimae kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha ya Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa mwaka wa fedha 2016/2017.

Mhe. Spika, awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa kutujaalia kufika hapa tukiwa wazima na wenye afya njema pamoja na kunipa nguvu ya kuweza kuwasilisha hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa mwaka wa Fedha 2016/2017. Shukrani zangu za dhati nazitoa kwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dkt. Ali Mohammed Shein kwa kuniamini na kuniteua kuwa Waziri wake wa Nchi Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Nimefarijika sana na uteuzi wake huo kwangu, kwa imani yake hiyo kwangu, ninamuahidi kwamba nitafanya kazi

zangu kwa uwezo wangu wote na sitomuangusha na namuomba Mwenyezi Mungu anizidishie kutimiza wajibu wangu huo ipasavyo.

Mhe. Spika, kwa upande wa uchaguzi mkuu tumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kumaliza uchaguzi wa marudio uliofanyika tarehe 20 Machi, 2016 kwa salama na amani. Kama kawaida yetu uchaguzi huo ulikuwa ni kielelezo tosha cha kuimarika kwa demokrasia hapa kwetu Zanzibar kwani taarifa zinaonesha kuwa wananchi zaidi ya asilimia 67 walijitokeza kupiga kura.

Mhe. Spika, nachukua fursa hii adhimu kumpongeza kwa dhati Mhe. Dkt. Ali Mohammed Shein kwa kuchaguliwa kwa mara nyengine tena kuwa Rais wa Zanzibar kwa ushindi wa kishindo wa asilimia 91.4. Kuchaguliwa kwake kunatokana na imani kubwa walionayo wananchi wa Zanzibar katika kuwatumikia na kuwaletea maendeleo. Natoa wito kwa wananchi wote kuifanyia kazi kauli mbiu yake isemayo "tusifanye kazi kwa mazoea". Namuomba Mwenyezi Mungu amjaalie afya njema na maisha marefu ili aweze kutekeleza majukumu yake na kutimiza ahadi alizozitoa kwa wananchi wetu.

Mhe. Spika, kwa namna ya pekee naomba kutumia nafasi hii pia kumpongeza Mhe. Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mhe. Mama Samia Suluhu Hassan kwa kuteuliwa kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, akiweka historia katika nchi yetu ya kuwa mwanamke wa kwanza kushika wadhifa huo kufuatia Uchaguzi Mkuu uliofanyika mwezi wa Oktoba 2015. Ni matumaini yetu kwamba kuchaguliwa kwao kutazidisha uimara wa Muungano wetu ikiwa ni pamoja na kuzishughulikia changamoto zake. Nawaomba Watanzania wote tuwaunge mkono viongozi wetu hawa katika kutekeleza majukumu yao mazito kwa taifa letu. Aidha, naomba tuiunge mkono kauli ya Mhe. John Pombe Joseph Magufuli ya kusema "Hapa kazi tu". Namuomba Mwenyezi Mungu awazidishie hekima na busara katika kuwatumikia wananchi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mhe. Spika, nachukua fursa hii kumpongeza Mhe. Balozi Seif Ali Iddi, Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar kwa kuteuliwa kushika wadhifa huo kwa mara nyengine tena. Kuteuliwa kwake kunathibitisha namna alivyomudu kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi mkubwa. Ni matumaini yangu kuwa kutokana na uwezo wake ataweza kuyatimiza matumaini ya Wazanzibari juu ya serikali yao na atamsaidia na kumshauri kwa karibu Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi katika kupeleka mbele gurudumu la

maendeleo na kuifanya Zanzibar kuwa visiwa vyenye neema na haiba ya kusifika.

Mhe. Spika, pongezi zangu za dhati zije kwako wewe binafsi kwa kuchaguliwa kuwa Spika wa Baraza la Tisa la Wawakilishi. Naamini uwezo mkubwa ulionao na uzoefu wako kwa Baraza hili na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ndiko kulikopelekea Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili kukuchagua kushika wadhifa huo. Aidha, nampongeza Mhe. Mgeni Hassan Juma, Mwakilishi wa nafasi maalum za Wanawake kuwa Naibu Spika. Pia, nampongeza Mhe. Shehe Hamad Mattar Mwakilishi wa Jimbo la Mgogoni kwa kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Baraza hili tukufu. Aidha, nachukua nafasi hii kumpongeza Mhe. Mwanaasha Khamis Juma, Mwakilishi wa wananchi wa Jimbo la Chukwani na yeye pia kwa kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti. Kwa pamoja nakutakieni kila la kheri katika kutekeleza majukumu yenu.

Mhe. Spika, pongezi zangu zisizo na kifani ziende kwa Mhe. Omar Seif Abeid Mwakilishi wa Wananchi Jimbo la Konde kwa kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa. Pia nawapongeza Waheshimiwa Wajumbe wote wa kamati hii kwa kuteuliwa kufanyakazi ndani ya kamati hii. Naahidi kuwa ofisi yangu itatoa ushirikiano wa dhati kwao katika kufanikisha majukumu yao ya kikazi.

Mhe. Spika, kabla sijamaliza salamu zangu za pongezi, kwa heshima pia naomba uniruhusu kuwapongeza wananchi wa Zanzibar na Tanzania kwa ujumla kwa kuendelea kukichagua Chama cha Mapinduzi kuongoza serikali zetu zote mbili. Salamu zangu za pongezi na shukrani ziende kwa Tume zetu za Uchaguzi, Tume ya Taifa ya Uchaguzi na Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar kwa kuandaa mazingira mazuri ya uchaguzi huru na wa haki, pia kwa vyombo vya ulinzi na usalama kwa kuhakikisha kuwa amani na utulivu inakuwepo katika kipindi chote cha uchaguzi na baada ya uchaguzi hadi leo hii. Mhe. Spika, kwa heshima na unyenyekevu mkubwa sana ninawashukuru wananchi wa Jimbo langu la Chwaka kwa kunirudisha tena kuwa Mwakilishi wao katika Baraza hili tukufu kwa kipindi cha miaka mitano ijayo. Bila ya shaka yote wameonesha imani na upendo mkubwa kwangu na nawaahidi kushirikiana nao kikamilifu kwa hali na mali katika kuleta maendeleo ya jimbo letu.

Mhe. Spika, kama tunavyojuwa katika kipindi cha Masika mvua zimeleta athari katika baadhi ya maeneo ya Visiwa vyetu ikiwemo mafuriko ya maji na maradhi. Naomba kutoa mkono wangu wa pole kwa wananchi waliopata maafa ya kuingiliwa na maji katika nyumba zao. Aidha, nawapa pole ndugu zetu waliopatwa na ugonjwa wa kipindupindu na waliondokewa na wapendwa wao

kutokana na ugonjwa huo. Namuomba Mwenyezi Mungu awape moyo wa subira katika kipindi hiki kigumu. Natoa wito kwa wananchi kuchukua tahadhari ili waepukane na maafa kama hayo hasa kwa kuzingatia maelekezo yanayotolewa na wataalamu wa ujenzi pamoja na maelekezo ya wataalamu wa afya.

MUUNDO WA OFISI YA RAIS NA MWENYEKITI WA BARAZA LA MAPINDUZI

Mhe. Spika, Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi amefanya mabadiliko ya muundo wa Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuongeza Idara mpya ya Ufuatiliaji na Tathmini ya Sera na Maamuzi ya Serikali. Muundo wa sasa utakuwa una idara hiyo ya ziada na utakuwa kama ifuatavyo:-

i. Ofisi ya Faragha ya Rais;
ii. Ofisi ya Baraza la Mapinduzi;
iii. Idara ya Ufuatiliaji na Tathmini ya Sera na Maamuzi ya Serikali;
iv. Idara ya Mawasiliano na Habari – Ikulu;
v. Idara ya Mipango, Sera na Utafiti;
vi. Idara ya Uendeshaji na Utumishi;
vii. Ofisi ya Usalama wa Serikali;
viii. Idara ya Ushirikiano wa Kimataifa na Uratibu wa Wazanzibari wanaoishi nje ya nchi; na
ix. Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Pemba.

MAJUKUMU YA OFISI YA RAIS NA MWENYEKITI WA BARAZA LA MAPINDUZI

Mhe. Spika, kulingana na muundo uliopo, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi inatekeleza majukumu yafuatayo:-

i. Kusimamia shughuli za Mhe. Rais;
ii. Kuendeleza taswira nzuri ya serikali mbele ya jamii;
iii. Kusimamia mambo yanayohusu Baraza la Mapinduzi;
iv. Kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa Sera na Maamuzi ya Serikali;
v. Kuratibu na kusimamia utekelezaji wa Sera za Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi;
vi. Kusimamia utekelezaji wa shughuli za Ofisi ya Usalama wa Serikali (*GSO*);

vii. Kuratibu ushirikiano wa Kimataifa na Uratibu wa Wazanzibari Wanaoishi nje ya Nchi (*Diaspora*); na
viii. Kuratibu na kusimamia shughuli za Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Pemba.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo ya utangulizi sasa naomba uniruhusu niwasilishe kwa ufupi Utekelezaji wa Programu za Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kipindi cha Julai 2015 – Machi 2016.

MAFANIKIO YA PROGRAMU ZA OFISI YA RAIS NA MWENYEKITI WA BARAZA LA MAPINDUZI KWA KIPINDI CHA JULAI – MACHI 2015/2016

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2015/2016, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Fungu A01 lilitengewa jumla ya TZS. 5,965.0 milioni. Kati ya hizo TZS. 1,200.0 milioni kwa ajili ya mradi wa maendeleo na TZS. 4,765.0 milioni kwa ajili ya kazi za kawaida. Fungu A02 lilitengewa jumla ya TZS. 1,663.0 milioni na Fungu A03 lilitengewa jumla ya TZS 663.4 milioni. Hadi kufikia mwezi Machi, 2016 Fungu A01 liliingiziwa TZS. 2,844.9 milioni, Fungu A02 liliingiziwa TZS. 889.2 milioni na Fungu A03 liliingiziwa TZS. 135.6 milioni. Kwa ujumla upatikanaji wa fedha ulikuwa asilimia 47.9. Kiambatisho Namba 1 kinaelezea fedha zilizoidhinishwa 2015/2016.

Mhe. Spika, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa mwaka wa fedha 2015/2016 ilijipangia kutekeleza Programu Kuu nane na Programu Ndogo 10. Programu hizo zilitekelezwa chini ya Fungu A01, A02 na A03. Utekelezaji wa Programu hizo upo kama ifuatavyo:-

i. Programu ya Kusimamia shughuli za Mheshimiwa Rais na Kuimarisha Mawasiliano Ikulu

Mhe. Spika, matokeo ya utekelezaji wa programu hii ni kuona kuwa umma na washirika wote kwa ujumla wanakuwa na uelewa mzuri kuhusu shughuli zinazotekelezwa na serikali yao. Kwa mwaka wa fedha 2015/2016, programu hii iliidhinishiwa TZS. 2,575.2 milioni kwa matumizi ya kazi za kawaida zilizopangwa katika programu hii na TZS. 1,200.0 milioni kwa kazi za maendeleo na hadi kufikia mwezi Machi, 2016 iliingiziwa TZS. 1,633.8 milioni kwa kazi za kawaida.

Mhe. Spika, kupitia programu hii mafanikio makubwa yamepatikana yakiwemo kuongezeka kwa uelewa wa wananchi baada ya ofisi kutoa taarifa mbali mbali juu ya utekelezaji wa shughuli za maendeleo na kijamii kupitia Jarida la Ikulu

na vipindi mbali mbali vilivyoandaliwa na kurushwa hewani kupitia vyombo vya habari. Aidha, ziara zilizofanywa na Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi zimewawezesha wananchi kujua utekelezaji wa shughuli zinazofanywa na serikali yao wakati anapokutana na kuzungumza na wananchi hao. Vile vile, hotuba za Mhe. Rais ambazo amezitoa katika shughuli mbali mbali zenye lengo la kuelezea mwelekeo wa Sera na Maendeleo ya Serikali zimechapishwa na kusambazwa kwa wananchi.

Mhe. Spika, utekelezaji halisi wa programu hii kupitia idara zinazohusika ni kama ifuatavyo:-

Ofisi ya Faragha ya Rais

Mhe. Spika, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mhe. Dkt. Ali Mohammed Shein alifanya ziara ya kikazi nchini Ujerumani tarehe 02 hadi 09 Juni, 2015. Ziara hiyo ilikuwa na madhumuni ya kuitikia mwaliko wa Taasisi ya '*Africa Verein'* wa kushiriki katika uzinduzi wa Tamasha la kila mwaka la Muziki na Utamaduni wa Afrika. Kwa mwaka 2015, Zanzibar ilipewa nafasi ya kipekee ya kujitangaza na kupanua soko la utalii nchini Ujerumani na katika nchi nyengine za Ulaya. Tamasha hilo lilifanyika katika Mji wa Wurzburg na Zanzibar ilitambulishwa kuwa ni Visiwa vyenye vivutio vya ajabu na vingi vya kuvutia (*Magic Islands*).

Mhe. Spika, Mhe. Rais na ujumbe aliofuatana nao, walitembelea mji wa Wurzburg, Berlin na Potsdam. Katika miji hiyo, Mhe. Rais alitembelea sehemu za kihistoria, kuzungumza na baadhi ya Watanzania wanaoishi Ujerumani na kufanya mazungumzo na timu ya wafanyabiashara inayoongozwa na Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wafanyakazi wa Ujerumani wanaowekeza na kufanya biashara katika Bara la Afrika Dkt. Stefan Liebing pamoja na kufungua Mkutano wa Kimataifa wa kila mwaka kuhusu biashara na uwekezaji. Kadhalika, ujumbe huo ulikutana na Mabalozi wa Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki wanaoziwakilisha nchi zao nchini Ujerumani na kutembelea Makumbusho ya Viumbe hai ya Berlin pamoja na Skuli ya Bruno-H-Burgel huko Potsdam yenye uhusiano na Skuli ya Mwanakwerekwe H.

Mhe. Spika, Mhe. Rais alitumia fursa hiyo pia kuelezea hali ya amani, utulivu na usalama iliyopo katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na vivutio mbali mbali vya utalii vilivyopo hapa nchini. Kadhalika, aliwaalika wananchi wa Ujerumani na washiriki wengine wa Tamasha hilo la Muziki na Utamaduni kuitembelea Zanzibar na kujionea vivutio vya utalii ikiwemo

utamaduni, mila, desturi, maeneo ya kihistoria, fukwe safi na ukarimu wa wananchi wake. Aidha, Mhe. Rais alimshukuru Meya wa Jiji la Wurzburg Mstahiki Christian Schuchardt kwa heshima waliyoipata Zanzibar katika Tamasha hilo na kusifu jitihada za jiji hilo katika kuhifadhi majengo ya kale. Mhe. Rais aliahidi Zanzibar kuiga uzoefu wa jiji hilo katika kutekeleza azma ya kuuhifadhi Mji Mkongwe na majengo yake.

Vile vile, Mhe. Rais na ujumbe wake walipotembelea Idara ya Magonjwa ya Tropiki katika Chuo Kikuu cha Wurzburg, alishauri uwezekano wa taasisi hiyo kushirikiana na Taasisi za Utafiti za Zanzibar hasa Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (*SUZA*) jambo ambalo lilikubaliwa.

Mhe. Spika, katika mkutano wake na Watanzania wanaoishi Ujerumani, Mhe. Rais aliwahakikishia Wanadiaspora hao kuwepo kwa amani na usalama nchini pamoja na kujadiliana nao kuhusu harakati za kisiasa hasa suala la Muungano wa Tanzania, mafanikio ya Serikali ya Umoja wa Kitaifa ya Zanzibar, hatua za maendeleo ya kiuchumi na kijamii nchini na kuwataka kuwa mabalozi wazuri wa kuitangaza nchi yetu huko. Vile vile, aliwanasihi kutii sheria za nchi wanayoishi na kuwaasa kutosahau nyumbani kwao na kufanya maandalizi ya kurejea baada ya kukamilisha yale waliyoyafuata ughaibuni.

Mhe. Spika, Mhe. Rais katika mwaka wa fedha uliopita alionana na wageni mbali mbali akiwemo Mkuu wa Nchi, Mawaziri, Mabalozi, Wakuu wa Taasisi za Kimataifa pamoja na watu mashuhuri. Viongozi hao wamezungumzia kuhusu kuimarisha uhusiano na ushirikiano kati ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hasa Zanzibar katika nyanja za uchumi, biashara, utalii na uwekezaji. Orodha kamili ipo katika kiambatisho Namba 3.

Mhe. Spika, Mhe. Rais alihudhuria mkutano wa kilele wa Wakuu wa nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki tarehe 2 Machi, 2016 uliofanyika jijini Arusha - Tanzania. Viongozi wengine waliohudhuria ni Mhe. Dk. John Pombe Joseph Magufuli; Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Yoweri Kaguta Museveni; Rais wa Uganda, Mhe. Paul Kagame; Rais wa Rwanda na Mhe. Uhuru Kenyatta; Rais wa Kenya. Wengine ni Mhe. Joseph Butore; Makamu wa Rais wa Burundi na Mhe. James Wani Igga; Makamu wa Rais Sudani ya Kusini. Katika mkutano huo, nchi wanachama ziliwafikiana juu ya Dira ya Kiuchumi 2050 na masuala mengine ya maendeleo ya mtangamano.

Mhe. Spika, kadhalika, katika kipindi hiki Mhe. Rais alikagua shughuli za maendeleo ikiwa ni pamoja na Mradi wa Maji safi na salama Makunduchi, Mradi wa Ujenzi wa Mji Mpya Fumba na kutembelea eneo litakalojengwa

Bandari mpya ya Mpigaduri. Aidha, Mhe. Rais alikagua maendeleo ya Mradi wa Kuimarisha Usafi na Mazingira ya Miji, Zanzibar (*ZUSP*). Katika mradi huu, alikagua hatua za ujenzi wa misingi ya maji ya mvua katika Uwanja wa Mnazi Mmoja, ujenzi wa ukuta wa Ufukwe wa Forodhani na kulizindua jengo la Manispaa ya Zanzibar lililofanyiwa matengenezo makubwa.

Mhe. Spika, kwa upande wa Pemba, kupitia mradi wa "*ZUSP*," Mhe. Rais alikagua maendeleo ya ujenzi wa vigazi, machinjio ya wanyama na jengo la Halmashauri ya Mji wa Chake chake. Vile vile, alikagua jengo la Halmashauri ya Mji wa Mkoani na ujenzi wa vigazi katika mji wa Mkoani. Kwa upande wa mji wa Wete, Mhe. Rais alikagua maendeleo ya ujenzi wa soko na jengo la Halmashauri ya mji wa Wete.

Mhe. Spika, katika kipindi hiki, vile vile, Mhe. Rais alikagua maendeleo ya Kiwanda cha Sukari Mahonda, alikagua maendeleo ya mradi wa Pennyroyal na ujenzi wa barabara ya Matemwe Mbuyutende. Mhe. Rais alifanya uzinduzi wa umeme katika kijiji cha Kijini Matemwe. Aidha, Mhe. Rais alipata fursa ya kukutana na Wanadiaspora na kula nao Chakula cha Mchana Ikulu. Vile vile, alifanya ufunguzi wa Skuli mpya ya Makangale kisiwani Pemba na kuzindua taa za kuongozea ndege katika kiwanja cha ndege cha Pemba.

Mhe. Spika, kwa nyakati mbali mbali katika kipindi kilichopita, Mhe. Rais alishiriki katika hafla za utoaji wa vifaa vya michezo Unguja na Pemba ambapo vile vile alishiriki katika uzinduzi wa Tamasha la Michezo ya Shirikisho la Vyuo Vikuu na Taasisi za Elimu ya Juu Zanzibar (*ZAHILFE*). Katika maeneo aliyoyatembelea, Mhe. Rais alitoa maelekezo kwa taasisi zinazohusika juu ya kuharakisha utekelezaji wa miradi hiyo ili kufikia malengo yaliyowekwa. Maeneo mengine aliyoyatembelea ni Kambi ya Wananchi waliopata maafa ya mafuriko pamoja na kambi ya wagonjwa wa maradhi ya kipindupindu iliyopo Chumbuni.

Mhe. Spika, pamoja na shughuli hizo Mhe. Rais katika kipindi hiki aliapishwa kuwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi tarehe 24 Machi, 2016 kufuatia ushindi wa kishindo alioupata katika uchaguzi mkuu uliofanyika tarehe 20 Machi, 2016. Kadhalika, tarehe 02 Mei, 2016 Mhe. Rais aliapishwa na Jaji Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuwa mjumbe wa Baraza la Mawaziri la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ili aweze kutekeleza majukumu yake katika Baraza hilo. Hafla hiyo ilifanyika mjini Dodoma ambapo alihudhuria kikao cha kwanza cha Baraza hilo. Vile vile, tarehe 05 Aprili, 2016 alizindua Baraza la Tisa la Wawakilishi kwa mujibu wa uwezo aliopewa katika Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984.

Mhe. Spika, Ofisi ya Faragha katika mwaka wa fedha unaomalizika, ilisimamia kwa ufanisi utekelezaji wa maagizo ya Mhe. Rais. Aidha, Ofisi hiyo ilifanikisha utunzaji wa majengo ya Ikulu yaliopo Mnazi Mmoja, Migombani, Kibweni, Dodoma, Mtaa wa Liabon Dar es Salaam, Mkoani Pemba, Chake Chake Pemba na Mkokotoni kwa kuyafanyia matengenezo madogo madogo ili kulinda haiba yake na kuimarisha mazingira ya kufanya kazi. Kadhalika, ofisi ilisimamia vyema huduma za Mhe. Rais pamoja na wageni waliofika kumtembelea.

Idara ya Mawasiliano na Habari - Ikulu

Mhe. Spika, Idara ya Mawasiliano na Habari - Ikulu imeandaa na kurusha hewani vipindi 26 vya redio na televisheni. Aidha, idara kwa kushirikiana na Idara ya Habari Maelezo imetoa taarifa kwa wananchi kupitia maonesho ya sinema vijijini. Ujumbe unaotolewa kupitia vipindi hivyo na maonesho ya sinema huelezea mafanikio ya utekelezaji wa shughuli mbali mbali za maendeleo zinazotekelezwa na serikali yao.

Mhe. Spika, Idara ya Mawasiliano na Habari - Ikulu vile vile imekuwa na utaratibu wa kutoa habari, picha na kalenda za Ikulu ambazo huchapishwa kila mwaka. Katika kipindi cha Julai – Machi 2015/2016 Kalenda za Ikulu nakala 4,500 zimechapishwa na kusambazwa katika Taasisi zote za Serikali na baadhi ya taasisi binafsi. Aidha, makala mbali mbali zimeandikwa na kuchapishwa kwenye magazeti ya ndani na nje ya nchi na kupitia jarida la Ikulu ambalo huchapishwa kila baada ya miezi miwili. Katika kipindi hiki cha utekelezaji matoleo namba 020, 021, 022, 023 na 024 ya jarida yalichapishwa na kusambazwa katika maeneo hayo.

i. Programu ya Usalama wa Watumishi wa Umma

Mhe. Spika, matokeo yaliyotarajiwa katika utekelezaji wa Programu hii ni kuimarika kwa usalama wa serikali na watumishi wake. Kwa mwaka wa Fedha 2015/2016, Programu hii ilitengewa TZS. 37 milioni na hadi kufikia mwezi Machi, 2016 iliingiziwa TZS. 15.1milioni.

Mhe. Spika, mafanikio yaliyopatikana kupitia Programu hii ni kuimarika kwa usalama wa serikali kupitia upekuzi unaofanywa kwa waajiriwa, utunzaji wa siri za serikali kwa kuimarisha Masjala za Siri na Bayana. Aidha, Wafanyakazi wa Serikali wanafanyakazi katika mazingira salama kupitia ukaguzi wa majengo ya serikali unaofanyika mara kwa mara.

Mhe. Spika, utekelezaji halisi wa Programu hii kupitia Ofisi ya Usalama wa Serikali ni kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, Ofisi ya Usalama wa Serikali imepokea maombi 508 kutoka Taasisi na Wizara mbali mbali za Serikali. Maombi hayo yamefanyiwa kazi na ushauri umepelekwa katika taasisi na wizara husika. Aidha, ukaguzi umefanyika katika majengo mbali mbali yakiwemo Bodi ya Chakula, Madawa na Vipodozi, Idara ya Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali, Bodi ya Mfuko wa Barabara, Mamlaka ya Uvuvi wa Bahari Kuu, iliyokuwa Wizara ya Katiba na Sheria, Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Pemba na Ikulu ndogo ya Dodoma.

ii. Programu ya Utawala na Uendeshaji wa Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi

Mhe. Spika, matokeo ya utekelezaji wa Programu hii ni kuwepo kwa mazingira mazuri ya utendaji kazi ambayo yatafanikisha utoaji wa huduma bora na maamuzi yatayotokana na matokeo ya tafiti. Kwa mwaka wa fedha 2015/2016, Programu ya Utumishi na Uendeshaji wa Ofisi ya Rais Ikulu iliidhinishiwa jumla ya TZS. 2,151.9 milioni kwa matumizi ya kazi zilizopangwa katika Programu hii na hadi kufikia mwezi Machi, 2016 iliingiziwa TZS. 1,118.8 milioni.

Mhe. Spika, kupitia programu hii mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na watumishi kupatiwa stahiki zao kwa wakati, kuimarika kwa mazingira ya kufanyia kazi na vitendea kazi vya kisasa. Ofisi imefanya kazi zake kwa kuzingatia Sheria ya Utumishi wa Umma na imefanya matumizi yake kwa kuzingatia Sheria ya Manunuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma. Aidha, watumishi wamejengewa uwezo kupitia mafunzo ya muda mrefu na mfupi.

Mhe. Spika, utekelezaji halisi wa Programu hii kupitia idara zinazohusika ni kama ifuatavyo:-

Idara ya Uendeshaji na Utumishi

Mhe. Spika, katika kipindi cha Julai – Machi 2016, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kupitia Idara ya Uendeshaji na Utumishi imesimamia upatikanaji wa huduma na vifaa vya kuendeshea ofisi, sambamba na matengenezo ya vipando na vifaa vyengine vya kufanyia kazi.

Mhe. Spika, wafanyakazi 73 wamepatiwa mafunzo ya muda mrefu na mfupi katika ngazi ya shahada ya Uzamili, Shahada, Stashahada na Cheti kwa kada za Uhasibu, Utunzaji wa Kumbukumbu, Ununuzi na Ugavi na Usimamizi wa Rasilimali Watu. Aidha, mafunzo ya Uelewa wa Sheria na Kanuni za Utumishi wa Umma yametolewa kwa Wakuu wote wa Idara na maofisa waandamizi 40, lengo kuu la kuendesha mafunzo hayo ni kusimamia watumishi kwa mujibu wa sheria na miongozo ya Utumishi wa Umma kwa nia ya kuleta ufanisi wa kazi. Kiambatisho Namba 4 na 5 vinatoa ufafanuzi zaidi.

Mhe. Spika, vikao vitano vya Bodi ya Zabuni na vikao viwili vya Kamati ya Ukaguzi wa Ndani vimefanyika. Manunuzi yote yalijadiliwa na kupitishwa na Vikao vya Bodi. Vile vile, Vikao vya Kamati ya Uongozi na Kamati Tendaji vimefanyika kwa ajili ya kujadili maagizo kutoka Baraza la Mapinduzi na ajenda nyengine zinazolenga kuongeza ufanisi wa kazi. Mishahara na stahiki nyengine za watumishi zimelipwa kwa kuzingatia sheria, kanuni na miongozo ya utumishi wa umma. Michango ya watumishi imewasilishwa *ZSSF* kwa wakati na wafanyakazi 32 waliostahiki wamepatiwa posho la likizo.

Idara ya Mipango, Sera na Utafiti

Mhe. Spika, utekelezaji wa shughuli za Mipango na Sera za Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi umefanyika kwa ufanisi. Utekelezaji huo ulifuatiwa na mkutano wa tathmini ambao uliwahusisha Maofisa wa viungo wa Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Kupitia mkutano huo, tathmini ya utekelezaji kwa kipindi cha Julai - Disemba 2015 iliwasilishwa. Aidha, maofisa walijengewa uwezo kupitia uwasilishaji wa mada mbali mbali zikiwemo: Namna bora ya kuandaa Viashiria, Umuhimu wa kuwasilisha ripoti kwa wakati na namna ya kuandaa Miradi ya Maendeleo.

Mhe. Spika, idara iliandaa ripoti ya utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya 2010-2015, ripoti za utekelezaji za kila robo mwaka, nusu na miezi tisa na ripoti ya tathmini ya utekelezaji wa shughuli za Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kipindi cha 2010-2015. Katika ripoti hizo, mafanikio mbali mbali yameidhinishwa pamoja na changamoto zilizojitokeza.

Mhe. Spika, Idara ya Mipango, Sera na Utafiti ilikamilisha utafiti juu mahitaji ya takwimu ya Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Idara pia, iliimarisha Kitengo cha TEHAMA pamoja na Maofisa wa Kitengo walipatiwa mafunzo ya muda mfupi. Aidha, vifaa kwa ajili ya kuimarisha mfumo wa ulinzi wa kompyuta na upatikanaji wa huduma ya intaneti ndani ya Ofisi vimefungwa. Vile vile, idara inaendelea kufanya tathmini ya usalama wa

mtandao wa Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Ripoti ya tathmini hiyo inatarajiwa kutolewa baada ya kukamilika zoezi hilo.

Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi – Pemba

Mhe. Spika, Ofisi imeshughulikia ziara tano za Mhe. Rais alizofanya Kisiwani Pemba. Lengo la ziara hizo lilikuwa ni kutembelea Miradi ya maendeleo ambayo ni barabara za Wete, Gando na Ukunjwi, Uzinduzi wa Kiwanja cha Kufurahishia watoto cha *ZSSF* Tibirinzi, uwekaji wa Jiwe la Msingi katika Hospitali ya Abdalla Mzee na uzinduzi wa Mfuko wa maendeleo wa zao la Karafuu katika Kiwanda cha Makonyo.

Mhe. Spika, ofisi pia imesimamia upatikanaji wa huduma katika majengo ya Ikulu yaliyoko Pemba. Huduma za umeme, maji na simu katika majengo ya Ikulu zimepatikana kwa wakati. Aidha, huduma za uendeshaji wa ofisi ikiwemo umeme, maji, mafuta, mtandao, simu vifaa vya kuandikia zimepatikana kwa wakati sambamba na matengenezo ya magari.

Mhe. Spika, wafanyakazi wa ofisi wamelipwa mishahara yao na michango yao katika *ZSSF*. Stahiki za watumishi zimelipwa ikiwemo malipo ya likizo za wafanyakazi 11 na malipo baada ya saa za kazi nayo wamelipwa. Aidha, ofisi imeendelea kuwajengea uwezo watumishi wake sita walioko masomoni katika ngazi ya shahada ya uzamili, shahada na stashahada.

Mhe. Spika, Ofisa Mdhamini amefanya vikao vitano vya Maofisa Wadhamini vilivyojadili maandalizi ya Ziara za Mhe. Rais wa Zanzibar, hali halisi ya mabadiliko ya Tabia ya Nchi, Maradhi ya Kipindupindu, mabadiliko ya wizara na agizo la serikali la kuzitaka wizara zenye majengo ya kukodi kuhamia katika majengo ya serikali. Hatua za utekelezaji wa maagizo hayo zinaendelea kufanyika.

iii. Programu ya Usimamizi wa Majukumu ya Kikatiba na Kisheria ya Baraza la Mapinduzi na Kamati ya Makatibu Wakuu

Mhe. Spika, matokeo ya utekelezaji wa programu hii ni kuimarika kwa sheria, sera na miongozo yenye kusaidia uendeshaji wa serikali, ukuaji wa uchumi na kupunguza umasikini. Kwa mwaka wa fedha 2015/2016, programu hii iliidhinishiwa jumla ya TZS. 479.0 milioni kwa matumizi ya kazi zilizopangwa katika programu hii na hadi kufikia mwezi wa Machi, 2016, ziliingizwa TZS. 180.8 milioni.

Mhe. Spika, kupitia programu hii, mafanikio mbali mbali yamepatikana yakiwemo kusimamia utekelezaji na kuidhinisha sera, sheria na mipango ya serikali.

Mhe. Spika, utekelezaji halisi wa programu hii kupitia Ofisi ya Baraza la Mapinduzi ni kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, Ofisi ya Baraza la Mapinduzi imesimamia kikamilifu uundwaji wa serikali mpya kufuatia kukamilika kwa uchaguzi mkuu ikiwemo uapishaji wa Waheshimiwa Viongozi wa ngazi za juu pamoja na kuwapatia vitendea kazi na miongozo ili kuwawezesha kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi. Aidha, ofisi imeratibu mafunzo maalum ya muda wa siku mbili kwa wateuliwa wapya katika ngazi za Waheshimiwa Mawaziri, Waheshimiwa Naibu Mawaziri, Makatibu Wakuu, Naibu Makatibu Wakuu, Wakuu wa Idara Maalum za SMZ na Wakuu wa Taasisi nyengine za Serikali. Katika mafunzo hayo mada mbali mbali ziliwasilishwa.

Mhe. Spika, katika kuhakikisha sera, sheria na miongozo ya nchi inatekelezeka kikamilifu kwa lengo la kuharakisha ukuaji wa maendeleo na kudumisha amani na utulivu nchini, ofisi imeendelea na vikao 11 vya kawaida vya Baraza la Mapinduzi na vikao 25 vya Kamati ya Makatibu Wakuu. Vikao vyengine viwili vya dharura vya Baraza la Mapinduzi na kimoja cha Kamati ya Makatibu Wakuu navyo viliratibiwa. Katika vikao hivyo, jumla ya nyaraka 18 zikiwemo za sera, sheria pamoja na taarifa 44 zilijadiliwa na kuamuliwa. Aidha, vikao vitano maalum vya kazi vya Mhe. Rais vilifanyika.

Mhe. Spika, Sambamba na kufanyika kwa vikao vya kawaida vya Baraza na Kamati ya Makatibu Wakuu, ofisi pia imeratibu jumla ya semina nne na mafunzo kwa Makatibu Wakuu kuhusu Sera ya Bima na Kanuni za Bima ya Kiislamu, Uandishi wa Nyaraka za Baraza la Mapinduzi, Rasimu ya Sera ya Huduma ya Msaada wa Kisheria (*Legal Aid Policy)*, na Kujenga Uwezo kwa Taasisi za Serikali Kutumia Ushahidi kwa ajili ya Kutunga Sera na Kufanya Maamuzi. Wakufunzi mbali mbali kutoka ndani na nje ya nchi akiwemo Katibu wa Baraza la Mawaziri la Zambia Mhe. Benard J. Kamphasa walishiriki kuendesha semina na mafunzo hayo.

Mhe. Spika, kutokana na Zanzibar kuwa mwanachama wa Mtandao wa Mabaraza ya Mawaziri ya Serikali za Afrika *(Africa Government Cabinet Network - AGCN)*, kwa mwaka wa fedha 2015/2016 Zanzibar imeweza kushiriki katika vikao vinavyoratibiwa na mtandao huo kwa lengo la kukuza uwezo wa sekretarieti za Mabaraza ya Mawaziri. Jumla ya viongozi wawili na

watendaji wanne wa sekretarieti ya Baraza la Mapinduzi kwa nyakati tofauti wamewezeshwa kuhudhuria vikao katika nchi za Uganda na Malawi, ambapo manufaa makubwa yamepatikana ikiwemo kuimarika uwezo wa sekretarieti katika uandaaji na uchambuzi wa nyaraka za Baraza la Mpinduzi na Kamati zake.

iv. Programu ya Uongozi na Utawala katika Ofisi ya Baraza la Mapinduzi

Mhe. Spika, matokeo ya utekelezaji wa programu hii ni kuimarika kwa mazingira ya kazi, kuongezeka kwa uwajibikaji na kurahisisha utoaji wa huduma bora za kiofisi. Kwa mwaka wa fedha 2015/2016, programu hii iliidhinishiwa jumla ya TZS. 1,184.0 milioni kwa matumizi ya kazi zilizopangwa na hadi kufikia mwezi Machi, 2016 ziliingizwa jumla ya TZS. 764.1 milioni.

Mhe. Spika, pamoja na mambo mengine, mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na kuongezeka kwa vitendea kazi vya ofisi, kuongeza ujuzi na ubunifu wa watumishi na mashirikiano ya karibu na taasisi mbali mbali.

Mhe. Spika, utekelezaji halisi wa programu hii kupitia Ofisi ya Baraza la Mapinduzi ni kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, ofisi imefanikiwa kuongeza vitendea kazi vipya na vya kisasa ikiwemo mtambo mpya wa mawasiliano (*PA System*) katika ukumbi wa mikutano wa Baraza la Mapinduzi na kuyaunganisha majengo ya ofisi na huduma ya Mkonga wa Taifa wa Mawasiliano wa Serikali. Aidha, utendaji wa ofisi umeendelea kuimarika na kuwa wenye ufanisi zaidi kutokana na kuendeleza programu za kujenga uwezo wa watumishi kitaaluma kwa mafunzo ya muda mrefu na mfupi kulingana na mahitaji ya ofisi na mabadiliko ya wakati.

Mhe. Spika, katika kuimarisha uhusiano na mataifa mengine, viongozi pamoja na watendaji wengine wa ofisi wamewezeshwa kushiriki shughuli mbali mbali katika majukwaa ya Kimataifa katika nchi za China na Singapore kwa lengo la kuongeza ujuzi, kubadilishana uzoefu na kujitathimini kulinganisha na utekelezaji na mafanikio ya mataifa hayo. Maudhui makuu katika ushiriki huo yalihusu Uongozi, Usimamizi wa Rasilimali Watu, Uongozi wa Fedha, Mashirikiano kati ya Taasisi za Umma na Sekta Binafsi, Teknolojia ya Habari na Mawaasiliano, Sera za Kiuchumi na Maendeleo Endelevu.

Mhe. Spika, aidha, viongozi na watendaji wengine wamewezeshwa kufanya utafiti wa tathmini za shughuli mbali mbali za serikali ikiwa ni pamoja na kufuatilia utekelezaji wa maamuzi ya Baraza la Mapinduzi na Kamati zake. Pia, ofisi imeimarisha uhusiano mzuri na Ofisi ya Katibu Mkuu Kiongozi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuratibu ziara za kikazi zinazofanywa na Katibu Mkuu Kiongozi (SMT) na watendaji wengine wa ofisi yake.

Mhe. Spika, ofisi imelipa mshahara watumishi wake na kupekeleka michango ya *ZSSF* kwa wakati. Aidha, watumishi watano walienda likizo ya kawaida na kupatiwa stahiki zao na watatu walipatiwa mafunzo ya muda mrefu na mfupi katika ngazi ya Stashahada na Shahada ya Uzamili katika fani za Utunzaji Kumbukumbu na Uhasibu.

Programu ya Kuratibu, Ushirikiano wa Kikanda na Mashirika ya Kimataifa

Mhe. Spika, matokeo ya utekelezaji wa programu hii ni kuimarika kwa ushiriki wa Zanzibar katika mikutano ya kikanda na kimataifa na kuhakikisha kuwa Zanzibar inanufaika na uhusiano huo. Kwa mwaka wa fedha 2015/2016, programu hii iliidhinishiwa jumla ya TZS. 389.7 milioni kwa matumizi ya kazi za kawaida zilizopangwa katika programu hii na hadi kufikia mwezi Machi, 2016 jumla ya TZS. 23.5 milioni zilikuwa zimepatikana.

Mhe. Spika, kupitia programu hii mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na wataalamu wa sekta mbali mbali kuwezeshwa kushiriki katika mikutano ya Jumuiya za Kikanda ndani na nje ya nchi. Hali hii imewawezesha kupanua wigo wa uelewa katika shughuli za mtangamano pamoja na kutambua fursa mbali mbali ikiwemo za kibiashara, uwekezaji na miradi.

Mhe. Spika, utekelezaji halisi wa programu hii kupitia Idara ya Ushirikiano wa Kimataifa na Uratibu wa Wazanzibari wanaoishi nje ya Nchi ni kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kama nilivyoeleza awali Mkutano wa Kilele wa Wakuu wa Nchi Wanachama za Jumuiya ya Afrika Mashariki uliofanyika tarehe 2 Machi, 2016. Mkutano huo ulimteua Mhe. Dkt. John Pombe Joseph Magufuli Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuendelea kuwa Mwenyekiti wa Jumuiya hiyo kwa mwaka mmoja. Aidha, Mhe. Liberat Mfumukeko kutoka Burundi aliteuliwa kuwa Katibu Mkuu wa Jumuiya. Pia, mkutano uliridhia Sudan ya Kusini kuwa mwanachama mpya na hivyo kufanya nchi wanachama sasa kuwa sita.

Mhe. Spika, Idara ya Ushirikiano wa Kimataifa na Uratibu wa Wazanzibari Wanaoishi nje ya Nchi imeshiriki katika mikutano mbali mbali ya Jumuiya za Kikanda ndani na nje ya nchi ambapo Tanzania ni mwanachama, ikiwemo Jumuiya ya *EAC, SADC, IORA* na utatu wa Jumuiya za *EAC - COMESA - SADC*. Miongoni mwa utekelezaji mzuri wa maamuzi ya Jumuiya ni kwamba tayari Kamisheni ya Kiswahili imehamia rasmi Zanzibar tarehe 15 Machi, 2016. Makao Makuu ya Kamisheni hiyo yapo eneo la Mpirani katika eneo la Mpirani katika eneo la Gymkhana pale Eacrotanal.

Mhe. Spika, Zanzibar ilishiriki katika mkutano wa kufanya mapitio ya Sheria za Tanzania ili kuweza kwenda sambamba na utekelezaji wa Itifaki ya Soko la Pamoja iliyofanyika Mkoani Morogoro na Kibaha Mkoa wa Pwani. Aidha, mkutano wa mapitio ya vikwazo vya biashara visivyo vya kiushuru uliofanyika Burundi, Arusha na Dar es Salaam pamoja na mikutano ya tathmini ya utekelezaji wa Kamati ya Kikanda ya utekelezaji wa Soko la Pamoja uliofanyika jijini Arusha na Mwanza. Pia, wafanyabiashara wadogo wadogo wa Zanzibar wameshiriki katika maonesho ya Jua Kali/Nguvu Kazi ya Afrika Mashariki yaliyofanyika tarehe 3 Disemba, 2015 jijini Dar es Salaam ambapo walipata fursa ya kutangaza ubora wa bidhaa zao pamoja na kujiimarisha katika Soko la Jumuiya la Afrika Mashariki (*EAC)*.

Programu ya Uratibu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa Wazanzibari Wanaoishi Nje ya Nchi

Mhe. Spika, matokeo ya utekelezaji wa programu hii ni Zanzibar kufaidika na michango ya Wazanzibari wanaoishi nje ya nchi katika maendeleo ya kijamii na kiuchumi. Kwa mwaka wa fedha 2015/2016, programu hii iliidhinishiwa jumla ya TZS. 112.1 milioni kwa matumizi ya kazi zilizopangwa katika programu hii na hadi kufikia mwezi Machi, 2016 iliingiziwa TZS. 95.1 milioni.

Mhe. Spika, utekelezaji wa programu hii umeleta mafanikio makubwa na kuimarika uhusiano kati ya serikali na Wazanzibari wanaoishi nje ya nchi. Jumuiya za Wazanzibari hao zimeendelea kusaidia kuimarisha sekta za afya na elimu. Aidha, kumekuwa na ongezeko la wataalamu wa kujitolea kutoka katika jumuiya mbali mbali za *Diaspora* wanaokuja nchini kusaidia shughuli za maendeleo.

Mhe. Spika, utekelezaji halisi wa programu hii kupitia idara inayohusika ni kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kwa upande wa *Diaspora*, watendaji wangu wameshiriki kongamano la Watanzania wanaoishi Birmingharm nchini Uingereza, lililofanyika mwezi Septemba, 2015. Kadhalika, Jumuiya ya Watanzania waishio Washington DC, katika mwezi Julai, 2015 kwa kushirikiana na *African Women's Cancer Awareness Association (AWCAA*) ya Marekani, walifika Zanzibar na kutoa huduma mbali mbali za afya kwa wananchi katika Hospitali Kuu ya Mnazi Mmoja na Skuli ya Afya iliyopo Mombasa pamoja na kukabidhi dawa mbali mbali na miwani kwa Wizara ya Afya Zanzibar.

Mhe. Spika, Jumuiya ya Wazanzibari wanaoishi katika nchi za Scandinavia (*Zandias*) wameendelea kushirikiana na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika kuimarisha sekta ya elimu kwa kuleta walimu wa kujitolea Zanzibar na kwa sasa walimu hao wapo Skuli ya Sekondari ya Nungwi na Kituo cha Elimu Mbadala Rahaleo. Aidha, wametoa msaada wa vitabu vya Elimu ya Afya kwa Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (*SUZA*). Jumuiya ya Wazanzibari wanaoishi nchini Canada (*ZACADIA*) nayo imetoa msaada wa maboksi 40 ya vitabu vya elimu kwa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar na baiskeli za magurudumu matatu kwa Jumuiya ya watu wenye ulemavu Zanzibar.

Mhe. Spika, kama tunavyofahamu kuwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania itaandaa Kongamano la Watanzania wanaoishi nje ya nchi mwezi Agosti, 2016 hapa Zanzibar. Katika kufanikisha suala hilo vikao vya maandalizi vimeshaanza. Ninawaomba Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu washirikiane na Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi katika kufanikisha shughuli hiyo muhimu kwa maendeleo ya nchi yetu.

MWELEKEO WA BAJETI YA OFISI YA RAIS NA MWENYEKITI WA BARAZA LA MAPINDUZI KWA MWAKA WA FEDHA 2016/2017

Mhe. Spika, hotuba ya bajeti ya Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ya mwaka wa fedha 2016/2017 ni ya kwanza katika muhula wa pili wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar Awamu ya Saba ulioanzia Machi, 2016. Hotuba hii imezingatia mipango mikuu ya Kitaifa ikiwemo MKUZA, Ilani ya Uchaguzi ya CCM 2015 – 2020, Mipango Endelevu ya Milenia na Maelekezo ya Hotuba ya Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi wakati akizindua Baraza la Tisa la Wawakilishi.

Mhe. Spika, naomba kulihakikishia Baraza lako Tukufu kuwa Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi itatekeleza majukumu yake kwa kuzingatia maelekezo na miongozo madhubuti ambayo Serikali ya Mapinduzi

ya Zanzibar ya Awamu ya Saba imeiandaa. Lengo ni kuhakikisha kuwa Zanzibar inapiga hatua zaidi za kimaendeleo pamoja na kudumisha mafanikio yaliopatikana.

Mhe. Spika, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi imeundwa na mafungu mawili ambayo ni Fungu A01 na Fungu A02. Idara na ofisi zinazounda Fungu A01 ni Ofisi ya Faragha ya Rais, Idara ya Mawasiliano na Habari - Ikulu, Idara ya Ushirikiano wa Kimataifa na Uratibu wa Wazanzibari Wanaoishi nje ya nchi, Idara ya Uendeshaji na Utumishi, Idara ya Mipango, Sera na Utafiti, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi - Pemba; Ofisi ya Usalama wa Serikali na Idara ya Ufuatiliaji na Tathmini ya Sera na Maamuzi ya Serikali. Aidha, Fungu A02 linaundwa na Ofisi ya Baraza la Mapinduzi.

Mhe. Spika, kwa mwaka 2016/17, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi imetengewa jumla ya TZS. 6,990.2 milioni kwa ajili ya matumizi ya utekelezaji wa programu zake. Kati ya hizo, TZS. 500.0 milioni kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo na TZS. 6,490.2 kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida.

PROGRAMU KUBWA NA NDOGO NA MAKISIO YA FEDHA ZINAZOHITAJIKA KWA MWAKA WA FEDHA 2016/2017

Mhe. Spika, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi imeandaa Programu Kuu tano na Programu Ndogo 14. Naomba niainishe Programu Kuu na Ndogo kwa mwaka wa fedha 2016/2017 pamoja na fedha zinazohitajika katika kila programu.

Mhe. Spika, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Fungu A01 ina jumla ya Programu Kuu tatu na Programu Ndogo tisa kama ifuatavyo:-

Programu ya Kusimamia Shughuli za Mheshimiwa Rais na Kuimarisha Mawasiliano Ikulu

Matokeo ya muda mrefu yanayotarajiwa kupitia programu hii ni Umma kwa ujumla kuwa na uelewa kuhusu shughuli zinazotekelezwa na Mheshimiwa Rais. Lengo kuu la Programu ni kusimamia shughuli za Mhe. Rais na kuendeleza taswira nzuri kwa umma. Vile vile, programu hii itajumuisha mradi wa maendeleo wa ujenzi wa nyumba za Ikulu na Nyumba za Serikali. Programu hii itakuwa na programu ndogo mbili zifuatazo:-

i. Programu Ndogo ya Uratibu wa Shughuli za Mhe. Rais
ii. Programu Ndogo ya Uimarishaji wa Mawasiliano baina ya serikali na wananchi

Mhe. Spika, katika kufikia malengo ya programu hii, shughuli zifuatazo zimepangwa kutekelezwa:-

i. Kufuatilia na kutekeleza ahadi na maagizo ya Mhe. Rais;
ii. Kuratibu ziara za ndani na nje za Mhe. Rais;
iii. Kuimarisha huduma katika Ikulu za Unguja, Dodoma na Dar es Salaam;
iv. Ujenzi wa Ikulu ya Micheweni, ujenzi wa nyumba ya Chake Chake na kulinda na kuzuia mmong'onyoko wa udongo katika Ikulu ya Mkoani;
v. Kukuza mawasiliano baina ya Mhe. Rais na wananchi kwa kuimarisha tovuti ya Idara ya Mawasiliano na Habari – Ikulu na mitandao ya kijamii; na
vi. Kuchapisha na kusambaza kalenda, majarida na vipeperushi vya Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

Mhe. Spika, ili Programu ya Kusimamia Shughuli za Mhe. Rais na Kuimarisha Mawasiliano Ikulu iweze kutekelezwa, kwa mwaka wa fedha 2016/2017, jumla ya TZS. 2,867.4 milioni zinahitajika kwa matumizi ya kazi za kawaida zilizopangwa na TZS. 500.0 milioni kwa ajili ya mradi wa maendeleo.

Programu ya Ushirikiano wa Kikanda, Kimataifa na Uratibu wa Wazanzibari Wanaoishi nje ya nchi

Matokeo ya muda mrefu yanayotarajiwa kupitia programu hii ni Zanzibar kufaidika na fursa za kiuchumi na kijamii zinazotokana na jumuiya za kikanda na kimataifa na Wazanzibari wanaoishi nje ya nchi. Malengo makuu ya programu hii ni kuimarisha mtengamano wa Kikanda, Taasisi za Kimataifa na ushirikiano mwema na nchi marafiki na kutumia fursa za kiuchumi na kijamii zinazotokana na jumuiya hizo na Wazanzibari wanaoishi nje ya nchi. Programu hii itakuwa na programu ndogo mbili zifuatazo:-

i. Programu Ndogo ya Kuiwakilisha Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika mikutano ya Kikanda na Kimataifa
ii. Programu Ndogo ya Uratibu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika masuala ya *Diaspora*

Mhe. Spika, katika kufikia malengo ya programu hii, shughuli zifuatazo zimepangwa kutekelezwa:-

i. Kushiriki katika mikutano ya kikanda ndani na nje ya nchi;
ii. Kushughulikia masuala ya kuwaunganisha *Diaspora* na jumuiya zake;
iii. Kuandaa kongamano la Watanzania wanaoishi nje ya nchi; na
iv. Kutoa taaluma kwa jamii juu ya umuhimu na fursa za mtengamano wa Kikanda na elimu juu dhana ya *Diaspora*.

Mhe. Spika, ili Programu ya Ushirikiano wa Kimataifa na Uratibu wa Wazanzibari Wanaoishi nje ya nchi iweze kutekelezwa, kwa mwaka wa fedha 2016/2017, jumla ya TZS. 504.5 milioni zinahitajika kwa matumizi ya kazi za kawaida zilizopangwa katika programu hii.

Programu ya Utumishi na Uendeshaji wa Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi

Matokeo ya muda mrefu yanayotarajiwa katika programu hii ni kuimarika kwa mazingira ya utendaji kazi katika Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Programu hii inalenga kuimarisha uwezo wa Kiutendaji na Kuratibu Shughuli za Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Unguja na Pemba. Aidha, inalenga Kuimarisha Shughuli za Mipango, Sera na kufanya Utafiti. Kuimarisha shughuli za Usalama wa Serikali. Programu hii itakuwa na programu ndogo tano zifuatazo:-

i. Programu ndogo ya Uratibu wa Shughuli za Mipango, Sera na Utafiti za Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi
ii. Programu ndogo ya Uratibu na Usimamizi wa Shughuli za Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi
iii. Programu ndogo ya Uratibu na Usimamizi wa Shughuli za Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi – Pemba
iv. Usimamizi wa Usalama wa Watumishi wa Umma
v. Ufuatiliaji na Tathmini ya Sera na Maamuzi ya Serikali

Mhe. Spika, katika kufikia malengo ya programu hii, shughuli zifuatazo zimepangwa kutekelezwa:-

i. Kupitia '*database'* ya maendeleo ya rasilimali watu;
ii. Kulipa mishahara kwa wafanyakazi, motisha pamoja na stahiki nyengine;

iii. Kuimarisha huduma na vitendea kazi za Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi;
iv. Kuandaa vikao vya Kamati ya Uongozi, Bodi ya Zabuni na Kamati ya Ukaguzi wa ndani;
v. Kuandaa mafunzo ya mpango wa rasilimali watu, urithishaji pamoja na kuwajengea uwezo wa kitaaluma wafanyakazi;
vi. Kufanya mapitio ya mpango mkakati wa Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na mpango mkakati wa mawasiliano Ikulu;
vii. Kufanya utafiti juu ya utoaji wa huduma katika Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi;
viii. Kuimarisha ufuatiliaji na tathmini wa shughuli za Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi;
ix. Kufanya upekuzi wa kiusalama kwa wafanyakazi na ukaguzi wa majengo ya serikali; na
x. Kuimarisha utendaji kazi na huduma za Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Pemba na Ikulu za Pemba.

Mhe. Spika, ili Programu ya Utawala na Uendeshaji wa Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi iweze kutekelezwa, kwa mwaka wa fedha 2016/2017, jumla ya TZS. 2,126.3 milioni zinahitajika kwa matumizi ya kazi zilizopangwa katika programu hii.

Mhe. Spika, **k**wa mwaka wa fedha 2016/2017, Ofisi ya Baraza la Mapinduzi yenye Fungu A02 itakuwa na jumla ya Programu Kuu mbili na Programu Ndogo tano zifuatazo:-

Programu ya Usimamizi wa Majukumu ya Kikatiba na Kisheria ya Baraza la Mapinduzi na Kamati ya Makatibu Wakuu

Matokeo ya muda mrefu yanayotarajiwa kwenye programu hii ni Kuimarika kwa Sheria, Sera na Miongozo yenye kusaidia ukuaji wa maendeleo na kudumisha amani na utulivu. Programu hii inalenga kuhakikisha kuwa uwajibikaji wa serikali katika kutoa huduma kwa wananchi. Programu hii itakuwa na programu ndogo tatu zifuatazo:-

i. Programu Ndogo ya Uratibu na Usimamizi wa Shughuli za Baraza la Mapinduzi na Kamati zake
ii. Programu Ndogo ya Tathmini ya Uwajibikaji na Utendaji Kazi wa Taasisi za Umma

iii. Programu Ndogo ya Ukuzaji Ufanisi wa Kitengo cha Teknolojia ya Habari na Mawasiliano

Mhe. Spika, katika kufikia malengo ya programu hii, shughuli zifuatazo zimepangwa kutekelezwa:-

i. Kutayarisha vikao vya kawaida na dharura vya Baraza la Mapinduzi na Kamati zake ikiwemo Kamati ya Makatibu Wakuu;
ii. Kutoa mafunzo ya kujenga uwezo kwa Viongozi wa Wakuu wa Kisiasa na Kiutendaji na Sekretarieti ya Baraza la Mapinduzi;
iii. Kutayarisha mikutano ya tathmini ya utendaji kazi na uwajibikaji (Bango Kitita) kati ya Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mpinduzi na Viongozi wa Wizara, Idara na Taasisi nyengine za Serikali; na
iv. Kuratibu shughuli za Mawaziri Wasio na Wizara Maalum.

Mhe. Spika, ili Programu ya Usimamizi wa Majukumu ya Kikatiba na Kisheria ya Baraza la Mapinduzi na Kamati ya Makatibu Wakuu iweze kutekelezwa ipasavyo, kwa mwaka wa fedha 2016/2017, jumla ya TZS. 176.5 milioni zinahitajika kwa matumizi ya kazi za kawaida zilizopangwa katika programu hii.

Programu ya Utumishi na Utawala wa Ofisi ya Baraza la Mapinduzi

Matokeo ya muda mrefu ya programu hii ni kuwa na mfumo bora na wa kisasa wa kuendesha shughuli za ofisi na uhifadhi nyaraka na kumbukumbu. Lengo kuu ni kuimarisha mazingira ya kazi, mahusiano ya umma na kuongeza ujuzi wa wafanyakazi. Programu hii itakuwa na Programu Ndogo mbili zifuatazo:-

i. Programu Ndogo ya Utumishi na Uendeshaji wa Ofisi ya Baraza la Mapinduzi
ii. Programu Ndogo ya Uimarishaji Uwezo wa Ofisi katika Kutunga na Kusimamia Sera, Sheria na Utumishi wa Umma

Mhe. Spika, katika kufikia malengo ya programu hii, shughuli zifuatazo zimepangwa kutekelezwa:-

i. Kuimarisha miundombinu ya ofisi, majengo pamoja na mazingira yake;

ii. Kuiwakilisha nchi katika Mikutano, Warsha na Makongamano nje ya nchi kwa lengo la kujifunza mafanikio yaliyofikiwa na mataifa rafiki;
iii. Kutoa mafunzo ya muda mfupi na mrefu kwa wafanyakazi wa ofisi;
iv. Kuanzisha maktaba ya ofisi;
v. Kuimarisha kitengo cha uhifadhi wa kumbukumbu za BLM na kamati zake;
vi. Kutayarisha Ripoti ya Mwaka ya Hali ya Utumishi wa Umma; na
vii. Kukusanya na kufuatilia utekelezaji wa Sera, Sheria na Miongozo ya Baraza la Mapinduzi.

Mhe. Spika, ili Programu ya Utumishi na Utawala wa Ofisi ya Baraza la Mapinduzi iweze kutekelezwa kwa ufanisi, kwa mwaka wa fedha 2016/2017, jumla ya TZS. 1,315.5 milioni zinahitajika kwa matumizi ya kazi za kawaida zilizopangwa katika programu hii.

VIPAUMBELE VIKUU VITAKAVYOTEKELEZWA NA ORMBLM KWA MWAKA WA FEDHA WA 2016/2017

Mhe. Spika, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa mwaka wa fedha 2016/2017 imepanga shughuli zake kwa kuzingatia vipaumbele vifuatavyo:-

i. Kuanza ujenzi wa Ikulu ya Micheweni na kuimarisha usalama katika nyumba za Ikulu;
ii. Kusimamia majukumu ya Kikatiba na Kisheria ya Baraza la Mapinduzi na Kamati zake;
iii. Kuimarisha mawasiliano baina ya Mhe. Rais na Wananchi kwa kutumia mtandao; na
iv. Kuandaa kongamano la Watanzania wanaoishi nje ya nchi.

MAOMBI YA FEDHA KWA KAZI ZILIZOPANGWA KUTEKELEZWA KATIKA MWAKA WA FEDHA 2016/2017

Mhe. Spika, ili kuiwezesha Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kutekeleza kazi zilizopangwa kwa mwaka 2016/2017, naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha makadirio ya matumizi ya Programu za Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi zenye jumla ya TZS. 6,990.2 milioni. Kati ya fedha hizo, TZS. 6,490.2 milioni kwa ajili ya matumizi ya

Kazi za Kawaida na TZS. 500.0 milioni kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Mgawanyo wa fedha zitakazotumika kwa utekelezaji wa kila programu zimeainishwa katika Kiambatisho Namba 2.

HITIMISHO

Mhe. Spika, kabla ya kumalizia hotuba yangu, naomba kutoa wito kwetu sote tukiwa Wawakilishi wa Wananchi kuwa mstari wa mbele katika kuhubiri amani, kusimamia shughuli za wananchi na kutekeleza ahadi tulizozitoa wakati wa kuomba ridhaa yao ya kuwaongoza majimboni kwetu. Vile vile, naomba kwa umoja wetu tuendelee kumpa mashirikiano makubwa Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ili aweze kutuongoza vyema na kufikia malengo tuliyoyakusudia.

Mhe. Spika, kwa njia ya kipekee naomba kuwapongeza na kuwashukuru kwa dhati Viongozi na Watendaji wa Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi wakiwemo Washauri wa Rais, Katibu wa Baraza la Mapinduzi na Katibu Mkuu Kiongozi Dkt. Abdulhamid Yahya Mzee, Katibu Mkuu Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Ndugu Salum Maulid Salum (Kibanzi), Naibu Katibu Baraza la Mapinduzi Ndugu Salmin Amour Abdalla, Katibu wa Rais na Naibu Katibu wa Rais na Wasaidizi wa Rais, Wakurugenzi na wafanyakazi wote kwa upendo na mashirikiano yao kazini. Katika kipindi kifupi cha kufanya kazi nao nimeshuhudia utendaji uliyo makini, ubunifu na ari ya kupigiwa mfano katika kujituma kwao, naomba wazidishe juhudi hizo ili tuweze kufikia malengo tuliyoyakusudia.

Mhe. Spika, kwa kumalizia naomba niwashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe kwa utulivu na umakini wenu mkubwa katika kunisikiliza.

Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.

(Hoja imetolewa iamuliwe)

Mhe. Simai Mohammed Said (Kny: Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa): Ahsante Mhe. Spika, na mimi kwa ruhusa yako, naomba kwa niaba ya Mwenyekiti wetu niweze hotuba ya maoni ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kuhusiana na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa mwaka fedha 2016/2017.

Mhe. Spika, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa utukufu kwa kutujaalia uzima na afya njema tukaweza kukutana tena katika Baraza hili la Tisa kwa ajili ya kuendelea kuwatumia wananchi wetu. Aidha, kukushukuru na kukupongeza wewe Mhe. Spika, kwa kuchaguliwa kwako kuliongoza Baraza hili Tukufu. Ni imani yangu kwamba utaliongoza Baraza hili kwa uadilifu wa hali ya juu na kuimarisha demokrasia katika chombo hichi muhimu cha wananchi.

Mhe. Spika, ninapenda kuchukua nafasi hii kuwapongeza Wawakilishi wote waliomo katika Baraza lako Tukufu kwa kuchaguliwa kwao kuja kuwakilisha wananchi. Ni wazi kwamba wananchi wamejenga imani kubwa kwetu. Nasi ahadi kwao ni kama tutawatumikia kwa dhati kama ambavyo walivyotuamini kutuleta katika chombo hichi kwa lengo la kutetea maslahi yao.
Mhe. Spika, sina budi pia kumshukuru Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na watendaji wake wote, wakiongozwa na Katibu Mkuu kwa mashirikiano waliyotupatia wakati wa kupitia makadirio ya bajeti ya wizara hii. Lakini pia niwashukuru Wajumbe wa Kamati yetu kwa umoja wao na kazi nzuri waliyoifanya kiasi cha kunirahishia kazi yangu ya kuongoza kikao kuwa nyepesi zaidi. Kwa hakika ni Wajumbe mahiri ambapo licha ya upya wao katika Baraza hili na hususan katika Kamati hii, wameweza kuijadili ipasavyo na kuhoji mambo mbali mbali kwa lengo la kuhakikisha kwamba fedha wanazoziidhinisha zinatumiwa kwa matumizi yaliyokusudiwa.

Mhe. Spika, kwa heshima ya hali ya juu ninapenda kuwatambua Wajumbe hao kwa majina kama ifuatavyo:-

1.Mhe. Omar Seif Abeid	-	Mwenyekiti
2.Mhe. Panya Ali Abdalla	-	Makamo Mwenyekiti
3.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	-	Mjumbe
4.Mhe. Hussein Ibrahim Makungu	-	Mjumbe
5.Mhe. Simai Mohammed Said	-	Mjumbe
6.Mhe. Mussa Ali Mussa	-	Mjumbe
7.Mhe. Mtumwa Suleiman Makame	-	Mjumbe
8.Mhe. Simai Mohammed Said	-	Mjumbe

Aidha, Kamati yetu inafanya kazi na makatibu wawili ambao kwa kiasi kikubwa wamekuwa wakitusaidia sana katika kutekeleza majukumu yetu. Makatibu hao ni:-

1. Ndg. Maryam Rashid Ali
2. Ndg. Othman Ali Haji

Mhe. Spika, ikumbukwe kwamba miongoni mwa majukumu ya msingi ya Kamati yetu ni kuchambua mapendekezo ya Serikali kuhusu makadirio ya wizara ya husika ya mapato na matumizi ya kila mwaka. Hivyo katika kutekeleza jukumu hilo lililoelezwa katika Kanuni ya 114(e), Kamati yangu ilikaa na kuijadili na hatimaye kupitisha Makadirio ya Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi mnamo tarehe 10/05/2016.Na leo hii kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Kamati ninawasilisha maoni ya Kamati kuhusiana na bajeti hiyo.

Mhe. Spika, baada ya utangulizi huo mfupi sasa naomba nitekeleze jukumu nililopewa na Kamati la kuwasilisha maoni yetu hapa mbele ya Baraza lako Tukufu moja kwa moja.

Kuhusu Mfumo wa Bajeti wa PBB:

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuanzia mwaka wa fedha 2015/2016, imeanzisha mfumo wa bajeti unaozingatia programu *(Programme Based Budget)* ambapo kwa bajeti hii itakuwa ni kipindi cha pili kutekelezwa licha kuwa ilishaanzwa kutekelezwa kwa mwaka wa fedha uliopita. Bado mfumo huu unabakia kuwa mfumo mpya kwa Wajumbe wako ukizingatia kwamba asilimia kubwa ya Wajumbe wa Baraza hili ni wapya. Hivyo mfumo huu wa *PBB* imekuwa ni changamoto kwao kuweza kuufahamu kwa ghafla na kupelekea ugumu kidogo kuweza kumudu kufanya uchanganuzi wa vitabu vya vitabu vilivyoletwa katika Kamati zako. Sambamba na hilo Wajumbe hawakupatiwa mafunzo ya kutosha lakini hata hivyo wamejitahidi kadri ya uwezo wao kuweza kuchambua bajeti hiyo kwa msaada wa Makatibu wetu ambao kwa kweli tunawashukuru sana.

Mhe. Spika, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa mwaka 2016/2017 ina mafungu mawili ambayo ni AO1 na AO2. Na imepanga kutekeleza programu kuu tano zenye programu ndogo kumi na nne ambazo kwa ujumla fedha iliyoombwa kwa Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ni Bilioni sita mia nne na tisini milioni na laki mbili.

Fungu la AO1 Ofisi Ikulu ina jumla ya programu kuu tatu na programu ndogo tisa. Programu kuu ni zifuatavyo:-

1. Programu ya kusimamia shughuli za Mhe. Rais na kuimarisha mawasiliano Ikulu
2. Programu ya ushirikiano wa kikanda, kimataifa na uratibu wa Wazanzibari nchi za nje (*DIASPORA*)

3. Programu ya utawala na uendeshaji Ofisi ya Rais Ikulu

Programu ndogo hizi zifuatazo:-

1. Programu ndogo ya uratibu wa shughuli za Mhe. Rais
2. Programu ndogo ya kuimarisha mawasiliano baina ya Mhe. Rais na wananchi
3. Programu ndogo ya kuiwakilisha Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika mikutano ya kikanda na kimataifa
4. Programu ndogo ya uratibu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika masuala ya *DIASPORA*
5. Programu ndogo ya uratibu na usimamizi wa shughuli za Ofisi Ikulu
6. Programu ndogo ya uratibu wa shughuli za mipango, sera na utafiti za Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi
7. Programu ndogo ya kuratibu na kusimamia shughuli za uratibu na usimamizi wa shughuli za Ofisi ya Rais Ikulu na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Pemba
8. Programu ndogo ya usimamizi wa usalama wa watumishi wa umma
9. Programu ndogo ya ufuatiliaji na tathmini ya sera na maamuzi ya serikali

Programu ya Kusimamia Shughuli za Mhe. Rais na Kuimarisha Mawasiliano Ikulu:

Mhe. Spika, programu hii ina jukumu la kusimamia shughuli za Mhe. Rais pamoja na kuimarisha mawasiliano. Programu hii ina programu ndogo mbili ambazo ni Programu ndogo ya uratibu wa shughuli za Mhe. Rais ambayo imetengewa shilingi bilioni mbili, mia sita na saba milioni na elfu tatu. Na shughuli zinazotarajiwa kutekelezwa ni pamoja na kufuatilia ahadi na maagizo ya Mhe. Rais, kuratibu ziara za ndani na za nje za Mhe. Rais, kutoa viburudishaji kwa wageni wa Mhe. Rais, kuchapisha hotuba na mambo mengine ya Mhe. Rais na kutoa zawadi kwa wageni kwa Mhe. Rais.

Mhe. Spika, programu ndogo ya pili ya kuimarisha mawasiliano baina ya Mhe. Rais na wananchi ambayo imepangwa shilingi milioni mia mbili, laki tatu na hamsini na moja elfu. Na shughuli zinazotekelezwa kwa fedha hizo ni pamoja na kutayarisha, kuchapisha na kusambaza kalenda za Ofisi ya Rais, kutayarisha, kuchapisha na kusambaza jarida la Ikulu, vipeperushi na

machapisho, kuimarisha tovuti ya Idara ya Mawasiliano. Kwa ujumla programu kuu ya kusimamia shughuli za Mhe. Rais imepangiwa kutumia shilingi bilioni mia nane, sitini na saba milioni, laki tatu na hamsini na tatu elfu.

Mhe. Spika, kamati yetu imeridhika na makadirio yaliyopangwa katika programu hii na ilipendekeza mambo mbali mbali ambayo yatakapozingatiwa yataboreshwa kwa kiasi kikubwa kumtangaza Rais wetu na kumfanya awe karibu na wananchi wake waliopo hapa nchini lakini pia hata wanaoishi nchi za nje. Kwanza kamati yangu katika kuona mawasiliano yanaimarika baina ya Rais wetu na wananchi ni vyema Idara ya Mawasiliano mbali na kusambaza na majarida na kalenda, mtangaze Rais kwa kutumia mfumo wa kisiasa wa teknolojia na mawasiliano kwa kutumia njia zinazoendana na dunia ya leo *(New Media),* kama vile *facebook, twitter, youtube.* Mfano pia *clips* muhimu za Rais, *short clips* za sekunde thalathini hadi sekunde arobaini kwa ajili ya *whatsApp* ili watu waone shughuli anazozifanya Mhe. Rais pamoja na kutambulika katika ulimwengu mzima kwa jinsia zote na rika zote.(*Makofi*)

Mhe. Spika, aidha kamati yetu inashauri kwamba Mhe. Rais angekuwa na utaratibu wa kuwaalika na kukaa pamoja na wawekezaji, wafanyabiashara na wadau mbali mbali wa maendeleo kwa lengo la kuzungumza na kubadilishana nao mawazo. Lakini pia kuwashukuru wale ambao wamekuwa wakiisaidia nchi yetu kwa njia moja au nyengine. Jambo hili linaweza kuongeza hamasa kwa wafanyabiashara na wawekezaji kuwekeza zaidi katika sekta mbali mbali.

Aidha, pale ambapo kunatokezea mgeni mashuhuri ambaye anastahiki kupewa zawadi, basi zawadi atakayopewa iwe ni zawadi yenye asili na iliyotengenezwa kwa ubunifu na iambatanishwe pamoja na historia ya mtengenezaji ili kuhakikisha kuwa mgeni anapopewa zawadi hiyo, basi anapata kujua historia ya Zanzibar ambayo wanaweza kuweka kumbukumbu katika Makumbusho yao lakini pia itaitangaza nchi katika masuala ya utalii.

Programu ya Ushirikiano wa Kikanda, Kimataifa na Uratibu wa Wazanzibari Wanaoishi Nchi za Nje:

Mhe. Spika, programu hii ina lengo la kuiwezesha Zanzibar kushiriki katika mikutano ya kikanda na kimataifa na kuwashirikisha ipasavyo Wazanzibari wanaoishi nje ya nchi katika maendeleo ya kiuchumi na kijamii ya nchi yao. Programu hii ina programu ndogo mbili ambazo programu ndogo ya kuwakilishi Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika mikutano ya kikanda na kimataifa ambayo imepangiwa kutekelezwa kwa shilingi mia mbili sitini na nne milioni, laki sita na sabini na tatu elfu ambapo miongoni mwa shughuli

zitakazofanywa ni pamoja na kuimarisha ushiriki wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika mikutano ya kikanda, kuendesha vikao vya ndani vya sekta kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, kushiriki katika mikutano ya mashauriano ili kupata msimamo mmoja wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kushiriki katika mikutano ya kikanda nje na ndani ya nchi na kutoa elimu kwa jamii juu ya umuhimu wa mtengamano wa Jumuiya za kikanda.

Mhe. Spika, programu ndogo ya pili ya uratibu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika masuala ya *DIASPORA* ambayo imepangwa kutekelezwa kwa shilingi mia mbili na thalathini na tisa milioni, laki nane arobaini na saba elfu. Na shughuli zilizopangwa katika kutekelezwa ni pamoja kushiriki katika mikutano ya mashauriano ya *DIASPORA* na Idara inayoshughulikia masula ya *DIASPORA* Dar es Salaam, kutoa elimu kwa jamii juu ya dhana ya *DIASPORA* na umuhimu wake, kushiriki mkutano wa wadau wa maendeleo kujadili agenda za *DIASPORA*, kuandaa kongamano la Watanzania wanaoishi nchi za nje na kusimamia shughuli za kila siku ya Idara ya Ushirikiano Kimataifa na Uratibu wa *DIASPORA*. Kwa ujumla programu ya ushirikiano wa kikanda, kimataifa na uratibu wa Wazanzibari wanaoishi nchi za nje imekadiriwa kutekelezwa kwa shilingi milioni mia tano na nne, laki tano na ishirini elfu.

Mhe. Spika, katika kuona azma ya kuwepo kwa Idara ya Uratibu wa Wazanzibari wanaoishi nchi za nje inazaa matunda. Kamati yangu inashauri kwamba wafanyakazi wote wanaokwenda ziara nchi za nje au kushiriki mikutano nchi za nje, wawasilishe ripoti za ziara au safari hizo kwa ujumla wake serikalini, ili ripoti hizo zifanyiwe kazi ili kuleta mafanikio kwa taifa letu. Sambamba na hilo safari hizo ziweze kuleta tija ya kuibua miradi mbali mbali kutoka kwa wahisani lakini pia wanapokwenda huko waitangaze vyema nchi yetu ili wawekezaji wavutike kuja kuwekeza katika sekta mbali mbali.

Mhe. Spika, kamati yetu katika suala zima la safari za nje wanazokwenda Mawaziri na watendaji mbali mbali wa Serikali, inataka kusisitiza juu ya ripoti wanazowasilisha Mawaziri husika katika Baraza la Mawaziri ziambatane na ripoti za utekelezaji wake ili tuone tija ya kweli inapatikana kwa nchi yetu. Aidha, kamati ilitaka kujua juu ya ziara za viongozi wakuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wanaposafiri safari za nje na kushauri kwamba wakati viongozi hao wanaposafiri, ni vyema wakajitayarisha na kuzingatia faida pamoja na fursa watakazozipata ziinufaishe na Zanzibar.

Mhe. Spika, aidha kamati iliishauri serikali kuwa na mashirikiano ya karibu na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hasa katika Wizara ambazo

hazihusiani na Muungano, lakini zenye sura ya Kimuungano. Kwa mfano, afya, elimu, utalii na kadhalika. Kamati pia ilihoji juu ya uhusiano uliopo baina ya Commoro na Tanzania hususan katika suala la Kampuni inayoitwa Hairu ambayo ni kampuni ya mvuvi iliyokuwa ije kuwekeza Zanzibar katika masuala ya uhifadhi wa samaki ambapo kamati ilipatiwa taarifa kama mipango inaendelea katika kufanikisha mradi huo.

Programu ya Utawala na Uendeshaji wa Ofisi ya Rais Ikulu:

Mhe. Spika, programu hii ina malengo ya kuimarisha shughuli na mipango, kuandaa na kuchambua sera na utafiti pamoja na kuimarisha uwezo wa kiutendaji na uratibu wa shughuli za Ofisi ya Rais Ikulu. Programu hii ina programu ndogo tano ambazo ni progrmu ndogo ya uratibu na usimamizi wa shughuli za Ofisi ya Rais Ikulu ambayo imepangiwa kutekelezwa kwa shilingi bilioni moja, mia moja na ishirini na sita milioni, laki tatu na ishirini na sita elfu ambazo zinakadiriwa kutumika katika shughuli za kusimamia utendeshaji wa Ofisi ya Rais Ikulu kwa kulipa mishahara, kununua vifaa vya usafiri, kuboresha na kukarabati vitendea kazi, Ofisi ya Majengo, kutoa huduma za kiutawala, kutoa mafunzo kwa waajiriwa wapya kumi na mbili na nyenginezo kama zinavyoonekana katika kitabu cha makadirio ya mapato na matumizi ya mwaka 2016/2017.

Mhe. Spika, katika programu ndogo hii kamati yangu inashauri kwamba ili jengo la Ikulu la Mnazi Mmoja liweze kuwa na haiba na mvuto zaidi kwa shughuli za Mhe. Rais ni vyema lifanyiwe ubunifu katika sehemu yake ya nyuma iliyo mkabala na bahari kwa kujengwa *jet* ambayo itaingia katika eneo la ufukwe wa bahari uliopo na kusanifiwa katika mtindo wa utamaduni wetu ambayo sehemu hiyo ataitumia Rais anapokuwa na wageni wake mashuhuri ili kupata utulivu katika hewa nzuri ya upepo wa bahari ya Hindi na kuwafanya wageni wavutike kuwekeza Zanzibar. (*Makofi*)

Mhe. Spika, programu ndogo ya pili ya uratibu wa shughuli za mipango, sera na utafiti za Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ambayo imekadiriwa kutekelezwa kwa TZ shilingi milioni mia tatu, laki saba na sabini na nane elfu zitakazotumika kwa kulipa mishahara kwa wafanyakazi na stahiki nyengine, kutoa mafunzo ya muda mrefu, kusimamia na kuiwisha tovuti ya Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, kufanya tathmini hali ya TEHAMA katika Ofisi ya Rais na Mwenyekiti, kuandaa na kuratibu vikao vya matayarisho ya hotuba ya bajeti na kadhalika.

Mhe. Spika, programu ndogo ya tatu ni ya kuyaratibu na kusimamia shughuli za uratibu na usimamizi wa shughuli za Ofisi ya Rais Ikulu na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Pemba. Programu hii imekaridiwa kutumia milioni mia sita, sitini na tatu na laki moja na kumi na tatu elfu ambazo zinatarajiwa kutumika kwa kutoa na kuratibu huduma za utawala, kulinda, kuhifadhi na kutoa huduma kwa Ikulu na nyumba za serikali zilizopo Pemba, kulipa mishahara na stahiki kwa wafanyakazi wa Pemba, kutoa huduma za usafiri, zana na matengenezo yake, kukarabati na majengo ya ofisi na ununuzi wa samani za ofisi.

Mhe. Spika, kamati yetu kupitia programu ndogo ya uratibu na usimamizi wa Ofisi ya Rais Ikulu na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Pemba inashauri kwamba jengo la Ikulu ya Chake Chake kufanyiwa ukarabati mkubwa, kwani haifanani na hadhi ya kuwa nyumba ya kukaa kiongozi mkubwa wa nchi. Kwani hali yake hairidhishi.(Makofi)

Vile vile kamati inapendekeza kuondoshwa kwa maofisa wa serikali ikiwa ni pamoja na maofisa wa Mahakama wanaokaa katika nyumba iliopo katika eneo la Ikulu ili nyumba hiyo iweze kufanyiwa ukarabati. Sambamba na hilo, kamati yangu ilitaka kujua juu ya matengenezo ya nyumba ya Ikulu ya Mkokotoni ambayo inahitaji kujengewa uzio kwa ajili ya kuzuia uingiaji ovyo wa watu katika eneo hilo.

Aidha, kamati inashauri kwamba wizara hii ikae pamoja na Waziri anayehusika na vikosi ili kukarabati sehemu ambayo askari wa KMKM wanakaa wakati wanapofanya kazi zao za ulinzi ili iendane na eneo hilo la Ikulu. (*Makofi*)

Mhe. Spika, programu ndogo ya nne ya usimamizi wa usalama wa watumishi wa umma ambayo imekadiriwa kutumia bilioni arobaini ambazo fedha hizo zinatarajiwa kutumika katika usalama wa mali, majengo ya serikali kwa Unguja na Pemba, kufanya ukaguzi wa kiusalama wa muda mfupi na endelevu kwa wafanyakazi, kuendesha mafunzo na semina kwa watumishi. Kamati inashauri kwamba ili wafanyakazi wafanye kazi katika mazingira yaliyo salama zaidi, ni vyema ukaguzi wa kiusalama wa majengo ukafanyika mara kwa mara, kwani kuna taasisi na idara mbali mbali ambazo wanafanya kazi katika majengo ambayo sio salama na hivyo kuhatarisha usalama wa wafanyakazi.

Mhe. Spika, kwa ujumla wake Programu kuu ya Programu ya Utawala na Uendeshaji wa Ofisi ya Rais Ikulu imekadiriwa kutumia TZS 2,126,326,000, (Bilioni mbili mia moja ishirini na sita milioni laki tatu na ishirini na sita elfu) ambazo kamati yangu inaona bado ni fedha chache kutengwa kwa Ofisi kubwa

kama hii, hususan ukizingatia uchakavu wa nyumba za Ikulu zinazohitaji kufanyiwa ukarabati ili ziweze kuendana na hadhi ya Rais wetu

Mhe. Spika, kamati yangu pia imepitia fungu A02 Ofisi ya Baraza la Mapinduzi, ambalo ni fungu linalojitegemea na kusimamiwa na Naibu Katibu Mkuu wa Baraza la Mapinduzi, Fungu hili lina program kuu mbili na program ndogo tano, program kuu ni:-

1. Programu ya usimamizi wa majukumu ya kikatiba na kisheria ya Baraza la Mapinduzi
2. Programu ya Utumishi na Utawala wa Ofisi ya Baraza la Mapinduzi,

Kwa upande wa program ndogo ni:-

I. Programu ndogo ya Uratibu na Usimamia Shughuli za Baraza la Mapinduzi na kamati zake
II. Programu ndogo ya tathmini ya uwajibikaji na utendaji kazi wa Taasisi za Umma
III. Programu ndogo ya kukuza ufanisi wa kitengo cha Teknologia ya Habari na Mawasiliano
IV. Program ndogo ya utumishi na uendeshaji wa Ofisi ya Baraza la Mapinduzi
V. Program ndogo ya pili ni uimarishaji uwezo wa Ofisi katika kusimamia Sera, Sheria na Utumishi wa Umma.

PROGRAMU YA USIMAMIZI WA MAJUKUMU YA KIKATIBA NA KISHERIA YA BARAZA LA MAPINDUZI NA KAMATI YA MAKATIBU WAKUU

Mhe. Spika, Programu ya usimamizi wa Majukumu ya kikatiba na kisheria ya Baraza la Mapinduzi na Kamati ya Makatibu Wakuu ambayo kwa ina lengo la kutayarisha na kusimamia vikao vya Baraza la Mapinduzi na Kamati ya Makatibu Wakuu, programu hii ina Programu ndogo tatu, programu ndogo ya kwanza ni ya kuratibu na kusimamia shughuli za Baraza la Mapinduzi na kamati zake ambayo imekadiriwa kutekelezwa kwa TZS 109,200,000 (Milioni mia moja na Tisa na laki mbili) ambazo zitatumika katika kutayarisha vikao 12 vya BLM na Kamati zake, kutayarisha vikao 12 vya Kamati za Baraza la Mapinduzi kutayarisha vikao 8 vya dharura vya BLM na 8 vya kamati ya Makatibu Wakuu wa SMZ, kutoa mafunzo ya kujenga uwezo kwa viongozi wa kisiasa na Sekretarieti ya Baraza la Mapinduzi.

Mhe. Spika, Program ndogo ya pili ni ya tathmini ya uwajibikaji na utendaji kazi wa Taasisi za Umma, ambayo imekadiriwa kutekelezwa kwa TZS 35,360,000 (Milioni thelathini na tano laki tatu na sitini elfu) ambazo zitatumika katika shughuli za kutayarisha mikutano miwili ya tathmini ya utendaji kazi kati ya Mhe. Rais na Viongozi wa Wizara za SMZ, kusaidia shughuli za kijamii na masuala mtambuka kupitia Mawaziri wasio na Wizara maalum.

Mhe. Spika, Program ndogo ya tatu ni ya kukuza ufanisi wa kitengo cha Teknologia ya Habari na Mawasiliano ambayo nayo imepangiwa kutekelezwa kwa TZS 31,930,000 (Milioni thelathini na Moja, laki tisa na thelathini elfu) katika kutekeleza shughuli za kusimamia huduma za mkonga wa Taifa wa Mawasiliano katika Ofisi, Kwa ujumla Programu kuu ya usimamizi wa Majukumu ya kikatiba na kisheria ya Baraza la Mapinduzi na Kamati ya Makatibu Wakuu kwa mwaka wa fedha 2016/2017 imekadiriwa kutumia 176,490,000 (Milioni Mia moja sabini na sita laki nne na tisiini elfu).

PROGRAMU YA UTUMISHI NA UTAWALA WA OFISI YA BARAZA LA MAPINDUZI

Mhe. Spika, kamati yangu pia katika Fungu A02 ilipitia Programu kuu ya Utumishi na Utawala wa Ofisi ya Baraza la Mapinduzi yenye lengo la kuimarisha mazingira ya kazi, mahusiano ya umma na kuwaongezea ujuzi wafanyakazi wa ofisi, Program hii ina program ndogo mbili ambazo ni program ndogo ya utumishi na uendeshaji wa Ofisi ya Baraza la Mapinduzi na program ndogo ya uimarishaji uwezo wa ofisi katika kusimamia Sera , sheria na Utumishi wa Umma, Programu ndogo ya utumishi na uendeshaji imepangiwa kutekelezwa kwa TZS 1,179,210,000 (Bilioni moja, mia moja sabini na tisa Milioni, laki mbili na elfu kumi) ambazo zimepangwa kutekelezwa katika shughuli mbali mbali, ikiwa ni pamoja na kuboresha miundombinu ya ofisi, majengo pamoja na mazingira yake, kuiwakilisha ofisi katika mikutano, warsha pamoja na makongamano ya ndani na nje ya nchi, na kurahisisha ufanisi wa shughuli za kiofisi.

Mhe. Spika, Program ndogo ya pili ni uimarishaji uwezo wa ofisi katika kusimamia Sera, Sheria za Utumishi wa Umma, program hii imepangwa kutekelezwa katika mwaka huu wa fedha kwa TZS 136,300,000 (Mia moja thelathini na sita milioni na laki tatu) ambazo zimepangwa kutumika katika kuendesha shughuli za uanzishaji wa Maktaba ya Baraza la Mapinduzi, uimarishaji wa kitengo cha uhifadhi wa kumbukumbu za Baraza la Mapinduzi, kutayarisha ripoti ya mwaka ya hali ya utumishi wa umma pamoja na

ukusanyaji na ufuatiliaji wa Sera,Sheria na Miongozo ya Baraza la Mapinduzi. Kwa ujumla wake Programu kuu ya Utumishi na Utawala wa Ofisi ya Baraza la Mapinduzi katika mwaka wa fedha 2016/2017 imekadiriwa kutumia TZS 1,315,510,000 (Bilioni moja,mia tatu kumi na tano Milioni, laki tano na elfu kumi).

Mhe. Spika, kamati yangu baada ya kuzipitia Programu zote nilizozitaja hapo kabla imeona fedha hizo ni kidogo kutengwa kwa ofisi kubwa kama hii ambayo ndio muhimili wa Serikali yetu, ambayo bado ina changamoto nyingi zinazohitaji kufanyiwa kazi zikiwemo zile za ubovu na uchakavu wa majengo ya nyumba za Ikulu, uhaba wa vitendea kazi, uhaba wa usafiri kwa ajili ya Idara mbali mbali. Hivyo Kamati inashauri kwamba hali itakaporuhusa katika Bajeti ya mwaka ujao 2017/2018 watengewe fedha ambazo zitaweza angalau kupunguza changamoto zinazoikabili Wizara hii muhimu hasa ile ya kukarabati nyumba za ikulu ikiwemo nyumba ya Kupumzikia ya Mkokotoni ambayo inahitaji kujengewa uzio na ile ya Chake Chake ambayo iko katika hali isiyoridhisha.

Mhe. Spika, mwisho napenda kukushukuru tena kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha maoni ya Kamati yangu kwa niaba ya Kamati pamoja na kuwashukuru Wajumbe wa Baraza lako tukufu kwa kunisikiliza, sasa niwaombe Wajumbe wa Baraza lako waijadili na hatimae waiunge mkono bajeti hii ili wamuwezeshe waziri kufanikisha na kutekeleza yale waliojipangia katika mwaka huu wa fedha.

Mhe. Spika, kwa niaba yangu na kwa niaba ya Kamati ya kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa kitaifa naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako sasa na mimi naomba niwe mjumbe wa mwanzo kuchagia bajeti ya Mhe. Waziri ikiwa ni maoni yangu haya nchi ya kamati yetu ambayo nimemalizia punde kuwasilisha hotuba yetu.

Mhe. Spika, ningependa kidogo kuanza na siasa, kwa sababu Rais wetu wa Zanzibar ndiye alama wa nchi yetu na watu wake. *(Makofi)*

Mhe. Spika, nilikuwa na rafiki yangu mpenzi sana ambaye kwa sasa ameshatangulia mbele ya haki, na alikuwa ni mlezi wangu aliyenisaidia kisiasa, ni Marehemu Jecha Thabiti Kombo. Ni mzoefu Mwenyezi Mungu amrehemu na namshukuru mdogo wake leo tuko naye hapa kama Waziri wetu wa Afya.

Mhe. Spika, aliniambia Marehemu Jecha siku moja, nakumbuka ilikuwa mwaka 2005. Akasema kwamba katika Kusini mwa Janga la Kusini la Sahara hakuna chama chochote ambacho kinafanya chaguzi zake, kuanzia shina, tawi, jimbo, wilaya, mkoa, taifa kama Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mhe. Spika, ningewaomba Waheshimiwa Wajumbe munisikilize vizuri, lakini karibuni mambo mengi yanayozungumzwa na wanasiasa ambao wao sio wapenzi au wafuasi wa Chama cha Mapinduzi wanapita maeneo mengi. Hapa natakanioneshe vitu viwili, Chama cha Mapinduzi kinapofanyakazi na uratibu wa kazi zake za kisiasa, kinachukua maoni kutoka chini kinaleta juu, taifa lakini pia kinashusha chini kuwasikiliza wananchi wake.

Mhe. Spika, katika uchaguzi wa marudio Chama cha Mapinduzi kiliwasikiliza wana CCM na wakawa wanasemaje, kwa sababu Tume ya Uchaguzi iko huru na wana CCM wakaleta mapendekezo yao na hatimaye yakatoka chini yakaenda juu na viongozi wakatushirikisha sisi, na Chama cha Mapinduzi kikakubali kushiriki katika uchaguzi wa marudio, na vyama vyengine pia vilikubali kushiriki katika uchaguzi wa marudio. Hawa watani wetu Chama cha Wananchi CUF, maamuzi ya kutoshiriki katika uchaguzi ule ni maamuzi yao, ni matatizo yao. Baraza Kuu lao la CUF ndio lililoamua kufanya maamuzi yale kushusha chini kwa wanachama wao. Sasa kama wanamtafuta adui, inabidi warudi kwenye Baraza Kuu lao wao wenyewe wagombane, kwa sababu mbaya wao yuko juu, wawache kuwalaumu Chama cha Mapinduzi na kututesa sisi. Kwa hivyo, mwacheni Mhe. Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi aendelee na kazi, msimu wa uchaguzi umekwisha, msimu wa siasa umekwisha, sasa hapa ni kazi tu. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kwa vile wizara hii ni muhimu sana ningependa nitoe maoni yangu pia juu ya masuala ambayo yanatukabili katika visiwa, ni suala la mazingira. Mchanga na mawe yanahitajika kujenga katika maeneo mengi katika miji ambayo inaendelea. Lakini kwa sasa unapopanda ndege kwenda juu, natambua kwamba jambo hili ipo wizara husika nitakuja kuyazungumza kwa undani. Lakini nataka nitowe tahadhari kwa wale ambao wanamshauri Rais, pamoja na Wajumbe wa Baraza la Mapinduzi, kwamba visiwa vyetu kwa hali tunavyokwenda huko mbele tunaweza tukajikuta tumebakiwa na mashimo na madimbwi ya maji Zanzibar kisiwa cha Unguja ni *Coral Island*. *(Makofi)*

Mhe. Spika, maeneo mengi yameshavamiwa imefika pahala makaburi ya Mwanakwerekwe pia yanachimbwa mchanga usiku na mchana na pia majimbo mengi yatazidi kuingiliwa na suala hili. Mimi sina wazo kamili au fikra ya kuweza kuwapa, lakini nashauri kutokana na Muungano wetu tuliokuwanao na

hapa sisi Wazanzibari tuwashukuru viongozi wetu ambao wameshatangulia mbele ya haki, Mwalimu Nyerere na Mzee Karume kwa kuziunganisha hizi nchi, kwa jinsi tunavyozaliana na uhaba wa ardhi tuliokuwa nao na huko mbele tunakokwenda, basi nimuhimu serikali ikatafuta njia ya kupata eneo la ardhi maeneo ya Tanga kuweka, ili ikiwezekana siku za mbele kuweza kusafirisha mawe mchanga kuleta hapa Zanzibar, kwa sababu haiwezekana tukaendelea kutumia mchanga na mawe katika visiwa vyetu, iko siku mchanga huu na mawe itakuwa haiwezekani. *(Makofi)*

Mhe. Spika, pia nataka nitowe wazo langu la tatu kwa kuchangia maoni ambayo yako nje ya kamati yetu. Nakumbuka katika miaka ya baada ya Mapinduzi, wakati Mhe. Rais wetu wa Zanzibar Mzee Abeid Karume alipokutana na balozi mdogo wa China Men Ying, alisema Zanzibar inategemea China sio kama rafiki bali kama ndugu. Sasa ninachotaka kukisema hapa kwa kupitia Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, kumpa wazo la kuanzisha *Zanzibar medal of owner*, medali ya kuwatunuku Wazanzibari katika shughuli na nyanja tofauti. Ni sahihi tunapojaribu kumpa medali mtu wakati wa sherehe za Mapinduzi na nyenginezo za kitaifa, ile medali inakuwa inamezwa na ile shughuli yenyewe. Nashauri tuanzishe sisi wenyewe medali yetu. Tuanzishe medali tatu, unapotoa medali unapata rafiki mpya.

Mhe. Spika, tuchukulie mfano, kwa muda wa miaka mitano ijayo, kila mwaka tukatoa medali tatu. Medali ya kwanza tukampa mkombozi wa Afrika Marehemu Nelson Mandela Rais wa Afrika ya Kusini Mwenyezi Mungu amrehemu. Kwa hivyo, magazeti yatakapoandika kwamba Zanzibar yamtunuku Shujaa wa Afrika, tunapompa medali mkulima bora, basi hapa katika visiwa vyetu watapigania ile medali kila mmoja. Tuweke medali tatu zitakazokuwa hazihusiani na sherehe zetu za kitaifa, ili tuweze kuwatambua mashujaa wetu. Tunatatizo hapa Zanzibar na Tanzania ya kutokuwa na mashujaa na kutowathamini michango yao. Kwa hivyo, tunapowapa medali watu tutapata marafiki wapya, tutaungana na nchi nyingi na kwa muda wa miaka mitano tutazungumza na nchi tofauti.

Mhe. Spika, ndio maana nikazungumza mfano wa China katika mwaka wa 1964 huyo balozi mdogo, ni kwa sababu ya China. Niseme katika historia baada ya Mapinduzi na Muungano wetu sisi Wazanzibari ndio tulikuwa karibu na China, na kutokana na Muungano wetu sisi Zanzibar ndio katika Jamhuri ya Muungano tukaiunganisha Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuwafanya Serikali ya Jamhuri ya China kuwa karibu zaidi na Tanzania, na hadi leo China na Tanzania wamekuwa marafiki wazuri, na ndio wao pia walitusaidia kupata *project* ile ya Tazara kwa mkopo mkubwa wa mabilioni ya

fedha, ambayo Afrika hadi leo ni kitendo cha kihistoria. Kwa hivyo, nashauri hiyo medali Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais uichukuwe, mkaijadilia na muweze kupata mawazo mema.

Baada ya hapo nakushukuru sana Mhe. Spika, ahsanteni kwa kunisikiliza, Mwenyezi Mungu awabariki, ahsanteni sana. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Ahsante Mhe. Simai Mohammed Said Mpakabasi kwa mchango wako. Sasa naomba nimwite mchangiaji wetu mwengine, Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata).

Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata): Mhe. Spika, awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uwezo wa kusimama hapa mbele ya Baraza lako tukufu, kuchangia hotuba hii ya Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, juu ya Ofisi ya Mhe. Rais na Mwenyekiti wa Baraza letu la Mapinduzi.

Mhe. Spika, nampongeza Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, kwa kazi nzuri anayoifanya kuhakikisha kwamba wananchi wetu wa Zanzibar wanaishi katika hali ya amani na utulivu na kufanya shughuli zao bila ya matatizo.

Pili, nimpongeze Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, nimpongeze Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu pamoja na watendaji wote wa taasisi mbali mbali katika ofisi hii.

Mhe. Spika, tunaamini hali ya nchi yetu ilivyo na tunaamini umahiri wa Rais wetu katika kuhakikisha kwamba amani na utulivu ndio mwelekeo wa Zanzibar na wa Tanzania kwa jumla. Kwa hivyo, kwa makusudi nampongeza kwa dhati kabisa, namtakia subra zaidi, utulivu katika mambo yake ili nchi iende salama huko mbele tunakokwenda.

Mhe. Spika, hata katika nyumba zetu au majumbani mwetu, ikiwa pana mtikisiko wa aina yoyote basi nyumba huwa haina baraka. Lakini pia familia inaweza kutawanyika baba akiwa na lake na mama akiwa na lake. Kwa hivyo, pamoja na ustahamilivu aliokuwa nao Mhe. Rais wetu, namuomba kwa dhati kabisa yeye ndiye baba wa nchi hii na yeye ndiye mwenye amri ya mwisho katika nchi hii. Akisema nataka wananchi wote wa Zanzibar wasitoke nje ya nyumba zao, basi hakuna hata mmoja ambaye atakayethubutu kutoka. Kwa hivyo, kwanza heshima ni kitu cha bure na mtu ajielewe analolifanya. *(Makofi)*

Mhe. Spika, mimi kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Kijitoupele, hasa CCM walionichagua na baadhi ya *CUF* walionipa kura zao, nasema tu kwamba lazima tutii amri ya nchi yetu na tuheshimu maamuzi ya nchi yetu na maamuzi ya nchi yetu kila siku mwelekeo wa sera ya Chama cha Mapinduzi ni amani na utulivu ndio mwelekeo wetu.

Mhe. Spika, bila ya hayo hatwendi na bila ya hayo tunaambiwa tu kwamba ustahamilivu una mwisho. Nimuombe Rais pamoja na yote awe mkali kidogo asikae akasema itakuwa hivi, palikuwa na muamsho Mhe. Spika, kila siku ya Ijumaa watoto walikuwa hawendi skuli mjini wanaogopa zahma inayojitokeza, ilianza hivi hivi choko choko ya chini chini kwa hivyo na muelekeo huu sisemi kama muamsho, lakini inaashiria yale yale yaliyotokea huko nyuma. Kwa hivyo niseme tu kwamba tutahadhari kabla halijatokea janga, vyenginevyo hatari itatukabili mbele yetu. Mungu aiondoe isije katika nchi yetu.

Mhe. Spika, katika hali yetu ya utendaji katika Wizara hii niseme tu kwamba Wizara ya Mhe. Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar ina mambo mengi lakini mambo yake yamekusanywa pamoja, kwa hivyo hata kuchangia kwake uwe mtu mtaalam sana ili upate mambo mbali mbali. Kwa hivyo ndio nikasema mwanzo tu kwamba mimi nawapongeza watendaji wote wa wizara hii katika sekta mbali mbali kwa kazi zao nzuri wanazofanya kwa kuhakikisha kwamba mambo yanakwenda bila ya matatizo.

Mhe. Spika, Mhe. Rais ndio tunayemtegemea katika nchi yetu, tunamtegemea Mwenyezi Mungu lakini Rais ndio kiongozi wetu katika nchi hata misikitini tunaambiwa tutajwa kiongozi wa nchi na anatajwa wale waliokuwa hawamtambui hiyari yao lakini yeye ndio mwenye jukumu la nchi hii. Awe kiongozi mzuri aende kwa amani na wenzake katika kuongoza na wasaidizi wake ili tuende vizuri.

Ninaloliomba Mheshimiwa hali ya maendeleo katika nchi yetu tunaitarajia na hali ya nchi yetu iko mikononi mwake Rais na wasaidizi wake ; Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, Waheshimiwa Mawaziri, Manaibu Mawaziri, Wawakilishi wote bila ya juhudi zetu sisi kumsaidia yeye hatwendi, tusitegemee kila kitu atakifanya Mhe. Rais au Rais aje ndio lifanyike. Tunaloweza kulitekeleza tulitekeleze kwa maslahi ya wananchi wetu wa Zanzibar.

Mhe. Spika, Mhe. Rais alipolizindua Baraza letu alitoa kauli nzuri na nampongeza basi kwa sababu yumo katika kuunda Serikali na naamini kauli yake na vitendo vitafuatia pindi litakapotokea hilo baya ninalotaka kulisema, alisema Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano Dkt. John Pombe Magufuli

alitangaza kupasua majibu au kutumbua majipu na anayatumbua kweli kweli, lakini yeye alisema likitokea kwa Zanzibar ikiwa pana uharibifu au ubadhirifu wa aina yoyote kwa kiongozi yeyote au mtendaji yeyote basi lile jipu akishalitumbua na moyo atautoa. Maana kutoa moyo ndio mwisho, maana jipu lisirudi tena maana jipu likitumbuliwa siku nyengine likikaa siku mbili tatu linaweza kurudi, lakini ukikamua ule moyo wake ukitoka haliji tena.

Namuomba sana Mhe. Rais na wasaidizi wake ndio sisi huku tufanyeni kazi kwa moyo wote na panapoleta uharibifu tupakemee au tupaseme au afukuzwe anayehusika, ili twende sambamba katika hali ya uchumi wetu wa nchi yetu na mahitaji yetu yamo mikononi mwetu safari hii.

Mhe. Spika, tunaamini Waheshimiwa Mawaziri ndio wasaidizi wakuu wa Mhe. Rais lakini pia ukenda kwa mapana zaidi kuna Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya na sisi Wawakilishi wa Majimbo mbali mbali na Masheha, na Madiwani pia wamo katika uongozi wa nchi hii. Kwa hivyo niwaombe wenzangu wakati umefika tufanyeni kazi kwa juhudi na maarifa ili maendeleo tunayohahitaji yapatikane.

Mhe. Spika, katika vijana wetu wanaoishi nchi za nje tumeambiwa kwamba katika kitabu hiki kuna utaratibu mzuri umepangwa juu ya kusaidia nchi yao. Mimi naamini Mhe. Spika, kila aliyetoka hapa akenda nje kutafuta maisha na si vibaya na haki yake kwa sababu ni wakati ambao kaona unafaa kwenda kule kwa maslahi yake yeye familia yake na Serikali yake. Kwa hivyo mimi niunge mkono kwa dhati hili na nimuombe Mhe. Waziri vijana hawa wapewe kila msaada, wapewe kila fani waweze kufanya kazi zao vizuri waliko na waheshimu sheria za nchi waliko ili wanachokipata wasaidie huku kwao kusaidia maendeleo ya ndugu zao na wazee wao katika nchi yetu. Hilo si baya na ni zuri linafaa kupewa kila barka ili litekelezeke.

Jengine Mhe. Spika, katika kitabu hiki kuna mambo mbali mbali ambayo yanahusiana na uhusiano wa kimataifa, jambo lolote kwa dunia ya leo huwezi kwenda peke yako bila ya marafiki, mimi niseme tu kwa wale marafiki zetu wa dhati kabisa tuzidi kukaa nao vizuri, kushauriana nao, kuelezana nao ili tupate mahitaji na uhusiano ule ulete mazao mazuri juu ya kusaidia nchi yetu.

Mhe. Spika, Mhe. Rais wa Zanzibar alifanya ziara huko nyuma ya kwenda Vietnam hapa ndipo nitakaposemea kwa sababu Wizara yake inahusika moja kwa moja kwa mambo ya nchi za nje. Bahati nzuri alikutana na Rais wa Vietnam baada ya ziara ile Mhe. Rais wa Vietnam alikuja Tanznia si muda mrefu hapa kwetu na Rais wa Zanzibar, alipata nafasi kuja kuonana nae

Tanzania Bara. Katika jambo kubwa lililozungumzwa na zuri kwa nchi yetu narudia pale pale ushirikiano wa kimataifa, maana yake kutafuta nyanja za kukuza mahusiano na maendeleo. Tuliambiwa tu kwamba wenzetu wa Vietnam wameendelea sana kutokana na mambo ya uvuvi na walisema watatusaidia kwa hali na mali.

Narudia kauli yangu niliyoitamka mwanzo katika Wizara ya Fedha na Uchumi au Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais katika hotuba yake, nilisema tu kwamba Zanzibar tumebahatika kuzungukwa na bahari na naamini kama tutatafuta viwanda na wenzetu marafiki wako kweli waje watusaidie, ili kuinua pato la nchi yetu. Zanzibar ni tajiri Mhe. Spika, na utajiri wake uko mikononi mwetu, tutafute mbinu tu namna gani tutatumia hikma na taratibu zetu ili tukwamuke hapa tulipo, twende mbele zaidi.

Mhe. Spika, siamini hata siku moja na sitegemei hata siku moja kwa nini wavuvi wa nje wanavua katika maeneo yetu haramu yaani wanavua uvuvi haramau, kwa sababu wanakwenda katika sehemu mbali mbali hawana kibali wanachukua samaki hata safari moja, tunasema tu kwamba Mhe. Magufuli aliwahi kukamata meli na samaki wengi wakaitwa samaki wa magufuli, tuliona. Kwa hivyo nimshauri Mhe. Waziri hizi ziara zetu tunapopata marafiki zetu tufanye kazi kwa maslahi ya kusaidia vijana wetu. Kwa sababu kama tutapata vyombo vya usafiri wa uvuvi mkubwa wa kwenda nje tutapata viwanda vizuri vya kusindika samaki wetu, hapo tutafanikiwa katika maisha yetu na kuongeza pato letu la nchi.

Mhe. Spika, wenzetu Tanzania Bara nikiona wale sato kutoka Ziwa Victoria wanasafirishwa kupelekwa nje ya nchi inapata mabilioni ya pesa, sisi tumezungurukwa na bahari katika Zanzibar hii kila pembe, kwa nini tushindwe. Mheshimiwa kutafuta mbinu ni suala la muhimu kwamba mafanikio tunayapata. Kwa hivyo Mhe. Spika, mimi hotuba hii nimesema tu kuchngia kwake utumie maarifa lakini yamo mengi wengine watakuja kusema. Mimi mwenyewe binafsi na kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Kijitoupele jimbo jipya kabisa naiunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia moja na naomba Waheshimiwa Wenzangu waichangie ili kumpa uwezo Mhe. Rais kufanya kazi zake vizuri pamoja na watendaji wake. Nashukuru Mheshimiwa naunga mkono kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf: Ahsante sana Mhe. Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi. Jambo la mwanzo namshukuru Mwenyezi Mungu kama kawaida yetu Waislam tunatakiwa tumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuwa ndiye aliyetuumba na aliyetupa afya. Namshukuru sana na vile vile

nimpongeze Mhe. Rais Dkt. Ali Mohammed Shein kwa ushindi wake mkubwa tuliompa wananchi wa Zanzibar. Vile vile kwa ushirikiano mkubwa aliopewa na Chama cha Mapinduzi kwa ujumla.

Mimi uchangiaji wangu wa leo utakuwa ni mdogo sana kwa sababu sitaki kuzungumza kutokana na hii hotuba au kitabu kilicholetwa kutoka Ofisi yake ni kizuri sana na kipo vizuri kinafahamika na kinaeleweka.

Mhe. Spika, mimi ningeanza kuzungumzia moja kwa moja kwenye yale niliyotaka kuyagusia kwa dakika chache ili niwaruhusu wenzangu waje waendelee kuchangia. Mimi nitaanza na Idara ya Ushirikiano wa Kimataifa na Uratibu wa Wazanzibari wanaoishi nje ya nchi, kwa kweli suala la ushirikiano wa kimataifa ni suala zuri kwa nchi yetu. Mimi ningemuomba Mhe. Rais pamoja na Waziri wake Afisi ya Rais wakaendelea na ziara zao za nje ya nchi. Kwa zile nchi zote wanazohisi wao zitakuwa muhimu sana kwenye kutangaza nchi yetu ya Zanzibar kwa njia yoyote ile, ikiwa ya utalii au biashara.

Ningeomba sana vile vile kwa Mhe. Rais na Ofisi yake kwa ujumla wasingojee tu wapate mialiko kutoka nchi za nje bali wao wenyewe vile vile waandae kwenda nchi zozote wanazohisi nzuri. Nafikiri zimetajwa baadhi ya nchi kama Ujerumani, Vietnam, Turkish na nchi nyengine. Mimi ningependelea zaidi akaangalie nchi ambazo hajawahi kwenda kiziara, inawezekana ameshawahi kwenda mwenyewe kutokana na uwezo wake aliokuwa nao, lakini kwa ajili ya Serikali nchi ambazo hajawahi kufika mfano Taiwan ni matajiri sana na wazuri sana kwenye *aluminum industry*, wako vizuri sana.

Nchi ni nyingi kama mfano Brazil, Rusia hizi ningependelea sana Mhe. Rais akazifikiria hata kama hatuna uwezo, nakubali lakini kila mwaka akajaribu kwenda mara moja mwenyewe binafsi mbali zile anazoalikwa. Mfano mdogo tu ningetoa kama kwa mwaka akasema mimi nakwenda *Europe* nafikiri ni nchi za hapo kwa hapo masafa fulani hata kwa gari umeshafika. Anaweza tu akachagua nchi tano kwenye ziara yake ya mwaka mmoja lakini atakapoanza Ufaransa basi kuna Belgium, karibu kuna Holland, kuna England iko karibu, kuna na Ujerumani ipo karibu. Anao uwezo wa kwenda pale akazitembelea nchi tano kwa pamoja, lakini vile vile lengo ni kuitangaza Zanzibar ikajulikana.

Kuna ndugu zetu wako nje ya nchi miaka mingi, ndugu zetu hawa waliondoka kwa sababu Zanzibar kama tunavyojua Serikali haitoweza kutoa ajira kwa wananchi wote, hata wafanyabiashara hawatokuwa na uwezo wa kuajiri wananchi wote, sasa wananchi hawa wakaamua tu wenyewe kwa njia zao kutafuta na kuondoka kwenda nje ya nchi kutafuta maisha. Lakini vile vile

tuwashukuru wanafanyakazi Uingireza wanafanyakazi Canada , wanafanya kazi Amerika lakini mapato yao yote wanakuja kuwaletea Zanzibar kwa wazee wao hapa. Wamejenga nyumba nzuri nzuri, asilimia 70 au 60 nyumba za hapa Mbweni zimejengwa na watu kutoka nchi za nje ambazo zinavutia sana kwa nchi yetu. Mimi nawapongeza sana na nawaomba vile vile kama wanahisi kuna manufaa zaidi huko basi hapa kwa sasa hivi wasirudi waendelee kuchuma halafu waje wafikirie kuja kufanya biashara hapa Zanzibar, na kujenga vitu vizuri ndani ya nchi yao.

Mhe. Spika, mimi ningetoa kama ushauri tu kwa hawa ndugu zetu kule nchi walizokuwepo Serikali ikajaribu kuzungumza nao, najua kama Serikali yao inakuwepo kwa kule kwamba wana mkubwa wao, kuna kamati fulani lakini wangekuwa wanashirikiana nao na kuwasiliana nao kila muda ili kwa kusikiliza matatizo na changamoto wanazopata wale ndugu zetu.

Vile vile, wasipate vikwazo vigumu vya kuonana na mabalozi kwa sababu kuna baadhi ya nchi hawa Diaspora baadhi yao niliwahi kuonana nao wakalalamika kwamba hata Mabalozi wale wa nchi ambao wanawakilisha Tanzania basi wanapokutwa na tatizo ni vigumu sana kupata msaada kwa kupitia njia ya ubalozi. Sasa kilichobakia pale wanashirikiana wenyewe, wana kama *community* ambayo kafiliwa mtu wa Zanzibar wanaitana mbio mbio wanapeana mchango, wanamaliza suala. Lakini kama balozi na kama nchi ni vigumu sana kukamilisha suala hili, hili suala wameshanambia mimi mwenyewe nimeshakaa nao nchi fulani fulani.

Jengine kwa ufupi kabisa ningeendelea kuzungumza Ofisi ya faragha ya Mhe. Rais nashukuru sana Ofisi hii inamuweka vizuri sana Mhe. Rais na inashirikiana vizuri na Mhe. Rais kwenye kumsaidia kazi zake. Hawa ni watendaji wazuri wa Mhe. Rais hata mimi nampongeza sana ndani ya jimbo langu la Chaani amenijengea tawi langu kubwa amenimalizia ambalo linaitwa Tawi la Mchezashauri na hata wanachama wangu wa Chama cha Mapinduzi na wananchi kwa ujumla, niliwaambia tawi hili mimi naweza nikasema Ikulu kwa Kaskazini kwa sababu ni tawi zuri na kubwa.

Mhe. Spika, nampongeza sana kwa ushirikiano wake wa kuja jimboni kwangu kuja kuzindua suala la umeme Kandwi, ametuletea umeme baada ya muda mrefu kuwa watu hawana umeme, kajitahidi katuletea umeme. Namshukuru sana kwa ukweli wake na utendaji wake mzuri wa kazi.

Sasa ningegusia Idara ya Ufuatiliaji na tathmini, watendaji wake na niwaombe sana washirikiane sana na Mhe. Rais kwa njia ya ukweli na ya uhakika. Kwa

sababu matatizo mengi yanatokezea duniani sana watendaji ndio wanaomharibia jina la Mhe. Rais sio Rais mwenyewe anayejiharibia. Mhe. Spika, Mhe. Rais yeye hatoweza kufanya kila kitu katika nchi yake, ameteua Mawaziri kwa sababu wamsaidie na wale Mawaziri wana Wizara wana Makatibu, wana watendaji kwa sababu wasaidie nchi, wamsaidie na Mhe. Rais ili mambo yaende. Lakini ukiangalia sio wote waaminifu, sitaki kuzungumzia mtu gani wala sehemu gani lakini ninachoomba wale walioaminiwa na Mhe. Rais kusaidia kufanya kazi, basi wamfanyie kazi kama Mwenyezi Mungu anavyotaka na kama Serikali ya Mapinduzi inavyotaka. Wasije wakamwendea kinyume wakamtia jina baya, wasije wakafanya mambo yakaleta jina baya katika Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mhe. Spika, mimi sina zaidi kama nilivyozungumza mwanzo leo nitachangia kidogo sababu imenifurahisha hotuba yake ni nzuri na kitabu chake ni kizuri. Kwa niaba ya wananchi wangu wa jimbo la Chaani wataungana nayo hii asilimia mia kwa mia. Ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi ya kuchangia hotuba ya Waziri wa Nchi Afisi ya Rais, na mimi niwashukuru sana wapiga kura wangu wa jimbo la Chake Chake Pemba, kwa kunichagua kuwa Muwakilishi wao na nawakilisha vizuri tu tukijaaliwa. Niseme tu kwamba nawapa pongezi sana asilimia karibu 80 habari ya mgomo mgomo huu naona wao kidogo wale watu wa pale ni wasomi na wachamungu wanajua sana. Suala hili kidogo wao wameliweka kando na sitaki niwasifu hali ikaja ikaharibika, lakini niwapongeze tu kwa hali hiyo.

Mhe. Spika, mimi niendelee kuchangia hotuba, niseme tu kwamba Mawaziri wetu na Manaibu Mawaziri waliopata nafasi katika kuteuliwa na Mhe. Rais wetu Dkt. Ali Mohammed Shein kumsaidia kuliongoza taifa hili. Mimi nichukue tu kuwapongeza lakini pia kukumbushana kwamba kwa dhamana waliyopewa wanajitahidi sana na wajitahidi zaidi, ili kumpunguzia mzigo na malalamiko ya wananchi kwa vitu hasa ambavyo naweza kusema ameviahidi alipokuwa akizunguka na sisi katika kujinadi na kuwatakia maendeleo mazuri wananchi wake wa Zanzibar.

Kwa hivyo, ningeomba mawaziri walikuwa wajaribu kufatilia vitu ambavyo Mhe. Rais alijitahidi kuzungumza na kuwaambia watu ili watakapomchagua na kumpa ridhaa ya wananchi basi vitu hivyo atavifanya. Kwa hivyo, ningeshauri sana wamsaidie Mhe. Rais vitu vile wavifanye kwa wakati ili mheshimiwa aweze kujinadi tena katika 2020 kwa kumtafutia kura Rais mwengine wa Chama cha Mapinduzi atakayegombea.

Mhe. Spika, jengine Dkt. Ali Mohammed Shein hivi karibuni alikuwa kama na uzinduzi fulani wa michezo Uwanja wa Amani. Mhe. Spika, Mhe. Rais alisisitiza sana uwezekano wa ngoma za asili ziwe ni chimbuko au ziweze kushika kasi na yeye aliahidi kwamba atazichangia kwa hali na mali ngoma zile zirudi au asili ya michezo ile irudi, ili Wazanzibari warudi kwenye haiba yao tuliyotokea. Nilikuwa namnukuu hilo na nilimsikia nilikuwepo Uwanja wa Amani kwa hivyo nikajua kwamba ana harakati hizo, lakini pia alikuwa na harakati za vijana ambao aliwaahidi sana katika michezo hasa ya mpira kuwaendeleza vizuri sana na vipaji vyao na vipaji vingi vingi. Kwa hivyo, ningeshauri Waziri wa Michezo ahakikishe mambo haya ambayo Mhe. Rais amesema hiyo ni amri kwa hivyo vitu hivyo viweze kutekelezeka ipasavyo ili mambo haya yaendelee.

Pia napenda kumshukuru Rais Dkt. Ali Mohammed Shein kwa kuendeleza kuwapenda sana wazee ambao anawajali kwa kuwapa pensheni kidogo ya mwisho wa mwezi, na pia na walemavu katika harakati nyingi anawajali sana na kuendeleza maelekezo yao. Ningeshauri tu ikiwezekana baada ya maendelezo ya kuwapa maposho hawa wazee basi na walemavu nao kama itawezekana hali itaruhusu nao waingizwe kwenye kundi hilo ili waweze kujikimu katika hali ambayo nahisi itasaidia sana.

Mhe. Spika, pia nimsifu Dkt. Ali Mohammed Shein kwa dhamira yake aliyoizungumza mwaka 2005 alipokuwa anaingia madarakani ya kujenga mashule mapya. Mhe. Spika, shule zile zimejengwa vizuri sana na zipo zinaendelea vizuri sana kila pahala unaoneshwa maeneo ambayo shule zile aliziahidi watu wengi hawakufikiria, lakini shule zipo na kwa kweli nampongeza sana kwa shule zile ambazo ni za kisasa na zina uwezo wa kutoa wataalamu wazuri sana.

Mhe. Spika, vile vile nizungumzie masuala ya mazingira kwa kweli masuala haya Zanzibar sasa hivi yanatuburuza, hali ya mazingira imekuwa hata miongo yetu ya mvua inakuwa haipatikani. Mheshimiwa nilikuwa nizungumze tu kwamba zile wizara ambazo zilikuwa za Makamu wa Kwanza wa Rais nilijaribu kuziangalia nyingi hapa ambazo zimemfikia Makamu wa Pili wa Rais katika kipindi cha miaka mitano hii zimefanya vibaya kidogo hazikuwa nae. Tulizungumza suala la ukimwi tulisema limeongezeka, suala la madawa ya kulevya limeongezeka, suala la mazingira ndio hali halisi hiyo, Mji wa Zanzibar ni mchafu maelekezo mengi hayakutendeka vizuri. Mimi ningeshauri sana wizara iliyopata bahati ya kuyachukua mazingira hayo kwa sasa hivi ikafanya kikweli sio ifanye kimazingira mazingira ambayo ni hatarishi kweli kweli.

Kwa hivyo, mimi mheshimiwa niongeze kwa sababu ya kupandisha mishahara kwa Dkt. Ali Mohammed Shein asilimia mia kwa mia. Hii nilikuwa na hofu kwamba Mhe. Rais ana nia nzuri sana ya kuwaongezea kipato cha chini kwa asilimia mia juu ya mishahara. Mheshimiwa hofu yangu ni kwamba wafanyabiashara wetu wanafanya vibaya hiyo biashara itaanza kupanda tena mara mbili yake, ile faida ya asilimia mia iliyotakiwa kumsaidia yule mtu ambaye ana kipato cha chini hali ile huwa haimsaidii zaidi inakuwa ni matatizo.

Sasa ningeshauri sana mfumko wa bei ukaweza kudhibitiwa angalau kwa nyanja tofauti tofauti za vile vitu ambavyo maana yake ndio vitu ambavyo ni vitu mama vinavyotumika. Kama vile mchele, sukari, unga, vitoe na mambo mengine ambayo binadamu anatakiwa kila siku ayatumie mambo haya basi mfumko wake wa bei ungeweza kubanwa au kushushwa kama kutakuwa na vitu vya anasa na starehe vikaongezeka bei kwa sababu hivi kila binadamu anavihitaji ni lazima aweze kuvipata.

Mhe. Spika, pia niweze kusema tu kwamba namshukuru pia Dkt. Ali Mohammed Shein kwa kupandisha mishahara, lakini cha msingi ningeomba tu kama hali itaruhusu Waziri wa Fedha na sisi wenyewe tukifanya kazi kwa ziada ahadi imeshatolewa ya Aprili kwamba watapandisha mishahara. Kama itawezekana kwa wananchi wake Mhe. Rais anavyowapenda tukashusha angalau Januari kama itawezekana ili tukapunguza muda kidogo ili wananchi wakapata kujikimu kwa haraka kidogo. Lakini kama haiwezekani ndio ahadi imeshatoka hakuna tatizo, hakuna umbali na huo Mwenyezi Mungu atatujaalia tutafanikiwa kwa hali na mali.

Mhe. Spika, mimi nasema Mhe. Rais amesisitiza sana kuhusu habari ya afya. Mheshimiwa afya kwa kweli upande wa Zanzibar bado viwango vyake havijatufikia, kila mmoja anayeumwa anapanda ndege, anapanda boti anakwenda Dar es Salaam tena wasi wasi wangu sio majengo ya afya, sio majengo ya kitu gani matatizo ni madaktari. Mhe. Spika, mimi nilivyokuwa nakumbuka hata kama ilikuwa sio sababu zenyewe madaktari bingwa wengi tulikuwa tukitoa nchi za nje ambazo ni nchi wahisan. Marafiki zetu kama Cuba, China na nyingi Urusi basi mimi nafikiri bado Zanzibar hatujaweza kujikimu kwa madaktari, bado madaktari wetu hawajakuwa na uwezo mkubwa na pia ni wachache.

Kwa hiyo, ningeshauri tu na nikamshauri Mhe. Rais akazungumza na hawa watu tukapata madaktari wa kuja kutusaidia katika hali hiyo kupunguza tu huu msongomano wa kwenda Dar es Salaam, kwenda kufa, kwenda kuhangaika

madaktari wakiwepo hapa itasaidia sana. Mimi ningeshauri zaidi kama kutakuwa na madaktari bingwa basi wakae pale hospitali ya Chake Chake maana yake ile ndio hospitali iliyopo *centre* kwa upande wa Pemba.

Mhe. Spika, vile vile kuhusu suala la mazingira, ni kwamba Chake Chake kwa kweli Zanzibar ni ndogo, miji inayoringia ni miwili. Inaringia Mji wa Mjini Magharibi na unaringia Mji wa Chake Chake Pemba, haidhuru kuna Mkoani, kuna Wete, kuna maeneo ya Nungwi. Lakini miji hii miwili ndio kioo cha nchi na ndio dira yenyewe inapofikia wageni wote.

Mhe. Spika, mji wa Zanzibar naujua kwamba una vigezo na mambo mengi unatiliwa pesa, unafanywa nini Mji Mkongwe, mheshimiwa Chake Chake nayo ina magofu, ina mambo yake yanataka kufanywa. Kwa hivyo, ningeshauri tu Mji wa Chake Chake ukatizamwa kwa jicho la huruma, kwa jicho la mapenzi sana kuanzia barabara zake pale za Msingini zikasafishwa, ikajengwa kisasa yenye mantiki nzuri na ule mji wenyewe ndio wenye maofisi yote hayo maofisi yakatengenezwa, maofisi yakapigwa rangi yakawa mazuri ule mji wenyewe ukawa unatikisika ukishuka Pemba ndio mji wenye *airport*, ndio mji mkuu pale pakakidhi haja kamili kabisa katika hali hiyo.

Mhe. Spika, mimi niseme tena pale Chake Chake tunaudhia, tuna matatizo pia ya *parking* na hasa eneo hili la mazingira ambalo liko huku chini Tibirinzi ambalo kwa haiba ya kizamani sasa hivi tumeingiwa na suala la mikoko. Mikoko pale imejaa mpaka imefikia pahali watu hawana pakuogelea, hapana sehemu ya kupunga upepo, sehemu ya Tibirizi imejaa mikoko enzi hizo maeneo yale walikuwa wakipelekwa Chuo cha Mafunzo wakiiong'oa na kusafisha na kuweka vizuri ili wananchi waweze kupunga upepo na kuogelea. Jioni watoto ilikuwa ni sehemu yao ambayo inafuatana hii mpaka kwenye sehemu ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais iliyoko Chake Chake maeneo yale yote yalikuwa safi na yalikuwa ya kupendeza. Mheshimiwa sasa hivi yameachwa pori, yameachwa uchafu na kwa kweli siingilii habari ya mazingira ya mikoko na kila kitu, lakini bado kuna haja ya kutizama zaidi suala hili, kwamba mikoko ni bora au bora mji wenyewe wa kuvutia na maeneo yake.

Mhe. Spika, lile eneo kama tutaliweza kuliweka vizuri itakuwa ni kama Forodhani ya pili ambayo badala ya Forodhani ya Mjini basi Forodhani ya pili itakuwa iko Chake Chake ni eneo zuri sana, limejipanga vizuri ukiangalia unaiona Misali ndio sehemu ikajengwa Ikulu kwa sababu inapendeza kweli kweli.

Mheshimiwa sasa hivi sehemu ile imekufa, sehemu ile imekuwa pori, imekuwa chafu hapaeleweki hivyo ningeishauri sana ofisi ya mazingira ikatizama kwa kina eneo lile vipi tulifanye ili liweze kupendeza, sio tufate mikoko tu, mikoko iko tele wewe ukizunguka Pemba nzima ni mikoko, lile eneo tungeliweka usafi tukalishughulikia kabisa.

Mhe. Spika, niseme na maeneo mawili, Ofisi ya Rais ina nguvu na ndio yenye kila kitu. Mheshimiwa na jumba la sinema la Chachani, lile jumba lishakaa hatarishi, lishakaa muda mrefu, halina viwango, halijuulikani mwenyewe limekaa hatarishi ni hatari kweli kweli. Ningeishauri wizara inayohusika ikatoa vielelezo vya kutosha kuhusu suala lile, lile jengo likajuulikana mwenyewe. Lile jengo likajuulikana kutengenezwa au lile jengo likajuulikana livunjwe ipatikane sehemu kubwa ya kujengwa kitu cha maana cha serikali hii. Ningeshauri hilo.

Mhe. Spika, jambo la pili nizungumzie pale Tibirinzi tuna jengo letu moja Wizara ya Fedha ni bovu limekosa viwango, lishavunjika, lishaleta hasara na tunalitizama labda liko kwenye kesi, labda liko kwenye mambo gani. Mimi ningeshauri Rais akaliingia suala hili ndio tunasema utakosa mwana na maji ya moto. Mheshimiwa lile jengo siku litakaloanguka mwenyewe basi ile hifadhi ya jamii nayo itakwenda na maji, kwa sababu limeegemea upande ule na lishaachia na watu wa hidhadhi *ZSSF* wamekaa tu wanatizama.

Basi mimi nasema tusifate ule msemo wa Kinyamwezi unaosema kwamba nilikuwa namuangalia tu, tutizame kwa kina lile suala lifanyweje ili lile jengo kama ni kuporomolewa liporomolewe na kama serikali imeshaingia hasara iingie lakini itafute suluhishe la lile eneo kwani ni hatari kwa kila hali. Kwa hivyo, hilo nilikuwa nalisemea sana kwamba linaweza kusaidia.
Mhe. Spika, kabla sijamaliza mchango wangu nilikuwa nasema, kwamba Mhe. Rais ana nia nzuri sana na wananchi wake na mimi ningependa tu kuwaasa, kuwaomba wananchi wote wa Zanzibar tumuunge mkono Dkt. Ali Mohammed Shein kwa nguvu zote yale makusudio aliyoyakusudia aweze kuyafanya bila ya vikwazo vyovyote.

Sisi tukianza kumtia vikwazo halafu itakuwa hatujasaidia kitu na yeye ni mtu ambaye kwa kweli nimshukuru sana na nimtakie kila la kheri kwa sababu mheshimiwa mimi najua kukaa na watu katika nyumba moja ambayo inakuwa katika makabila tofauti inakuwa ni tatizo kubwa. Mhe. Rais wa Zanzibar amekaa na vyama katika serikali yake kwa muda wa miaka mitano, amekaa na Makamu kutoka Chama cha CUF, amekaa na Makamu kutoka Chama cha Mapinduzi na mawaziri tofauti, mheshimiwa hakubagua aliwaendeleza watu

wale amekaa nao kwa wema na mimi nikamshukuru nikasema kwamba sifikirii kama tutapata kiongozi mwadilifu kama Dkt. Shein.

Mhe. Spika, kabla sijasema chochote naunga mkono hoja asilimia mia kwa mia namtakia kheri na nawatakieni kheri nyote. Ahsante sana mheshimiwa. (*Makofi*)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, muda wa asubuhi utakuwa umemalizika kwa sababu hizi dakika chache zilizobaki hazimtoshi mchangiaji anayefuata kuweza kuchangia. Waheshimiwa napenda niwakumbushe tu wakati mnapochangia mjaribu ku-*focus* kwenye bajeti ya hii wizara msiende nje sana. Baada ya hayo nasitisha shughuli za Baraza mpaka saa 11:00.

(Saa 6:50 mchana Baraza liliahirishwa mpaka saa 11:00 jioni)

(Saa 11:00 jioni Baraza lilirudia)

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Mhe. Spika, kwanza nishukuru kwa kunipa nafasi jioni hii ya leo kuwa mchangiaji wa mwanzo wa bajeti hii ya Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

Mhe. Spika, kwanza niwapongeze viongozi wa wizara hii kwa kuanza na Mhe. Waziri kaka yangu Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu), Katibu Mkuu wa wizara hii na watendaji wake kwa bajeti waliyotuletea mbele yetu. Ni bajeti nzuri inayoonesha mwelekeo mzuri wa Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar katika Ofisi ya Rais Ikulu.
Mhe. Spika, naomba niende kwenye kutoa mchango katika ukurasa wa 23 kwenye Programu ya Uratibu na Ushirikiano wa Kikanda na Mashirika ya Kimataifa. Katika bajeti iliyopita tuliona hapa kwa mujibu wa kitabu hiki kulitengwa fedha shilingi 389.7 milioni, lakini matumizi au kilichoingizwa ni shilingi 23.5 milioni.

Mhe. Spika, kwangu katika uhalisia wa programu hii katika utekelezaji wake unanitia mashaka sana, kwa sababu eneo hili lina mikutano mbali mbali na kitabu kimeonesha kuwa wameshiriki mikutano mbali mbali na ninavyoelewa mimi katika programu hii ni pamoja na ushiriki wa mikutano ya *SADC*, Mashirikiano ya Bahari ya Hindi *IORA* na utatu kama walivyoeleza humu katika kitabu chao kuwa *SADC*, *EAC* na *COMESA*.

Mhe. Spika, uelewa wangu na ufuatiliaji wa mambo haya ya Afrika Mashariki na katika huu utatu waliouzungumza humu na *IORA* iko mikutano mikubwa inafanyika wanahudhuria Marais, iko mikutano mikubwa inafanyika wanahudhuria mawaziri, lakini iko mikutano ile ya *technician team* ambayo mara nyingi ndio huandaa yale mambo ambayo viongozi wetu wakuu wanakwenda kukutana. Kama sikosei katika eneo hili katika ufuatiliaji wangu *SADC* mawaziri katika nchi za jumuiya hii wanakutana mara moja kwa mwaka sambamba na Marais.

Katika utatu wanakutana pia mara moja kwa mwaka lakini Marais wanakutana mara mbili. Sasa sijui kwa bajeti hii na ndio maana nikasema napata mashaka, ninaizungumzia ili kuona Mhe. Waziri kwa sababu ni mpya katika wizara hii lakini Katibu Mkuu ni mtendaji ambaye yupo kwa kipindi kirefu najua tutapata majawabu mazuri, lakini tuone vipi ushiriki wetu katika eneo hili.

Mhe. Spika, ninayasema haya kwa sababu leo hii tunashiriki humu katika jumuiya hizi kesho kutwa tu, tukipitisha bajeti mpya mambo mengi yatazidi kwa sababu tutakuwa tunashughulikia masuala ya kimataifa wenyewe. Kwa hivyo, kabla hatujafika huko na ndio maana nauliza hapa, akija Mhe. Waziri anambie katika taasisi hizi nilizozitaja kwa maana ya *SADC*, utatu wa *SADC EAC* na *COMESA* katika maeneo mawili sina tatizo na *technician team* zile zinazokutana. Nina tatizo la mawaziri na Marais kushiriki kwao wakiwemo hawa wa kwetu tunaowajadili hapa na Marais wa kwetu ndio ambao tunawajadili hapa, ushiriki wao katika eneo hili wameshiriki mara ngapi na kama hawajashiriki ni kwa nini.

Kwa sababu kuwemo katika jumuiya vikao vikawa vinafanyika na bajeti inatengwa na matumizi haya kama tunavyoyaona ni shilingi 389.7 milioni wametumia 23.5 milioni mimi napata mashaka kweli, ndio maana nikaona leo sitaki nichangie sana kwenye bajeti hii kwa sababu najua wizara ina wataalamu wametufikisha pahala pazuri, lakini kuna maeneo na sisi tupate kujua kwa faida ya wenzetu.

Mhe. Spika, nije katika Programu ya Uratibu wa Serikali kwa Wazanzibari wanaoishi nje ya Nchi. Nayo tumeona bajeti iliyotengwa ilikuwa shilingi 112.1 milioni, matumizi waliyoyapata ni shilingi 95.1 milioni. Bajeti hii naamini iliombwa pamoja na mishahara na shughuli ambazo zimepangwa.

Mhe. Spika, moja ya shughuli ambazo waliziainisha katika bajeti iliyopita kuwa ni uandaaji wa sera ya *DIASPORA*. Juzi nilichangia kidogo lakini nikasema nasubiri pia itapofika bajeti ya wizara husika ndio niseme hasa.

Namshukuru sana Mhe. Waziri amenipa jawabu nzuri na za uhakika na nimeridhika. Namshukuru sana kaka yangu Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu) kwa majibu yake yale ya juzi, lakini alinijibu tu kuwa sera tayari imeshatayarishwa sasa sijui niendelee kuiuliza wizara hii matumizi ya sera hii baada ya kukamilika imeshaanza, kama bado kwa nini.

Pili, miongoni mwa shughuli zake katika programu hii niliyazungumza juzi na leo naendelea kuyazungumza moja ni kuwatambua Wazanzibari waliokuweko nje ya nchi, pili kuwashajihisha na tatu kuwapa malengo yale ambayo tutaungana nao katika kuisaidia nchi hii. Kwa hiyo, naamini kwa kipindi chote cha kazi hii iliyofanywa na pesa iliyotengwa tayari tumewatambua. Sasa labda nimuulize Mhe. Waziri atakapokuja anithibitishie mpaka sasa kitengo hiki kimeweza kuwatambua wangapi. Lakini la pili tumeshirikiana nao katika mambo gani mpaka sasa.

Vile vile kwa sababu tuna kazi ya kuwatambua lazima tutakuwa tumeandaa *data base* ambayo tumewawekea, labda waje watueleze mfumo mzuri ambao tunakwenda nao na kushughulikia Wazanzibari hawa waliokuweko nje ya nchi.

Ofisi ya Faragha. Mhe. Spika, nimeona pia katika kitabu hiki kuwa Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi tarehe 2 Machi, 2016 alihudhuria mkutano Arusha. Katika mkutano huu waliweka kwa wanachama wote wanajumuiya wa mkutano huu, walijadili na kuweka malengo ya kiuchumi 2050 (*Twenty fifty*). Sasa hapa napo pamenipa mashaka kwa sababu sisi tuna masuala yetu ambayo tunajipangia ndani ya kiuchumi na ndio maana tukatengeneza *mission* na *vision* na tunao mpango wetu tunaokwenda nao. Sasa napata mashaka kidogo aje aniweke sawa kuna mshabihiano gani wa lile walilokubaliana kwa mujibu wa kitabu hiki 2050 na ile 1520 ambayo tunakwenda nayo sisi, mana tusije tukaingia pahala ambapo hata huo uchumi wetu ulipofikia.

Mhe. Spika, mwisho kwa sababu kitabu hiki maeneo mengi kimenifilisi sasa nikasema nichangie maeneo madogo lakini iwe ni faida ya kuuliza kwa sababu ya jamii yetu. Jumuiya yetu ambayo tunashiriki ya Afrika Mashariki ni jumuiya ambayo sisi ni wanachama na tunashiriki katika mambo mbali mbali ya kiuchumi. Ziko nguvu za kiuchumi tunaziweka tunapeana mikakati na kila mmoja akirudi katika nchi yake anatekeleza.

Wenzetu wana jumuiya kama hii wametengeneza hapa *foreign policy* yao, wanapokwenda wanatumia ile moja wanapotoka nje kwa maana kama *European Union* wanayo *foreign policy* yao. Sasa sisi katika Jumuiya ya Afrika

Mashariki hii tunayo *foreign policy* ambayo tunaitumia tutakapotoka katika eneo letu hili la Afrika Mashariki kwenda katika nchi nyengine za nje. Ili sote tuwe na sauri moja katika nchi hizi, tunatetea kitu kimoja, lakini pia kama sisi waheshimiwa humu tuna safari nyingi ambazo tunategemea kuzipata pengine za binafsi pengine basi Baraza litatoa nafasi hizo basi tukienda kule tuone kama kuna *foreign policy* ambayo inatumia Jumuiya ya Afrika Mashariki inazungumzia nini na tukakizungumze kile ambacho kimo ndani ya jumuiya yetu.

Mhe. Spika, mimi leo kitabu hiki kimenifilisi sana lakini maeneo hayo matatu nikasema nichangie kwa udogo wake lakini pia kwa umuhimu mkubwa. Naomba niwapongeze tena viongozi wa wizara hii, lakini kwangu pia nitamke kuunga mkono bajeti hii kwa asilimia mia moja. Mhe. Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia jioni ya leo.

Mhe. Suleiman Makame Ali: Mhe. Spika, ahsante nashukuru kwa kunipa nafasi hii ya jioni ya leo nikiwa ni mmoja wapo wa kuchangia katika hotuba hii ya Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

Mhe. Spika, mimi sitaki niseme mengi sana kwa sababu hii hotuba imejengeka kusema kweli, ni hotuba ya aina yake na ni hotuba ya mfano. Vile vile niwape pongezi zangu za dhati wale wote walioshiriki kuandaa hotuba hii, wote kwa ujumla.

Mhe. Spika, mimi niende katika suala la kuwapa pencheni wazee, hii ni ahadi ya Rais ambayo Mhe. Rais aliahidi kuwapatia pencheni wazee wetu waliofikia umri wa miaka 70 na kuendelea. Mimi hili naliunga mkono na ni suala zuri sana na kwa Tanzania nadhani sisi Wazanzibari ni wa kwanza kuliko Tanzania Bara kule kwa wenzetu.

Mhe. Spika, niseme kwamba naiomba ile wizara husika ya Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto iwe makini sana na suala hili la kusimamia pencheni ya wazee. Kwa sababu Mhe. Rais ameliahidi hili isijekuwa kama masuala ya *welfare*. Wale wazee wanaopokea shilingi 5000 hata kama atakuwa mtu keshafariki lakini ile pesa inachukuliwa, lakini sasa hapa hii wizara niiombe iwe makini sana kulisimamia hili na kuonekana kwamba hizi pesa hazipotei na kumpa nguvu Rais wetu ili kuhamasika zaidi na hawa wazee wetu.

Mhe. Spika, kuna hiki kitengo cha kuratibu shughuli za Mhe. Rais katika hii ofisi, niiombe ofisi hii iwe makini sana katika kufuatilia ahadi anazozitoa Mhe. Rais kwa sababu hapo ndio kila kitu, iwe makini na ifuatilie ahadi hususan zile

alizozitoa kwenye kampeni ya kuomba kura kwenye uchaguzi mkuu wa mwaka 2015; ahadi zile nyingi alizozitoa zinatekelezeka. Kwa hiyo, niiombe ofisi izichukue ahadi zile na izifanyie kazi ili wananchi wetu wawe na imani na Rais wao na aonekane kuwa ndiye bora kwa sababu ahadi zote zinakamilishwa kwa wakati kama zilivyopangwa.

Mhe. Spika, kuhusu suala la ziara Pemba. Hili suala la ziara nalo pia ni zuri sana kwa kule Pemba hususan kwa wakati huu mgumu tulionao, ipo haja Mhe. Rais kufanya ziara kule Pemba mara kwa mara kwa sababu ndio kama hivyo tunavyoona hali za Pemba atakapokwenda Mhe. Rais pengine huenda yale mambo yalioko kule yakapungua kutokana na zile kasumba zinazopelekwa na wenzetu. Kwa hiyo, niiombe ofisi iangalie na suala hili ili kumshauri Mhe. Rais kwenda kule Pemba mara kwa mara.

Mhe. Spika, mimi sitaki niseme mengi kwa sababu hii hotuba kusema kweli sikuona vyema kuwa nisisimame kuchangia tu, lakini hotuba iko vizuri sana ni hotuba ya aina yake niseme haijawahi kutokezea. Kwa sababu hotuba kama hii basi wakati mwengine wale watu wa kuchangia huwa kidogo, kwa sababu yote yaliyosemwa humu ni masuala kusema kweli kama ya kuweka sawa tu. Kwa hiyo, mimi naipongeza tena ofisi hii naiomba iwe makini sana na ahadi zote zile alizoziahidi Mhe. Rais wazifuatilie na wazifanyie kazi.

Mhe. Spika, naunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia moja na kama kuna asilimia nyengine za ziada basi naongezea.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Mhe. Spika, ahsante sana na mimi Hassan Khamis Hafidh wa Jimbo la Welezo kunipa nafasi hii jioni hii ya leo kuchangia hotuba ya Mhe. Waziri mpya wa Ofisi ya Rais Ikulu na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

Mhe. Spika, nami niungane na wenzangu hasa Mhe. Suleiman Makame Ali alivyosema ameangalia kitabu hiki kwa jinsi kilivyopendeza na maneno yalivyoandikika kwa umakini na umahiri wa bajeti hii iliyowasilishwa leo. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kwa kweli na mimi nichukue fursa hii kumpongeza sana Mhe. Waziri kwa kuteuliwa kushika nafasi hiyo kubwa ya uwaziri Ofisi ya Rais Ikulu. Lakini pia naomba nichukue fursa hii kuwapongeza watendaji wa ofisi hii kwa kushirikiana nae katika kuleta hotuba nzuri iliyopangia, kuanzia Katibu Mkuu ndugu Salum Maulid Saluma kwa mashirikiano anayoyatoa na Mhe. Waziri.

Kadhalika Katibu wa Rais, Naibu Katibu wa Rais, Mkurugenzi wa *Diaspora* na Wakurugenzi wote. Mhe. Spika, lakini bila ya kuwasahau washauri wa Rais ambao wanamshauri Mhe. Rais kila siku pamoja na watendaji wake wote wa Afisi ya Rais Ikulu na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. (*Makofi*)

Mhe. Spika, pia napenda nichukuwe fursa hii ingawaje naona mwenye hajafika kumshukuru aliyekuwa Waziri wa Afisi ya Rais Ikulu na Utawala Bora wakati ule Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame Mwadini. Sababu ya shukurani hizi ni kwamba na mimi nilipata fursa ya kuwa pale kama mtendaji kwa kweli alitulea vizuri. Alikuwa anatushauri vizuri na leo hapa Barazani sote ni mashahidi hasa wapya tulioingia kwamba mshauri wetu na mwalimu wetu hapa Barazani ni Mhe. Mwinyihaji Makame, anatushauri vizuri, anatulea vizuri na anatuongza vizuri na tumuombee dua Mwenyezi Mungu ampe moyo huo huo wa kutulea na kutuongeza. (*Makofi*)

Mhe. Spika, sasa naanza kuchangia hotuba yangu, Mhe. Spika, Ikulu nitanukuu maneno ya Mwalim Julius Nyerere alisema kwamba:-

"Ikulu ni pahala patakatifu" kwa maneno hayo utakatifu wake ndio maana Ikulu zote duniani zina rangi nyeupe kwa sababu ya utakatifu wake. Sasa mimi ni tegemeo langu kwamba kutokana na utakatifu wake na ukubwa wa Afisi ya Rais Ikulu, maana yake zipo Afisi nyengine za Rais lakini ile ni maalum ni Afisi ya Rais Ikulu, ni pahala patakatifu na mambo yake yote yanatakiwa yawe matakatifu.

Sasa Mhe. Spika, kwa kweli kuna mambo pale Ikulu ambayo namuomba sana Mhe. Waziri ayasimamie na ayashughulikie nayo yainuke yawe matakatifu. Mfano Mhe. Spika, mtendaji wa Ikulu Afisa mfano ana *Master degree*, ana uzoefu wa miaka 20 lakini kimshahara anapitwa na dereva wa Shirika la Bima. Sasa hapo unaweza ukaona tafauti baina ya mtendaji wa Ikulu na dereva wa Shirika la Bima haiendani na ule utakatifu wa Ikulu na mtendaji wa Shirika la Bima kumpita kimshahara ambaye ni dereva. Namuomba sana Mhe. Waziri hebu aliangalie hili.

Kadhalika mtendaji dereva wa Ikulu nawaombea sana watendaji wote waangaliwe kwa jicho la rehema. Dereva wa Ikulu asifanane na dereva wa taasisi nyengine yoyote nchi hii, lazima anapotokea ajulikane huyu ni dereva wa Ikulu kutokana na kivazi chake na mambo yake. Lakini ili afikie huku madereva hawa na watendaji hawa wanahitaji kuwezeshwa.

Mhe. Spika, kama mtendaji wa taasisi nyengine anapewa posho la nguo au viatu kwa mwaka laki mbili kutokana na utakatifu wa Ikulu ni lazima basi apewe wa Ikulu mara mbili yake kama kule wanapata laki mbili kule wapate laki nne. Ili anapoingia pahali pale patakatifu awe na yeye mtakatifu, awe *smart*.

Mhe. Spika, bila ya kuficha baadhi ya watu wanaingia Ikulu na ni watendaji wa Ikulu wakiwa wachafu bila ya kuficha hasa ukizingatia pale ni pahala patakatifu. Lakini ukiwauliza wanakwambia kweli bwana pesa zinazowezeshwa kununua nguo ni kidogo. Kwa hivyo, Mhe. Spika, na mimi nilikuwa mtendaji pale kwa heshima kubwa na taadhima kubwa nawaombea wenzangu wawezeshwe, kwa sababu pale ni pahala patakatifu na wao ni lazima wawe tafauti na idara na taasisi nyengine zote za serikali. Pale ni Ikulu mtendaji wake lazima aonekane ki -Ikulu.

Mhe. Spika, kwa utakatifu wa Ikulu anaealikwa na kuingia Ikulu nae lazima aende *smart* . Kuna mzee mmoja anaitwa mzee Ali alinambia mwaka wa 1971 yeye alialikwa Ikulu na Mzee Abeid Aman Karume basi alikuwa na kaunda suti ikabidi aipeleke kwa Goa mjini kwenda kupigwa pasi, kwa jinsi alivyothamini ile hadhi ya kualikwa Ikulu na alivyopathamini pale mahali penyewe. Lakini leo ndani ya Ikulu unamkuta mtu kavaa viatu vya kuparaza, anaingia Ikulu.

Mhe. Spika, namuomba sana Mhe. Waziri ni kijana wa leo alisimamie hili, la ziada hata mtu mtendaji wa serikali anaalikwa bango kitita kuonana na Rais, basi hutambui kavaaje, kaja pahali patakatifu yeye mwenyewe kaja mchafu. Mhe. Spika, namuomba sana Mhe. Waziri Ikulu ni pahala patakatifu asiingie mtu mchafu, kambi ya Jeshi tu huingii mtu ukiwa mchafu. Lakini nashangaa sana Ikulu anaingia mtu mchafu, anaingia na viatu vya kuparaza humtambui kama huyu mtu anafanya kazi gereji na hapa ni Ikulu.

Kuhusu hoja ya watendaji Mhe. Spika, mauomba sana Mhe. Waziri mtendaji akisha wezeshwa kupewa pesa za kwamba anunue nguo na avae ili awe *smart* pale Ikulu na kama hafanyi hivyo mimi namuomba Mhe. Spika, asiwe na muhali amuhamishe na ampeleke karakana, akafanye kazi karakana ndio kunako watu wachafu, pale ni Ikulu.

Baada ya hayo Mhe. Spika, naomba kusema sasa kuna sera ya *Diaspora*. Mimi nina ushahidi kwamba sera ya *Diaspora* haijesha. Sasa namuomba sana Mhe. Waziri aniambie lini sera ya *Diaspora* itakwisha na itaanza kutumika.

Mhe. Spika, Ikulu ina idara huku nje umaarufu inaitwa jumba la "*ZIPA*". Kama nilivyoeleza mwanzo kutokana na utakatifu wa jumba lile za *ZIPA* bado halina hadhi ya kuwa ni taasisi ya takatifu katika hii nchi Ikulu. Nakuomba sana Mhe. Waziri yaboreshwe mazingira ya pale ili yaendenae na hadhi ya ki- Ikulu, bado hapana hadhi ya ki- Ikulu.

Mhe. Spika, kadhalika naomba kuchukuwa fursa hii kumuomba sana Mhe. Waziri Ikulu ni pahala patakatifu, lakini hamna nyenzo za walemavu kuweza kupita na ile ni nyumba ya wote. Mlemavu akienda Ikulu anapata shida na hatakiwi apate shida, anatakiwa apate shida kwengine lakini asipate shida Ikulu katika kuingia kupata huduma. Naomba sana hili litizamwe na lifanyiwe kazi.

Mhe. Spika, sasa nakwenda katika Idara ya Ushirikiano wa Kimataifa na Uratibu wa Wazanzibari wanaoishi nje ya nchi. Mhe. Spika, idara hii ilikuwepo zamani ilikuwa inaitwa Idara ya Ushirikiano wa Kimataifa na Uratibu Uchumi. Baada ya kuja Rais wa awamu wa saba Dkt. Mhe. Ali Mohammed Shein akabadilisha jina akaita Idara ya Ushirikiano wa Taifa na Uratibu wa Wazanzibari wanaoishi nje ya nchi.

Mhe. Spika, idara hii ina *units* nne, *unit* ya kwanza ni *protocol*. Mhe. Spika, naomba kuchukuwa fursa hii kwa masikitiko makubwa, tayari pale Ikulu ipo *unit* ya *protocol* lakini masikitiko yangu kwamba Mhe. Waziri anahudhuria katika vikao mbali mbali akiwa hana *protocol* na wale Mambo ya Nje Zanzibar wanakuwa hawaendi. Kwa hivyo, Mhe. Rais hatua ya kuwa na *protocol PACU* wanafanya kazi ya *protocol* kitu ambacho si kazi yao wana kazi yao. Naomba kumuomba Mhe. Spika, kwamba lazima umefika wakati *unit* ipo na naomba iwezeshwe na iweze kufanya kazi yake ya kuweka *image* ya Mhe. Rais katika suala zima la *protocol*.

Mhe. Spika, kuna *unit* nyengine pale inaitwa *unit* ya Ushirikiano wa kikanda. Kazi yake kubwa ni mtengamano wa kikanda na kuifanya Zanzibar ishiriki vikao pamoja na faida zitokanazo na mtangamano wa kikanda, vikao vya *SADEC, Indian-Ocean Rim Association* na vikao vya *EAC*.

Mhe. Spika, naomba sana na vikao vya *African Union* idara hii iwe inashiriki. Kwa sababu wenzetu wa Bara wanashiriki kwa nini Zanzibar iwe haishiriki. Mhe. Waziri aje anijibu kwa nini *AU* tunakuwa hatushiriki na sisi pia tumo katika Afrika tunatakiwa tushiriki. Lakini kikubwa naomba sana Mhe. Spika, kule vinavyozungumzwa vina faida wasibaniwe hawa kupewa pesa kushiriki vikao hivi kwa sababau vikao hivi vinafaida kwa maendeleo ya Zanzibar.

Chengine Mhe. Spika, naomba kumuomba Mhe. Waziri umefika wakati sasa si kuhudhuria vikao tu lakini tufaidike na zile *projects* zinazotokana kule, bado tumefaidika na *project* moja tu mimi ndio ninayoijua kujengwa kwa Baraza la Kiswahili la *East African Community* pale Eacrotanal . Lakini kuna *projects* nyingi zote zinakwenda Bara na sisi Zanzibar ni sehemu ya Muungano wa Tanzania. Umefika wakati sasa na sisi tupate hizi *projects* zisiende Bara tu. Njia zote *East Africa* zimejengwa Bara na sisi ni wanachama kama ni Watanzania na kwa nini hata barabara moja haijajengwa Zanzibar, Mhe. Waziri aje anijibu hili.

Pia Mhe. Spika, kuna Idara ya Ushirikiano wa Kimataifa pale, kazi yake kubwa ni ushirikiano wa kimataifa na kuweka *image* ile *International Cooperation*. Namuomba sana Mhe. Waziri Taasisi za Kimataifa ziko nyingi Bara nilifanya *research* nikakuta kuna taasisi 324 Zanzibar ziko chake. Hii ni kutokana na muamko mdogo tulionao niliweza kuitia *IOM, UNHCR* na taasisi nyingi za kimataifa na tumepata faida kubwa kutoka kwao.

Naomba sana Mhe. Spika, idara hii iendelee kuzitafuta na kuzishajiisha Taasisi za kimataifa zenye malengo ya kusaidia maendeleo zije wazialike kushirikiana na Wazanzibari katika kutafuta maendeleo endelevu.

Mhe. Spika, nitatoa mfano Shirika la Kiengereza ambalo linatoa huduma kwa nchi maskini kama Zanzibar. Kuna *Plan International*, mashirika haya yako mengi. Umefika wakati sasa Mhe. Spika, tuyatafute tuyashajiishe na yaje kusaidia Zanzibar.

Mhe. Spika, sasa naingia katika *unit* ya *Diaspora*, naomba kidogo nitoe elimu kwa sababu mimi ni mwana *Diaspora*. Watu wengi inaposemwa *Diaspora* hujiuliza huyu ndie mdudu gani na wengine wanaita maneno chungu mzima. Maana yake ni Raia wa nchi fulani wanaoishi nje ya mipaka ya nchi yao. Lakini sifa zake lazima awe ana mashirikiano na nchi yake anayotoka, akiwa hana mashirikiano mtu huyu basi si *Diaspora*, anaitwa mkimbizi.

Mhe. Spika, nchi nyingi za Kiafrika zinao raia wanaoishi nje baada ya utafiti kufanywa, utafiti umebaini raia wa nchi za Kiafrika wanaoishi nje zamani walipewa majina tafauti kama wasaliti, wakimbizi lakini wana faida na nchi zao wanazotoka, kwa sababu wanatuma, wanachukuwa yale mapato zile nchi walizofikia wanayaleta kwao. Kwa Zanzibar tulifanya utafiti tukagundua dola milioni moja kila mwezi zinakuja Zanzibar kutoka kwa wana *Diaspora* hizi zinakuwa *official*, zinazokuja *unofficial* kwa njia ya *panya road* ni karibu dola za kimarekani milioni tatu. Lakini pia Afisi ya Takwim ilifanya utafiti ikabaini

asilimia 12% ya kaya za Zanzibar zinaishi kutokana na kutengemea kipato cha ndugu zao na jamaa zao wanaoishi nje ya nchi.

Mhe. Spika, Zanzibar kuna kaya laki mbili na hamsini kaya thatathini na saba elfu chakula chao cha kila siku kinatokana na wana *Diaspora*. Nini unajifunza, unajifunza kwamba hawa raia za Zanzibar wanaoishi nje ya nchi kumbe wana umuhimu mkubwa kwa sababu wanawasaidia kuwapa maendeleo raia wenzeo.

Mhe. Spika, sifa ya ma-*Diaspora* wengi wanaoishi nje aghalabu huwa ni wapinzani. Mhe. Rais wa Zimbabwe Robert Mugambe alisema *" You are the people of Zimbabwe but you do not know the struggle of Zimbabwe, but you are friend of Zimbabwe, you helped Zimbabwe during the struggle of Independence ...".* Akiwa na maana kwamba nyinyi kila siku mnakaa nje mnaisaliti Zimbabwe lakini mnasaidia Zimbabwe, kwa hivyo, nyinyi ni wana Zimbabwe na nyinyi nitakusaidieni aliwapa uraia wa nchi mbili.

Mhe. Spika, naomba sana Mzanzibari anaeishi nje ya nchi leo hii hapa Zanzibar anakuwa akija kama mgeni na hapati *good treatment,* anakuwa sawa sawa na Muengereza aliezaliwa Scotland tu kwa sababu anamiliki *passport* ya nje.

Mhe. Spika, namuomba sana Mhe. Waziri sera ya *Diaspora* imalizwe kwa haraka ili iweze kutoa mwanya kwa wana *Diaspora* kushiriki maendeleo ya Zanzibar na wanapokuja nchini kwao wasiwe kama wageni wengine.

Mwisho kabisa Mhe. Spika, naomba kusema kwamba Zanzibar tunao ma-*Diaspora* wengi wako Oman, Uengereza, Marekani, Canada. Lakini kuna swali maarufu je, Wazanzibari wanaoishi Tanzania Bara wale ni wana-*Diaspoara*, hilo ni swali ambalo watu wengi hatuna jibu.

Mhe. Spika, namuomba sana Mhe. Waziri sera ya *Diaspora* ina umuhimu mkubwa na wana *Diaspora* wote wako tayari kuchangia, lakini kutokana na kutokumaliza kwa Sera ya *Diaspora* leo hii *Milele Foundation* wanapata shida kwa kupata *visa* hapa nchini na wanasaidia Zanzibar bilioni tatu, wamesaidia maskuli na mahospitali mbali mbali. Lakini hatuwezi kuwagaia *visa* ya ukaazi. Anakaa miezi inambidi atoke ende Kenya arudi tena hiyo sio sahihi. Mhe. Spika, waswahili wamesema "Abebwae hujikaza".

Mhe. Spika, baada ya hayo machache namtakia kheri nyingi Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais Ikulu. Nawatakia kheri sana watendaji wote wa Afisi ya Rais Ikulu. Lakini mwisho kabisa napenda kuchukuwa fursa hii kumpongeza

Mhe. Waziri na mimi nimeikubali hotuba hii mia kwa mia na kumuomba aendelee na *spirit* hiyo hiyo na atafika. Ahsante. *(Makofi)*

Mhe. Rashid Makame Shamsi: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kwa kunipatia nafasi alau niseme machache katika kuichangia hotuba hii ya Mhe. Waziri wa Nchi katika Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

Kabla sijasema hayo ningependa nitoe shukurani na pongezi za dhati kwa Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa hekima na busara katika kuiongoza nchi hii.

Vile vile nichukuwe fursa hii kumpongeza Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa uwasilishaji mzuri wa hotuba hii ambayo imepangia vyema, isingekuwa sawa kuchangia lakini nimehisi kuna mambo mawili matatu ambayo ningetaka ufafanuzi.

Niipongeze sana kamati ambayo iliwasilisha masuala yanayohusiana na afisi hii na nichukuwe fursa nimpongeze sana Mhe. Simai Mohammed Said (Mpaka basi) kwa uwasilishaji wake mzuri. Niwapongeze vile vile Wajumbe wote walonitangulia kwa michango yao mizuri. (*Makofi*)

Mhe. Spika, nina machache ya kuweza kuchangia katika bajeti hii ya Ofisi ya Rais. La kwanza nielekee katika programu ya kusimamia shughuli za Mhe.Rais na kuimarisha mawasiliano Ikulu kwenye ukurasa wa 28.

Kuna kifungu kinachohusiana na ufuatiliaji na utekelezaji wa ahadi na maagizo ya Mhe. Rais. Kwanza nichukue fursa hii kumpongeza sana Rais wetu wa Zanzibar, kwa kuwa muadilifu, kwa kuwa ni mkweli katika kutekeleza ahadi ambazo anazitoa zenye mstakabala wa maendeleo ya nchi hii. Ikiwemo ahadi ya ujenzi wa mitaro ya kutoa maji machafu ambao mradi wake umo ndani ya Jimbo langu la Magomeni. Nimshukuru sana. (*Makofi*)

Mhe. Spika, Mhe. Rais alitoa ahadi na ameitekeleza ya ujenzi wa Tawi la CCM pale Wandarasi katika Jimbo langu la Magomeni. Nimshukuru sana. Lakini Mhe. Spika, katika ujenzi huo ambao haujakabidhiwa rasmi una mapungufu kidogo katika ujenzi huo ambayo hayakamilika ikiwemo miundo mbinu ya vyoo, kuungwa kwa umeme na vibao vya madirisha.

Mhe. Spika, katika eneo letu hili. Kuna wale ambao hawapendelei maendeleo hususan ya Chama cha Mapinduzi, wameanza kupenyeza mikono katika madirisha hayo na kuzivunja *plugs* na *switches* zote ambazo zimo ndani ya tawi

hilo. Mhe. Spika, ningemuomba Mhe. Waziri atakapokuja kufanya majumuisho aweze kuniwekea sawa kwamba ujenzi huo wa tawi umefikia mwisho hautoendelea, kwa sababu sisi viongozi tuloingia madarakani pale tuna ari kubwa ya kuweza kulimaliza jengo lile. Kwa hivyo ningependa ufafanuzi na ikiwezekana kama umefikia mwisho basi tupate maandishi kamili ili na sisi tutie mkono wetu, kwa kulimaliza jengo hili na hatimaye tumualike Mhe. Rais kuja kulifungua. (*Makofi*)

Mhe. Spika, sasa nielekee kwenye suala zima la ujenzi wa nyumba za Ikulu na nyumba za serikali. Kwanza nipongeze juhudi za serikali kupitia Ofisi hii kwa kufikiria kuweza kuyafanyia ukarabati majengo ya Ikulu na majengo ya nyumba za serikali zilizo chini ya Ofisi hii. Mhe. Spika, ninaelewa kwamba miaka ya nyuma kulikuwa na nyumba nyingi za serikali ambazo zilikuwa pembezoni mwa fukwe katika sehemu mbali mbali za visiwa. Nyumba hizi zilikuwa zinatumika na viongozi wa serikali kwa kupumzika. Hivi sasa baadhi ya nyumba nyingi sana zitakuwa ni chakavu.

Vile vile inawezekana baadhi ya nyumba zimeuzwa. Kuna nyumba Makunduchi, Jambiani, Paje, Fumba na kadhalika. Ningependa Mhe. Spika, Mhe. Waziri atakapokuja atwambie nyumba hizi ambazo zimebakia zipo chini ya Ofisi yake ni ngapi, na ni ngapi ambazo zimeuzwa na kwa gharama gani na nani ameuziwa. Vile vile ningemuomba kwamba zile ambazo bado zimebakia ni ngapi na vile vile ningemuomba azifanyie ukarabati, kwa sababu hivi sasa nyumba hizo nyingi zimechakaa.

Mhe. Spika, nimalizie michango yangu katika programu ya kuratibu ushirikiano wa kikanda na mashirika ya kimataifa kwenye ukurasa wa 23 na 24. Mhe. Spika, imeelezwa katika bajeti hii au kitabu hichi kuna Kamisheni ya Kiswahili ambayo Makao Makuu yake yapo hapa Zanzibar katika majengo ya *EACROTANAL*.

Mhe. Spika, moja kati ya mambo ya mashirikiano na nchi za kikanda, hili ni suala moja ambalo tunakupongeza sana alau na sisi Zanzibar kuweza kufikiriwa kuwa na kituo au taasisi ya kimashirikiano katika nchi yetu. Lakini ningependa Mhe. Waziri atakapokuja kufanya majumuisho aweze kutwambia kwa faida ya wananchi, Kamisheni hii ya Kiswahili ina wafanyakazi wangapi wa Zanzibar. Kwa sababu uzoefu unaonesha kwamba katika mashirikiano haya basi Zanzibar tunapata nafasi ndogo sana ya uajiri. Pamoja na pengine kukodisha majengo yetu ni manufaa gani mengine ya kiuchumi, ya kijamii na ya kiutamaduni ambayo tunapata Zanzibar kutokana na kuwepo kwa Kamisheni hii katika visiwa vyetu.

Mhe. Spika, baada ya michango hiyo michache, ningependa kuishukuru tena Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuweza kuwasilisha hotuba hii nzuri, iliyopangika lakini vile vile niwatakie watendaji wote ambao walishirikiana na Mhe. Waziri kwenye uandaaji na hatimaye uwasilishaji wa hotuba hii. (*Makofi*)

Mwisho na mimi nitamke rasmi kwamba naiunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia. Ahsante sana. (*Makofi*)

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Rashid Makame Shamsi. Sasa naomba nimwite Mhe. Yussuf Hassan Iddi na Mhe. Bihindi Hamad Khamis ajiandae.

Mhe. Yussuf Hassan Iddi: Mhe. Spika, ahsante na mimi jioni ya leo kuweza kunipa fursa hii ya kuweza kutoa mchango wangu katika hotuba ya Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

Kwanza kabisa sina budi nimshukuru na kumpongeza kwa dhati kabisa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa umakini na ueledi wake mkubwa wa kuiongoza nchi yetu. Sisi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi tunamwambia kwamba tupo pamoja naye katika harakati za kuleta maendeleo ya nchi yetu. (*Makofi*)

Mhe. Spika, pia nimpongeze Mhe. Waziri kwa namna ya pekee ya uwandaaji wa kitabu hichi ambao kwa uwoni wangu nimeona kiko tofauti na kile kilichopita. Kwa hivyo ninampongeza Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake kwa kuweza kuandaa bajeti hii. Bajeti ni nzuri na safi na ndiyo maana Wajumbe wengi hawakuweza kuichangia.

Mhe. Spika, mimi nianze kwenye ukurasa wa 5 wa kitabu hiki. Kwenye majukumu ya Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi katika Kifungu cha 6 kusimamia utekelezaji wa shughuli za Ofisi ya Baraza la Mapinduzi (*GSO*). Ofisi hii ni muhimu sana katika mustakabali wa nchi yetu na kazi yake kubwa sana na kufanyia ukaguzi kabla na baada ya uajiri wafanyakazi wa SMZ.

Kwa uwoni wangu kwa kipindi cha miaka mitano iliyopita, naona Ofisi hii imeachwa nyuma sana na wakati majukumu yake ni makubwa kweli kweli. Kwa hivyo namuomba Mhe. Waziri Ofisi hii aipe kipaumbele ili iweze kutekeleza majukumu yake kama kawaida. Ukiangalia kitabu hiki kwenye ukurasa wa 39 katika utekelezaji wa mapitio ya bajeti, chini huku katika Ofisi ya Usalama wa Serikali (*GSO*). Utakuta kwamba bajeti yake ni milioni

thalathini na saba nukta tisa tu. Siyo kama hizi pesa zote zimepatikana ni asilimia 37 tu ya bajeti yake ndiyo zilizopatikana. Ukiangalia bajeti ya mwaka 2016/2017 ni milioni arobaini. Ni fedha kidogo sana. Wakati hizi milioni arobaini kwa taasisi nyengine ni *OC* ya mwezi mmoja au miezi miwili lakini taasisi hii inapewa mwaka mzima.

Kwa hivyo nimuombe tu Mhe. Spika, Mhe. Waziri atakapofanya majumuisho anieleze ni kwa nini Ofisi hii muhimu na nyeti lakini bajeti imekuwa ndogo na hata ufanisi wake umepungua. Ukitazama katika kitabu kikubwa hiki cha Fungu AO1 ukurasa 8, chini huku utakuta kwamba kwa mwaka 2015 ilifanya upekuzi wa awali wafanyakazi watumishi 80, lakini mwaka huu wapo 200. Kwa hivyo hii yote imetokana na kwamba uhaba wa bajeti kwa taasisi hii na ni muhimu kwa mustakabali wa nchi yetu.

Mhe. Spika, niende kwenye ukurasa wa 30 katika programu ya ushirikiano wa kimataifa. Mhe. Spika, kwanza nitoe shukurani kwa Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kumpa nafasi Rais wa Zanzibar kwa kumuwakilisha nchini Comoro kwenye sherehe za kumuapisha Rais wa nchi hiyo. Hivyo kwa mara ya kwanza toka tumalize uchaguzi Mhe. Rais wa Zanzibar amepata mualiko wa kwenda nchini Comoro. Lakini hapa nilikuwa nimuulize Mhe. Waziri kwamba je, heshima aliyopata Rais wa Zanzibar kule Comoro inastahiki. Hivyo naomba utakapofanya majumuisho anipe ufafanuzi.

La pili, tumeona kwamba katika awamu iliyopita Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Jakaya Mrisho Kikwete anapofanya safari za nje, basi anachukua Wawakilishi kutoka Zanzibar ambapo wanaungana na msafara ule wa safari za nje. Lakini hapa vile vile Mhe. Waziri nataka nikuulize kwamba Mhe. Waziri Mkuu alipokwenda Lusaka Zambia kwenye mkutano wa ADB. Je, Zanzibar tulipata ushiriki huo.

Makamu wa Rais alipokwenda Afrika Kusini. Nani aliyetuwasilisha katika msafara wa Makamu wa Rais. Kwa hivyo masuala haya naomba Mhe. Waziri ili niweze kupitisha bajeti hii, basi naomba unipatie ufafanuzi.

Ukija katika ukurasa wa 31 kwenye programu ya utumishi na uendeshaji wa Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwenye ufuatiliaji na tathmini ya sera na maamuzi ya serikali. Hapa ninataka nipongeze tu serikali kwa uamuzi wake wa kuanzisha Idara hii ya Kufuatilia na tathmini ya sera na maamuzi ya serikali. Kwa sababu serikali ina sera nyingi na maamuzi mengi yanayotolewa lakini kulikuwa kunakosekana kitu kimoja, yaani utekelezaji. Kwa hivyo kuwepo kwa taasisi hii, sera nyingi zile ambazo zimekwama na

maamuzi mengi yale ambayo yamekwama katika serikali yetu, basi yanaweza yakatatuka. Hivyo niipongeze sana serikali kwa uamuzi wa kuanzisha taasisi hii.

Mhe. Spika, niende kwenye ukurasa wa *34 paragraph* ya 88 *roman (iii)* ambayo inaelezea Bango Kitita. Nimpongeze tu Mheshimiwa awamu ya saba kwa kuanzisha utaratibu huu wa Bango Kitita. Nia yake ni nzuri tu. Lakini niiombe serikali kwamba baadhi ya watendaji wa serikali siyo waaminifu, wakishapata ratiba ya Bango Kitita wanajifungia wiki nzima ofisini mwao, wanapika taarifa, halafu wanawasilisha kwa Mhe. Rais. (*Makofi*)

Sasa niiombe tu serikali kwamba baada ya kumaliza vile vikao vya Bango Kitita, basi kuwe na ufuatiliaji ili kujua usahihi halisi wa zile taarifa zilizotolewa na zile wizara. Kwa sababu kwa sasa hivi tunaona baada ya vile vikao vya Bango Kitita kumalizika, hakuna ufuatiliaji wowote, yanakuwa yale yamekwisha. Na pale taarifa inayowasilishwa inakuwa ni nzuri tu lakini kumbe uhalisia katika wizara ile husika ukenda, yale mambo yote yanakuwa hamna. Tumesema sasa tunataka tubadilike, *business as usual* hatutaki katika awamu hii ya pili ya Awamu ya Saba. Kwa hivyo tunaiomba sana serikali kwamba ihakikishe taarifa za Bango Kitita basi zinakuwa ni halisia na zenye ukweli. (*Makofi*)

Mhe. Spika, ukija ukurasa wa 39 kwenye mapitio ya utekelezaji wa bajeti ya 2015/2016 pamoja na mapendekezo ya bajeti ya 2016/2017, hapa kidogo Mhe. Waziri atakapofanya majumuisho naomba anipe ufafanuzi kwa nini baadhi ya idara bajeti zipo chini na wakati zina majukumu makubwa. Kuna Idara ya Mipango, Sera na Utafiti ambayo kwa mwaka huu wa fedha ambao tunaoujadili wa 2016/2017 zimepangwa milioni mia tatu nukta nane. Karibuni milioni sitini na saba zimepunguzwa ukilinganisha na bajeti ya mwaka jana. Kwa hivyo kwa nini bajeti hii Idara ya Mipango, Sera na Utafiti ni idara nyeti, ina mipango mingi na ndiyo roho ya wizara zimepunguzwa pesa hizi. Kwa hivyo ninataka nijue.

Idara ya Mawasiliano Ikulu. Bajeti iliyopita ya 2015/2016 bajeti yake ilikuwa ni milioni mia mbili na kumi na saba. Lakini kwa mujibu wa kitabu hichi 2016/2017 utakuta bajeti yake ni milioni mia mbili. Kwa hivyo kuna upungufu kama wa milioni kumi na saba nukta nne. Idara hii unaweza ukasema ndiyo chombo ambacho kinaleta mawasiliano kwa jamii. Hata kuna maelezo huku imechapisha majarida mengi tu kwa mwaka uliopita na kuelezea utekelezaji wa ilani pamoja na ahadi za Mhe. Rais. Kwa hivyo kuipunja pesa. Maana yake zile ahadi za Mhe. Rais zitakuwa hazijulikani. Watashindwa hawa kuweza kufanya

machapisho, kuandaa vipindi. Kwa yote ni jukumu lao. Kwa hivyo kwa nini pesa hapa zimepunguzwa na wakati majukumu yake yapo mengi.

Mwisho tu Mhe. Spika, ninataka nipate ufafanuzi. Mhe. Rais tunajua kwamba ana washauri wa mambo ya uchumi, mambo ya nje, mambo ya mila na sanaa. Hawa washauri kwa kweli ni kama *link* ya zile fani ambazo wanazitumikia pamoja na Mhe.Rais. Sasa nilikuwa ninataka kujua kwamba je, hawa washauri wanakutana kule na wadau wa zile fani zao kabla ya kuonana na Mhe. Rais. Kama wanakutana mikutano mingapi ya washauri wamefanya na hawa wadau ili na wao kutoa *input* zao katika kuijenga nchi hii.

Kwa sababu nchi hii haiongozwi na mtu mmoja. Mawazo ya watu tofauti tofauti yanaunganishwa pamoja, yanawasilishwa na ndipo tunakwenda mbele. Kwa hivyo Mhe. Spika, Mhe. Waziri utakapofanya majumuisho basi nilikuwa naomba ufafanuzi kwa hawa washauri wa Mhe. Rais.

Baada ya maelezo hayo. Mhe. Spika, mimi naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja na kumi kwa hotuba hii.

Ahsante sana. (*Makofi*)

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Yussuf Hassan Iddi. Sasa naomba nimwite Mhe. Bihindi Hamad Khamis.

Mhe. Bihindi Hamad Khamis: Mhe. Spika, ahsante na mimi kunipa nafasi ya kuweza kuchangia bajeti hii ya Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

Kwanza kabisa nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, kunijaalia leo hii nikaweza kuchangia jioni hii ikiwa ni mara yangu ya mwanzo kuweza kuchangia kwenye hotuba ya bajeti ya Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. (*Makofi*)

Kwanza kabisa nianze kumpongeza Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Nimpongeze Katibu Mkuu Kiongozi, Katibu Mkuu wa Ofisi ya Rais pamoja na watendaji wake wote.

Mhe. Spika, kwa kweli bajeti hii ambayo imewasilishwa na Mhe. Waziri leo hii ni bajeti ambayo ameielezea kwa kina na ina ufanisi wa hali ya juu. Tuna matumaini makubwa sana kama bajeti hii ndiyo dira ya 2016/2017.

Mhe. Spika, kwanza kabisa nimpongeze Mhe. Rais kwa hatua ambayo ameichukua kwa kuweza kufanya ziara kwenye Kisiwa cha Pemba ili kuweza kuonana na wananchi ambao wana hali ngumu ya kisiasa.

Nikiendelea na mchango wangu kwenye bajeti hii, ingawaje bajeti hii nimeeleza mwanzo kama imetoshelezeka na kwa ufanisi wa hali ya juu, sitokuwa na mchango mkubwa sana, nitaeleza machache yanayohusiana na bajeti hii jumla kwa jumla.

Mhe. Spika, mimi kwanza nimpongeze Mhe. Rais kwa kuweza kubuni na kuweza kuyatengeneza majengo ya Ikulu Pemba. Kama tunavyojua majengo yetu ya Ikulu Pemba mengi yalikuwa ni mabovu, lakini kwenye programu hii imeonesha kwamba itakuwa na ufanisi wa hali ya juu ili kuweza kutekeleza majukumu yake ya serikali pamoja na kuona wananchi wa Pemba na Unguja wanayaona majengo yao yakiwa ni ya serikali na ya Ikulu yanaendelea vizuri. (*Makofi*)

Pia nimpongeze Mhe. Spika, Mhe. Waziri na hotuba hii ambayo ameelezea kuwa wataliendeleza jengo la *Rest House* ambayo ipo Wilaya ya Micheweni na Jimbo la Micheweni. Ninataka nisema kwamba Mhe. Spika, jengo hili la *Rest House* iliopo Micheweni ni muda mrefu sana. Mhe. Waziri nilikuwa ninataka kwenye majumuisho yako uje unieleze ni mwaka gani jengo hili lilianza kujengwa na ni mkandarasi gani aliyepewa jengo hili kujenga na halikuweza kumaliza kwa muda wa kipindi cha 2010 hadi kufikia 2015. Mhe. Spika, pia jengine ni kitu gani kilichosababisha kama Rest House hii ifikie mpaka 2016 kama haijamalizika. (*Makofi*)

Mhe. Spika, jengine nimpongeze Mhe. Rais kwenye safari yake aliyokwenda Ujerumani, aliambatana na wajasiriamali wa visiwa viwili vya Unguja na Pemba. Pia nimpongeze Rais kwa kufanya hivyo kwa sababu alifanya hivyo kwa ajili ya kuviunganisha visiwa viwili vya Unguja na Pemba ili wajasiriamali waweze kufaidika na wachukue hatua kwa yale waliyokwenda kujifunza kuja kuwaelimisha wenzao ili waweze kufuatilia majukumu ya wajasiriamali kwa kujikwamua kwenye umaskini. (*Makofi*)

Mhe. Spika, nikiendelea mbele kwenye bajeti hii. Kwa kweli nimesimama hapa kuweza kumpongeza lakini ninamuomba Mhe. Waziri yale yote niliyomuuliza aje anipe ufafanuzi wa hali ya juu, kwa sababu suala hili la *Rest House* ya Micheweni ni suala sugu sana. Anieleze kwa kina ili niweze kufahamu nijue kwamba wananchi wangu wa Micheweni watafarajika na suala hili. (*Makofi*)

Mhe. Spika, nikiendelea kwenye bajeti hii niwapongeze sana washauri wa Rais na viongozi wote ambao wanashirikiana na Mhe. Rais kumpa maelekezo ili kuweza kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi zaidi.

Mhe. Spika, nimesema sitokuwa na mchango mkubwa, ila kama sikusimama itakuwa sikuitendea haki wizara hii.

Mhe. Spika, ahsante sana. (*Makofi*)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe huyo ndio aliyekuwa mchangiaji wetu wa mwisho. Sasa kwa sababu bado tunao wakati na Mhe. Waziri atahitaji kwenda kuwasiliana na watendaji kabla ya kuja kufanya majumuisho ili kuja kukuleteeni majibu yaliyo sahihi. Nitamuomba sasa Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Makamu wa Pili wa Rais ili aweze kutoa hoja ya kutengua kanuni ya muda na ili tumpe nafasi sasa Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi aweze kwenda kufanya *consultation* na watendaji wake ili aweze kuja kujumuisha kesho asubuhi hapa.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Makamu wa Pili wa Rais hebu tusaidie kidogo.

KUAHIRISHA BARAZA KABLA YA WAKATI WAKE

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, kwa kuwa wachangiaji wa hotuba ya Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na kwa kuwa Mhe. Waziri anahitaji muda wa kutosha ili aweze kutoa majibu sahihi yatakayokidhi matakwa ya Waheshimiwa Wajumbe.

Kwa hivyo Mhe. Spika, naomba tuweke kando Kanuni ya Muda ili tuweze kuahirisha Baraza lako hili kwa leo mpaka kesho tarehe 01/06/2016 saa 3.00 asubuhi barabara na yeye Mhe. Waziri atakuwa amepata muda wa kutosha wa kujitayarisha na kujibu hoja.

Naomba kutoa hoja.

Mhe. Spika: Ahsante Mhe. Waziri. Waheshimiwa hoja imetolewa. Sasa naomba niwahoji wale wanaokubaliana na hiyo hoja wanyanyue mikono, wanaokaa. Waliokubali wameshinda. (*Makofi*)

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Spika, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

(Saa 12:03 jioni Baraza liliahirishwa hadi tarehe 01/06/2016 saa 3:00 asubuhi)